**31 JANUARI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA NNE**

**Kikao cha Pili – Tarehe 31 Januari, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi Mbunge wa Lushoto sasa aulize swali lake.

Na. 21

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Gare - Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za ujenzi katika Kituo cha Afya Gare?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Jimbo la Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilipeleka kiasi cha shilingi milioni 18 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la kutolea huduma za nje *(OPD)* katika Kituo cha Gare.

Mheshimiwa Spika, Serikali itatuma timu ya Wataalam kufanya tathmini ya eneo na mahitaji halisi ya ujenzi wa Kituo cha afya Gare ili Wananchi wa Kata ya Gare wapate huduma za afya. Baada ya tathmini hiyo Serikali iko tayari kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye kata zote za kimkakati kote nchini ikiwemo Kata ya Gare.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri. Huu ni mwaka wa tisa majibu ni haya haya na nakumbuka mwaka jana Bunge la Bajeti Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI alisimama na kusema Kituo cha Afya Gare kimetengewa na kitaanza kujengwa muda wowote. Wananchi walifurahi na walimpongeza Rais na mimi mwenyewe kwa kazi kubwa tunayoifanya huku Bungeni.

Je, kwa kauli ya Waziri nataka kujua ni lini Kituo cha Afya Gare kitatengewa fedha? Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wananchi wa Kijiji cha Chumbageni Kata ya Ngulwi walijenga zahanati ikafikia mtambaa wa panya yaani kwenye lenta na Serikali iliwapa shilingi milioni hamsini. Wakati wanasubiri maelekezo shilingi milioni hamsini zile zilihamishwa na viongozi wa halmashauri.

Je, ni nini kauli ya Serikali kurudisha fedha hizo zilizoondolewa na viongozi wa halmashgauri katika Zahanati ile ya Chumbageni? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shekilindi, la kwanza hili ni lini fedha itatengwa kwa ajili ya Kituo cha Afya Gare. Nikirejea katika majibu yangu ya msingi kwamba timu ya wataalamu itakwenda Gare na kufanya tathmini na kuona vile vigezo vilivyowekwa ikiwemo idadi ya wakazi wa kata hiyo na vigezo vingine vya kuweza kupata kituo vcha afya kama vimetimia.

Mheshimiwa Spika, vikiwa vimetimia Serikali itatafuta fedha na kuzitenga kwa ajili ya kuwajengea Wananchi wa Kata ya Gare kituo chao cha afya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shekilindi amekuwa akilifuatilia sana suala hili namtoa mashaka kwamba Serikali itafanya hiyo tathmini na kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la Kijiji cha Chumbageni ambacho kilipekewa shilingi milioni hamsini na Serikali kwa ajili ya kuunga mkono jitihada za wananchi za kujenga zahanati. Fedha hizi zilitolewa na Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenda kuwaunga mkono wananchi katika nguvu kazi waliyoiweka. Sasa kama fedha ile ilihamishwa maana yake ilienda kinyume na namna ambavyo wenyewe waliomba walipoleta takwimu kule halmashauri na Serikali kupeleka fedha.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi natumia nafasi hii ndani ya Bunge lako hili tukufu kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Lushoto kuhakikisha fedha hizi shilingi milioni 50 zilizotolewa na Serikali Kuu zinarejeshwa mara moja katika Kijiji cha Chumbageni

ili kuweza kumalizia maboma ya zahanati ambayo wananchi walijenga wenyewe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, anasema miaka tisa bado Serikali inatafuta yaani kutafuta fedha ni suala lingine lakini kujiridhisha kwamba kama kata inahitaji kituo cha afya au hapana sidhani kama hilo litachukua miaka tisa. Hebu mjibu Mheshimiwa anasema ameuliza hili miaka tisa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nakiri kwamba tathmini hii ilifanyika mara ya kwanza na ikagundulkika Kata ya Gare ilikuwa ina wakazi elfu 12 katika kipindi tathmini ya kwanza inafanyika ambapo bado ilikuwa haikidhi vigezo vya kuweza kupata kituo cha afya. Vilevile, Kata ya Gare Mheshimiwa Shekilindi atakuwa ni shahidi, ipo kilomita 15 kutoka hospitali ya wilaya kipindi hicho wakati tathmini inafanyika.

Mheshimiwa Spika, hivyo ninaposema tathmini iatafanyoika tena maana yake timu itaenda kuona sasa mazingira yamebadilika idadi ya wakazi na kadhalika ili Serikali iweze kutafuta fedha na kurtenga kwa ajili ya kuweza kujenga kituo cha afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Zahanati ya Kiloleni Wilaya ya Busega imepandishwa hadhi kuwa kituo cha afya, haina wodi za kulaza wagonjwa na haina *theater.* Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kujenga majenga majengo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali itapeleka fedha pale ambapo upatikalnaji wake utakuwepo na tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha

kuona ni namna gani tutapata fedha ya kupeleka Halmashauri ya Wilaya ya Busega kwa ajili ya kujenga hiki Kituo cha Afya ambacho kimepandishwa hadhi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Kituo cha Afya cha Ngongowele kilipewa fedha shilingi milioni 250 za Fedha za Matokeo Makubwa Sasa lakini mradi huu tunaambiwa ume-*phase out*. Je, ni lini Serikali itatuletea fedha kumalizia kituo kile cha afya Ngongowele?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie Bunge lako tukufu hili kumuelekeza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Lindi kwenda katika Kituo hiki cha Afya cha Ngongowele ambacho kilipelekewa shilingi milioni 250 na kufanya tathmini na kuona ni kiasi kinahitajika kwa ajili ya kumalizia majengo ya kituo hiki cha afya pale Ngongowele na kuwasilisha taarifa hiyo Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili Serikali iweze kuona na kuweka katika mipango yake ya kutafuta fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii, kwa kuwa Serikali ina mpango wa kujenga Kituo cha Afya Lyabukande katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga; je ni lini itapeleka fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu, Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali itatafuta na kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Lyabukande kadiri ya upatikanaji wa fedha hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, kwenye Mkutano wa Kumi na Tatu Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa alipitisha fomu kwa Wabunge wote kututaka kujaza kituo cha afya ambacho kila Mbunge angependa kijengwe; je, nini kauli ya Serikali ni lini fedha hizo zitaletwa ili vituo hivyo vya afya vijengwe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu, Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mhata, fomu zile Waheshimiwa Wabunge walipojaza maeneo ambayo wao wangetamani vituo hivi vijengwe timu ilitumwa kwenda kufanya tathmini. Tathmini ile imekamilika katika yale maeneo na sasa taarifa ile imeshawasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, fedha hiyo kwa sasa Serikali inaitafuta kwa ajili ya kuweza kuifikisha katika maeneo ambayo Wabunge waliomba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa Bunge lililopita Mheshimiwa Waziri huyu huyu aliahidi kwamba Kata ya Kitulo itapewa kituo cha afya; je, ni lini mtapeleka fedha ili kituo cha afya kianze kujengwa pale Matamba?

**SPIKA:** Bunge lililopita ukimaanisha Novemba?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika,

Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Matamba kadiri ya upatikanaji wake. Hivi sasa Serikali ipo mbioni katika ukamilishaji wa hatua za mwisho kwa ajili ya kupata vituo vya afya hasa vile ambavyo Waheshimiwa Wabunge mlikuwa mmejaza katika zile fomu. Fedha imepatikana na ipo katika mchakato sasa wa kuweza kuletwa katika maeneo yenu kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivi vya afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo Mbunge wa Nkenge sasa aulize swali lake.

Na. 22

**Ajira za Walimu wa Somo la Kilimo Shule za Kata Nchini**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali haitoi kipaumbele cha ajira kwa walimu wa somo la kilimo katika shule za sekondari za kata ili kuhimiza vijana kujiajiri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Florrent Laurent Kyombo, Mbunge wa Jimbo la Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa hatua kwa hatua wa Sera mpya na Mitaala ya elimu nchini. Mabadiliko haya yatapelekea uhitaji wa walimu katika fani mbalimbali ikiwemo kilimo na ufundi ambazo zitawapa fursa vijana kujiajiri baada ya kumaliza Sekondari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na naomba kuwa na swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tunatambua juhudi za Serikali ambapo imeendelea kuwezesha vijana kupitia *BBT* ambayo imewezesha vijana wengi lakini pia na sera na mitaala mipya itakuwa ni chachu katika kuwainua vijana. Swali langu, wakati tunaisubiri hii mitaala ianze, kwa wakati wa sasa ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha vijana wanaohitimu masomo ya sekondari wanaweza kujiajiri, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kyombo, mkakati wa Serikali kwa sasa kuhakikisha vijana ambao wanamaliza elimu ya Sekondari wanaweza kujiajiri. Ninyi ni mashahidi Mheshimiwa Rais alitafuta fedha na kuhakikisha kwamba wilaya zote nchini zinajengewa *VETA* kwa ajili ya kuweza kutoa elimu ya ufundi na kuwaandaa vijana wetu kwa ajili yakuweza kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, vilevile kupitia Wizara ya Elimu Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan imetafuta fedha kwa ajili ya kuweza kujenga shule ya mpya za ufundi katika wilaya mbalimbali hapa nchini ambayo nayo itaenda kusaidia katika kuhakikisha vijana wetu wanapata ujuzi na stadi za kuweza kuwasaidia mara ambapo wanamaliza elimu yao ya sekondari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara Mbunge wa Tarime vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 23

**Kutenga fedha kufuatilia Miradi ya Maendeleo Ngazi ya Kata**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali haitengi fedha za kufuatilia Miradi ya Maendeleo kwa ngazi za kata na vijiji nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Nibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi za msingi ili kuongeza ufanisi na tija katika miradi inayotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, miradi inayotekelezwa katika vijiji na kata husimamiwa na viongozi na wataalam na watendaji wa ngazi zote za Serikali kuanzia Taifa, mikoa, halmashauri, kata, vijiji na mitaa. Gharama za ufuatiliaji wa miradi hii hutokana na bajeti za Serikali za usimamizi wa miradi kutokana na fedha za Matumizi Mengineyo *(OC)* na fedha za mapato ya ndani katika halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua ufinyu wa bajeti za kufuatilia miradi hususani katika ngazi za kata na vijiji kutokana na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ili kuongeza bajeti ya usimamizi wa miradi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kote Nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nimesikiliza majibu ya Serikali naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ni kwamba fedha za ufuatiliaji zinaanzia makao makuu pale TAMISEMI zinaenda kwenye ngazi ya mkoa

zinaishia kwenye ngazi ya halmashauri. Zile Kamati za Ujenzi, Mapokezi na Manunuzi hawalipwi chochote.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nijue Mheshimiwa Naibu Waziri anaona ni sawa wananchi wa kawaida wanaunda kamati ambayo inasimamia mradi kwa siku 30, siku 60 na siku 120 wanashinda njaa kutwa nzima. Unaona ni sahihi hili jambo kufanyika kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kwa majibu yake hapa anasema kuna fedha ya *OC* inatumika, anaweza akaleta takwimu kwamba katika majengo yote humu ndani ni halmashauri gani ambayo viongozi wale wa chini kabisa kwenye kamati ya ujenzi ya vijiji wamewahi kulipwa chochote cha maji au chakula? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Waitara. Hili la kwanza la fedha ya ufuatiliaji, kwa dhana nzima ya *D by D* wenye majukumu na mamlaka ya kuweza kusimamia ujenzi wa miradi mbalimbali katika halmashauri ni halmashauri yenyewe.

Mheshimiwa Spika, hii miradi ya vituo vya afya, shule na kadhalika inayoletwa ni *complimentary* kutoka Serikali Kuu lakini mamlaka na wajibu wa halmashauri kuendana na dhana nzima ya *D by D* ni wao wenyewe kuweza kukusanya mapato yao na kuweza kupanga miradi yao ya maendeleo na kutenga fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, sasa katika miradi hii ambayo inatoka Serikali Kuu fedha ya *monitoring* huwa ipo mkoani, huwa inapelekwa wilayani mfano kwenye shule ujenzi wa shule mpya hizi za mikoa kuna fedha imepelekwa katika mkoa, kuna fedha imepelekwa shilingi milioni nne katika halmashauri na kuna shilingi milioni moja katika shule yenyewe husika ambayo inajengwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nawatake wakurugenzi wote nchini kuendelea kuiishi dhana nzima ya *D by D* na kutenga fedha ya ufuatiliaji kwenye miradi ya maendeleo ambayo inaletwa na Serikali Kuu kwa kutenga fedha kutoka kwenye mapato yao ya ndani ili kama alivyosema Mheshimiwa Waitara hizi kamati ambazo zipo pale shuleni za mapokezi, za manunuzi na kamati ya ujenzi basi walau waweze kuwa wanapata hata maji ya kunywa kipindi cha usimamizi wa miradi hii.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la takwimu, tutafuatilia kutoka kwenye halmashauri zetu tena kwenye ileile dhana ya ugatuaji wa Madaraka kwenda kule kwenye halmashauri tutafuatilia na kuona ni halmashauri zipi ambazo zilitenga fedha hizi na tutaleta mbele ya Bunge lako tukufu.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 24

**Kukarabati barabara za Vijijini Manyara**

**MHE. REGINA N. QWARAY** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa dharura wa kuzikarabati barabara za vijijini zilizoharibiwa na mvua za *el-nino* katika Mkoa wa Manyara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza kuzikarabati barabara za vijijini zilizoharibiwa na Mvua za *El-nino* ambapo kiasi cha shilingi milioni 498 kimepelekwa *TARURA* Mkoa wa Manyara kwa ajili ya kurekebisha uharibifu unaoweza kurekebishika kwa sasa ikiwemo kuondoa matope barabarani, kuchonga baadhi ya barabara, kuweka changarawe, kuchimba, kusafisha mifereji na kurekebisha mikondo ya mito.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitiada za kutafuta fedha za kurekebisha miundombinu ya barabara zilizoathiriwa na mvua zinazoendelea kunyesha kote nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwanza, nianze kwa kuishukuru Serikali kwa namna ambavyo imetukimbilia wananchi wa Mkoa wa Manyara hususan Wilaya ya Hanang wakati tulipopata maporomoko ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana pamoja na Bunge lako kwa namna ambavyo mmetuletea misaada sisi wananchi wa Hanang, tunakushukuru sana. Nawashukuru wananchi wote Watanzania kwa namna ambavyo wametukimbilia na kutuletea misaada kipindi chote cha athari ya maporomoko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza; kwa kuwa bado mvua za *El Nino* zinaendelea katika maeneo mengi hapa nchini hususan Mkoa wetu wa Manyara, na fedha tulizotengewa na Serikali bado ni kidogo sana ukizingatia athari tuliyonayo;

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kutoa fedha ya dharura kwa ajili ya kukabiliana na hali halisi?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa maeneo mengi sasa hivi yameharibika, madaraja yamesombwa na wananchi hawana namna ya kufika katika maeneo mbalimbali;

Je, Serikali haioni sasa kuwa kuna haja ya kufanya tathmin ya kina ili kukabiliana na athari ya maporomoko pamoja na athari ya mafuriko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Regina Ndege. La kwanza, hili la kwamba Serikali haioni haja ya kutoa fedha ya dharura; kama ambavyo nilijibu katika majibu yangu ya msingi, shilingi milioni 498 iliyokwenda kule ni fedha ya dharura siyo fedha ambayo ilikuwa imetengwa katika bajeti ya *TARURA* Mkoa wa Manyara kwa ajili ya kuondoa matope na kuhakikisha njia zinapitisha wakati wote hasa kipindi hiki ambacho mvua hizi bado zinaendelea kunyesha.

Mheshimiwa Spika, naenda kwenye swali lake la pili, tathmini ya kina inafanyika. Tayari *TARURA* imefanya tathmini hadi kufikia mwisho wa Januari kuona athari za mvua katika maeneo yote nchini na ni kiasi gani cha fedha ambacho kinahitajika kwa ajili ya kuweza kukarabati barabara hizi na kuhakikisha zinapitika.

Mheshimiwa Spika, kwa kauli ya mtendaji mkuu wa *TARURA* ameshawaelekeza mameneja wote wa mikoa hapa nchini kuhakikisha kokote kule ambapo barabara imekatika basi atafutwe mkandarasi aweze kuanza kutengeneza wakati fedha hiyo inatafutwa kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Barabara ya Mabogini – Kahe inahudumia wakazi wa Majimbo ya Moshi Vijijini na Vunjo. Barabara hii imeharibika sana kutokana na mvua nyingi za *El Nino* zinazoendelea.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati barabara hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala za Barabara Mijini na Vijijini (*TARURA*) tayari imeshapeleka shilingi milioni 368 katika Halmashauri ya Moshi Vijijini kwa ajili ya ukarabati wa barabara mbalimbali ikiwemo ya Elimu Sekondari na Muungano Sekondari. Bado tathmini inaendelea kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii ambayo ameitaja Profesa Ndakidemi ya Kahe hadi Mabogini ambayo pia inaunga Majimbo mawili, Jimbo la Profesa Ndakidemi na Jimbo la Dkt. Kimei kule Vunjo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kata ya Igumu pamoja na Kata ya Image kwa sasa hazina mawasiliano kutokana na barabara kuharibika kutokana na mvua zinazoendelea.

Je, ni hatua gani za dharura zinachukuliwa ili Wananchi wale wapate mawasiliano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya awali kwamba hivi sasa *TARURA* kote nchini wanafanya tathmini ya uharibifu uliotokana na mvua ulivyofanyika. Tathmini ya kwanza ilifanyika, hadi kufikia mwisho wa mwezi huu Januari walikuwa wamekamilisha tathmini hiyo. Vile vile, kama nilivyosema mtendaji mkuu wa *TARURA* ameshawaelekeza mameneja wote wa mikoa kwenye maeneo kama ya Igumu na Image ambako mawasiliano yamekatika kabisa basi atafutwe mkandarasi kwa ajili ya kuweza kuunga barabara hiyo wakati fedha hiyo inatafutwa kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naona mmesimama, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu maswali yote inaonekana yanaongelea hii changamoto ya mvua zilizonyesha na maeneo hayo kupata athari nadhani wote hawa waulize kwa pamoja halafu uwape jibu kuliko kurudia jibu hilo hilo kwa kila barabara. Haya, simameni hivyo hivyo ili msiongezeke. Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Barabara ya kutoka Iringa kwenda Pawaga, Jimbo la Isimani kutoka kijiji cha Igodikafu Darajani kuelekea Mbuyuni imeharibika sana kwa sababu ya mvua hii.

Je, ni upi mkakati wa dharura wa Serikali kuhakikisha Wananchi hawa wanapata huduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Kilwa, Francis Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *TARURA* katika Wilaya ya Kilwa imeshafanya tathmini ya uharibifu uliotokana na mvua za *El Nino* katika barabara zetu za vijijini.

Je, ni lini Serikali italeta fedha za dharura Wilayani Kilwa ambazo zimeombwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Baba Askofu wewe umesimama saa ngapi? Mheshimiwa Kakoso. *(Kicheko)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tanganyika ni miongoni mwa Wilaya ambazo zimepata athari kubwa sana za barabara zilizoko vijijinii chini ya *TARURA*. Je, Serikali ina mkakati gani wa kunusuru barabara hizo ili wananchi waweze kupata huduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 80 ya barabara za Jimbo la Rorya hazipitiki kutokana na mvua kubwa inayonyesha. Kwa kuwa tumefanya tathmini tayari na

tumeandika barua kwa mkurugenzi wa *TARURA*, tunataka tupate kauli ya Serikali.

Je, ni lini sasa fedha hii itakwenda kwa ajili ya marekebisho ya barabara hizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Arumeru Magharibi limeathirika sana na mafuriko ambayo yameathiri Jimbo hilo kwa sehemu kubwa kwa kuharibu barabara na madaraja. Nataka kufahamu, Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Jimbo la Arumeru Magharibi linaangaliwa kwa jicho la huruma kutokana na jiografia yake ili kupata fedha za dharura zaidi kukarabati barabara na madaraja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamis Taletale, swali la nyongeza.

**MHE. HAMIS S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara za Jimbo letu la Morogoro Kusini Mashariki zote zimeharibika.

Je, ni lini Serikali itakuja kutuletea fedha za mfuko wa dharura?

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kutokana na mvua za *El Nino* Jimbo la Mbulu Vijijini, Kata ya Eshkesh, Yaeda Chini, Gidhim, Haydarer, Tumati na Yaeda Ampa zote hazina mawasiliano na maombi yameshaletwa *TARURA*.

Je, ni lini mnatupatia fedha za dharura ili Jimbo hili lipate mawasiliano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Askofu Gwajima, swali la nyongeza. Ngoja nitaje jina lako kabisa maana Gwajima mko wawili humu ndani. Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, swali la nyongeza.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, barabara zote za jimbo la Kawe jijini Dar es Salaam zote zimevunjika na kukatika vipande vipande kwa sababu wa wingi wa mvua zinazonyesha. Nimefika *TARURA* mkoa wakasema hawana fedha, *TARURA* wilaya hawana fedha. Nini mpango wa dharura wa Serikali kuokoa barabara za Jimbo la Kawe? Neno dharura lizingatiwe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa umesimama baada kwa hiyo, la sivyo utanifanya kama miwani yangu haioni sawa sawa nirudi hospitali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa maswali hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nijibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wake ambayo yote yalikuwa yamelenga katika kuulizia fedha lini itakwenda.

Mheshimiwa Spika, fedha ya dharura tayari imeanza kwenda kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini, pale kwa Mheshimiwa Josephat Gwajima tayari kuna shilingi milioni 598 ambayo imepelekwa katika eneo lake kwa ajili ya kuhakikisha barabara zinaanza kufunguliwa na kuweza kuanza kupitika.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge pia wameyazungumzia mfano Iringa kule, Mheshimiwa Tendega hapa ameulizia barabara ya kutoka Idodikafu na kwenda maeneo mengineyo Pawaga na kadhalika tayari fedha vile vile Iringa imepelekwa ya dharura. Kwa hiyo, *TARURA* kupitia makao makuu yake tayari imeanza kutoa fedha hizo na kupeleka.

Mheshimiwa Spika, fedha nyingine tunasubiri wenzetu wa Wizara ya Fedha waweze kuleta fedha kwa ajili ya kuweza kwenda kuendelea kufungua barabara katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri nafikiri kuna Wabunge ambao imebidi hapo niwakalishe; lakini hoja ya msingi ni kwamba umesema hapo fedha zimeanza kwenda, basi vipaumbele vitolewe kwa yale maeneo ambayo hayana mawasiliano kabisa, halafu yafuate yale ambayo yana mawasiliano lakini hayapitiki, yaani magari yanakwama, japokuwa barabara ipo, kwa sababu ya hali ya barabara katika kipindi hiki. Baadaye ndipo tuwafikie na hao wengine ambao wako vizuri kidogo. Kwa hiyo, tathmini ifanyike kwa nchi nzima. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge nadhani mtakubaliana kwamba tumeshamuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mengi yanamtosha. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 25

**Mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inapambana na mabadiliko ya tabianchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Dar es Salaam, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kupambana dhidi ya athari ya mabadiliko ya tabianchi. Mikakati iliyopo ni pamoja na Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi wa 2021 – 2026 na Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi ya Mazingira wa 2022 – 2032. Aidha, Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inao Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi wa 2014 – 2030. Mipango hii kwa pamoja inaeleza changamoto na hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika kupambana dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati iliyokuwepo, bado Serikali inaendelea na kampeni mbalimbali za kuhamasisha Wananchi ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo zoezi la upandaji miti, kuhamasisha ubunifu, utafiti na uendelezaji wa teknolojia za kukabiliana na mabadiliko ya tabiachi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo nimeyaelewa vizuri lakini bado kuna maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi ni ajenda ya kidunia lakini pia ni pamoja na kunyesha kwa mvua nyingi, ukame, mafuriko, kuharibika kwa mito, kujaa kwa bahari na mambo mengine tele.

Je, Serikali ina mpango gani wa kibajeti kuhakikisha tunakabiliana na hali hiyo katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Mkoa wa Dar es Salaam ni miongoni mwa mikoa ambayo imekumbwa na madhara ya mabadiliko ya tabianchi. Kulikuwa na mvua kubwa

ambazo zimesababisha mafuriko lakini mafuriko hayo yanasababishwa mengine na ujengaji mbaya wa miundombinu ikiwepo miferejii pamoja na miundombinu ya barabara.

Je, Serikali imejipanga vipi sasa kuhakikisha wanahakiki miundombinu yote ya barabara katika Mkoa wa Dar es Salaam ili kuepuka mafuriko ya mara kwa mara katika jiji na Mkoa wote wa Dar es Salaam? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kisangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo hili la mvua ni jambo ambalo limejitokeza na limeleta athari kubwa na nyingi katika maeneo mengi ya Tanzania. Kikubwa namwambia Mheshimiwa Mbunge kwa upande wa kujiandaa kibajeti atupe nafasi, awe na subira, tuende tukakae na Wizara nyingine za kisekta. Kwa sababu jambo hili la ukarabati wa madaraja na mambo mengine lazima sasa twende tukakae na wenzetu wa TAMISEMI, tukae na wenzetu wa Ujenzi pamoja na sisi ili tuone namna ambavyo tunaweza tukapata hizi fedha ambazo zitakwenda kutengeneza miundombinu rafiki itakayohamisha maji kutoka eneo moja kwenda eneo lingine ili kuepuka mafuriko na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mkakati namuambia Mheshimiwa Mbunge tayari tuna mwongozo maalum ambao unakwenda kusafisha mito. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira alishaunda Kamati maalum ambayo ilipita kwa ajili ya kufanya utafiti na kubaini chanzo. Nini chanzo cha haya mambo, ikiwemo mkusanyiko wa mchanga na kuziba kwa hiyo mifereji. Tukabaini mambo mengi sana kwanza ni mvua kubwa lakini mkusanyiko wa mchanga na miundombinu ambayo ilikuwa imechakaa.

Mheshimiwa Spika, kikubwa ambacho tumechukua kwanza ni kuendelea kutoa elimu kwa jamii ikiwemo ya kutokuishi na

kukaa na kujenga kwenye maeneo ambayo yanaweza kutuama maji. Pia, kusimamia sheria ikiwemo Sheria ya mita 60 pamoja na kufanya juhudi ya usafishaji wa hii mito, kutoa michanga na takataka nyingine ambazo zinaweza zikaleta mafuriko na kusababisha athari kwa wananchi, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, swali la nyongeza.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Jimbo la Nungwi ni miongoni mwa majimbo yanayoendelea kupata athari kubwa kutokana na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi. Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimefikia hatua gani katika kukabiliana na athari hizo, hususan katika maeneo ya fukwe za bahari kule Nungwi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, zipo hatua nyingi ambazo kama Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo tunazichukua katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Moja, ni kuendelea kutoa elimu kwa wananchi hasa kwa upande wa Zanzibar ukanda wa bahari, shughuli za uchumi wa blue zizingatie athari za kimazingira.

Mheshimiwa Spika, kingine tunaendelea kutafuta fedha kuona namna ambavyo tunajenga kuta ambazo zinaweza zikazuia maji ya bahari yasiingie mtaani pamoja na kusimamia Sheria nyingine za usimamizi na uchafuzi wa mazingira, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hivi karibuni katika Jimbo la Hai hususan Vijiji vya Mshara, Lyamungo na maeneo mengine zimenyesha mvua ambazo hazijawahi kutokea kabisa, mvua kubwa za mawe. Hali ambayo inahusishwa na kuyeyuka kwa theluji ya Mlima Kilimanjaro na

kuleta madhara makubwa sana kwenye miundombinu chakula na mazao.

Mheshimiwa Spika, naomba kauli ya Serikali kutokana na jambo hili kwa sababu limeleta taharuki kwa wananchi, ni jambo ambalo halijawahi kutokea, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mafuwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kipindi cha hivi karibuni kumejitokeza athari na hasa zile zilizosababiswa na jua kali ambalo lilitokea kipindi cha nyuma kabla ya kuanza mvua hizi kitu ambacho kimepelekea baadhi ya watu kufanya shughuli za kibinadamu katika maeneo ya mlima ule ikiwemo masuala ya kilimo, ufugaji na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, mwisho wa siku wengine walifika hatua ya kuchoma moto maeneo yale. Namwambia Mheshimiwa kwamba zipo hatua madhubuti ambazo kama Serikali tumeanza kuzichukua zikiwemo za kuendelea kuwahamasisha wananchi na kuwapa taaluma kwamba shughuli za kibinadamu zinazoweza kuharibu mazingira katika maeneo yale zisifanyike kwa sababu ni maeneo yenye kivutio.

Mheshimiwa Spika, kikubwa tunataka tuendelee kuwaambia wananchi kuwamba Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Wizara nyingine zikiwemo za maliasili na nyingine tutaendelea kuhifadhi mlima huo ili uweze kuwa kivutio muhimu kwa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha hiyo mvua nadhani wote tunakubaliana kwamba ni mabadiliko ya tabianchi lakini siyo kwamba ni ile barafu inayoyeyuka Kilimanjaro inayoleta hiyo

mvua kwa sababu hata Mbeya huwa inanyesha na kule hatuna Kilimanjaro. Kwa hiyo, hao wanaofikiri hivyo tuwaweke sawa maana haiko kisayansi sasa tusije tukapeleka picha kwamba barafu inayotoka pale ndiyo inayoenda kunyesha ile mvua.

Mheshimiwa Khalifa, swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mabadiliko ya tabianchi yamevikumba sana Visiwa vya Unguja na Pemba kwa maji ya bahari kuvamia makazi ya watu.

Je, ni lini Serikali itafanya utafiti na kuyatambua maeneo hayo na kuja na majawabu ya muda mfupi na muda mrefu?

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri zima kisemeo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumpongeza Naibu Waziri wangu kwa majibu mazuri sana kwa maswali yote ya mwanzo ya nyongeza na maswali ya msingi.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya rejea swali la Mheshimiwa Khalifa; kwanza naomba kumshukuru Mbunge huyu kwa sababu miongoni mwa eneo ambalo tulipata changamoto kubwa ni eneo la Jimbo lake, na kwa bahati nzuri tumeanza ujenzi wa tuta katika eneo lile. Hata hivyo tumeituma timu yetu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta kuhakikisha inafanya tathmini ya eneo lote la nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jambo hili sasa linaendelea na Wabunge tutakuja kubainisha hapa ni maeneo gani yanahitaji

jinsi gani tufanye marekebisho, pande zote mbili, Bara na Visiwani ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa salama. Hata hivyo tujue kwamba hali sasa hivi ya mabadiliko ya tabianchi yamekuwa makubwa sana. Tuna kila sababu kushirikiana kwa pamoja katika kukabiliana na hali hii na hususan katika kutekeleza swala zima la utekelezaji wa afua zote zinazohusu utunzaji wa mazingira, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge ahsante sana.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate.

Na. 26

**Ujenzi wa Barabara ya Nanjoka – Mtwara Pachani**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE K.n.y. MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kujenga barabara ya lami kuanzia Nanjoka – Nalasi - Mchoteke – Njenga – Mjimwema - Magozini hadi Mtwara Pachani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:- -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* tayari imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya Mtwara Pachani – Nalasi hadi Tunduru yenye urefu wa kilometa 300. Aidha, tarehe 21 Desemba, 2023, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* ilisaini mkataba kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 1.5 katika eneo la Tunduru Mjini ambapo Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha kwa sehemu iliyobaki. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, barabara hii kama alivyosema ina Kilometa 300 na ni muhimu sana kwa Jimbo la Tunduru Kusini pamoja na Wilaya ya Namtumbo.

Je, Serikali haioni haja ya kuongeza fedha za kuijenga kwa kiwango cha lami barabara hii angalau kwa Kilometa 50 ili kupunguza adha ya wananchi wa Majimbo haya wawili wanayoipata kutokana na barabara hii kuwa mbaya?

Swali la pili, kwa kuwa tathmini na upembuzi wa kina ulikamilika tangu 2020 na baadhi ya nyumba za watu ziliwekewa alama ya *X*, ni lini sasa Serikali itamaliza mchakato wa kulipa fidia kwenye zile nyumba ambazo zimewekwa alama ya *X* ambapo watu hao wanaishi bila matumaini yeyote? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara hii ina Kilometa hizo 300 na kwa sababu ya upatikanaji wa fedha ndiyo maana Serikali imeamua kwamba ili barabara hiyo iweze kupitika kwa kipindi chote cha mwaka, tumeamua maeneo yote yale korofi pamoja na madaraja kuyajenga walau kwa kiwango cha lami ili yale maeneo korofi yasiwe ni kikwazo kwa barabara hii kupitika katika mwaka wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami na hata pengine kujenga kwa kiasi kikubwa kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mbunge kwamba walau ziwe kilometa 50.

Mheshimiwa Spika, tunadhani tukijenga kwanza maeneo yale yote ambayo yanasababisha barabara isipitike, litakuwa ni jambo jema kuliko ukajenga kilometa hata 50 lakini maeneo korofi yale yakawa bado hayawezi kupitika. Nadhani Mheshimwa Mbunge, kama fedha itapatikana, ni kuijenga yote na kuijenga pengine kwa kilometa nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la fidia naomba nilichukue halafu nifuatilie kuona tumefikia wapi katika kuwalipa wanachi hawa ambao bado wanafikiria lini watalipwa hiyo fidia. Naomba kulichukua na nitamjulisha Mheshimiwa Mbunge mara baada ya kikao hiki cha asubuhi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Chalinze – Morogoro kwa njia nne ili kupunguza msongamano wa magari? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Chalinze – Morogoro njia nne, kwanza tunaanzia Kibaha – Chalinze, awamu ya kwanza Itakuwa Chalinze – Morogoro, na tayari Serikali imeshafanya maandalizi, barabara hii itajengwa kwa mfumo wa *PPP*. Kwa hiyo, taratibu zimeshaanza za kuanza mchakato huo wa kuijenga barabara njia nne kwa ubia kati ya wadau na Serikali. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali mafupi, majibu mafupi. Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni lini ujenzi wa barabara ya Iringa *bypass* utaanza kwa kiwango cha lami ukiunganisha na Ruaha Msembe? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri amepita pale na ameshatoa maelekezo kwa *TANROADS* kuhakikisha kwamba ile barabara ya *bypass* Iringa inakamilishwa haraka sana kwa kiwango cha lami kwa sababu tayari imeshaanza. Kwa upande wa barabara ya Iringa – Msembe ambayo ni Kilometa kama 103, ambayo wanaotufadhilli ni *World Bank,* tayari tuko kwenye hatua za manunuzi kuijenga hiyo barabara yote kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza, ama ni nani? Mheshimiwa Dkt. Samizi, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipatia nafasi; je, ni lini Serikali itakagua ujenzi wa barabara ya kipande cha Kibondo *town link* ambao unasuasua kwa muda mrefu sasa ni miaka minne?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kipande hiki anachokisema nimepita mwezi wa kwanza huu kuangalia kinachotukwamisha, lakini tulichofanya ni kuhakikisha kwamba zile *IPC* ambazo zilikuwa hazijalipwa lakini pia kulikuwa na changamoto ndani ya uongozi wa kampuni yenyewe inayoongoza iweze kujipanga na tuweze kukamilisha hiyo Barabara, sasa hivi nadhani tupo kwenye asilimia zaidi ya 50, kwa hiyo nina hakika barabara hiyo itakamilika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Barabara ya Mogitu – Haydom Mheshimiwa Naibu Waziri ameshaitembelea mara nyingi. Je, ni lini ujenzi wake utaanza kwa kiwango cha lami hasa eneo la Mogitu ambalo ni korofi sana na Mlima Chavda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara hii itajengwa kama ilivyokuwa imepangwa kwenye bajeti kwa kiasi hicho. Natambua kweli kama anavyosema kuna eneo ambalo ni korofi sana na Serikali tunategemea tuanze kwenye hilo eneo korofi ili wananchi wasiweze kukwama kupita kati ya Mogitu – Haydom. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, shukrani zenu zote nimezipokea kwa hiyo hamna haja ya kusema ahsante Mheshimiwa Spika nimeshazipokea. Mheshimiwa Stella Fiyao.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati gani wa kuunganisha Wilaya ya Mbozi na Wilaya ya Songwe kwa kujenga barabara kupitia Mlowo – Isansa – Magamba – Mkwajuni ili kurahisisha huduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, tayari imeshapokea maombi hayo kutoka *RCC* Mkoa wa Songwe na Meneja wa Mkoa ameshaelekezwa kuanza kufanya usanifu ili kipande kile kilichobaki kuunganisha kati ya Mkoa wa Songwe na Wilaya ya Songwe ambazo hazijaunganishwa kwa kiwango cha *TANROADS* waweze kuanza upembuzi na usanifu ili tuweze kuwa na barabara hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuondoa msongamano katika barabara ya Kilwa eneo la Kongowe – Kokoto ambalo ni lango kuu la kuingia na kutoka Dar es Salaam kwa wakazi wa Mikoa ya Kusini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, kwanza ina mipango ambayo tulishapewa maelekezo na Mheshimiwa Rais kwamba ijengwe kwa njia nne ama njia sita kati ya eneo alilolitaja nadhani mpaka Vikindu kwa njia hizo nne ama sita. Nitaangalia vizuri, lakini ni kati ya nne ama sita kwa sababu ya upana na umuhimu wa barabara hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya Amkeni – Kitangali – Mtama kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli hiyo barabara inaunganisha hayo Majimbo mawili, ambacho sasa hivi tunakifanya na Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi, tumekuwa tukiendelea kwanza wakati tunatafuta fedha kuijenga kwa kiwango cha lami ama zege katika maeneo ambayo yana miinuko mikubwa. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili tuweze kujenga kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mkuranga wana kiu kubwa ya barabara ya Mkuranga – Kisiju, ni lini itakamilika kwa ujenzi wa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami tutakapokuwa tumefanya upembuzi na usanifu wa kina, hiyo barabara tutaijenga kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalumu, sasa aulize swali lake.

Na. 27

**Ujenzi wa Barabara ya Same – Mkomazi**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza: -

Je, nini kinakwamisha ujenzi wa barabara ya Same - Kisiwani - Ndungu hadi Mkomazi licha ya kutengewa fedha miaka minne mfululizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali ilitenga fedha kiasi cha shilingi milioni 860 na zilitumika kwa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Same – Kisiwani – Ndungu hadi Mkomazi yenye urefu wa kilomita 96.46 na kazi ilikamilika mwezi Septemba, 2022. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi milioni 6,300 ambazo zilitumika kwa kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa kipande cha kilometa 5.2 kutoka Gonja – Ndungu ambapo kazi za ujenzi zinaendelea na zimefikia asilimia 55 na zinatarajiwa kukamilika Juni, 2024.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ipo katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu za kusaini mkataba wa mkandarasi ili kuanza kujenga sehemu iliyobaki yenye urefu wa kilometa 91.26 kwa kiwango cha lami na imegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni Same – Kisiwani – Mroyo yenye urefu wa kilometa 56.8 na Mroyo – Ndungu – Mkomazi yenye urefu wa kilometa 36 ili kuharakisha ujenzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, swali la nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli, ukiangalia takwimu aliyoitoa Mheshimiwa Waziri hapa zina utata mkubwa sana kiasi ambacho nitakiomba Kiti chako kiruhusu akafanyie kazi upya ya kujibu hili swali. Nikitoa mfano, anasema upembuzi yakinifu kutoka Same – Kisiwani – Ndungu ulikamilika Septemba, 2022, hapohapo anasema kuna Mkandarasi alipewa *contract* 2020/2021 kwa kipande cha Kilometa 5.2, akapewa *contract* ya shilingi bilioni sita.

Mheshimiwa Spika, hapohapo akizungumzia hizo kilometa ambazo zitatengenezwa na *contractors* wawili wanaokuja, ukimjumlisha hazifiki kilometa ambazo zitajengwa. Sasa,

ukiangalia ni kwamba Mheshimiwa Waziri hujafanya *homework* yako vizuri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kwamba hii barabara imekuwa na utata kwa muda mrefu, naomba Kiti chako ama kiagize akafanye kazi upya au tumuombe Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, akaangalie hii barabara jinsi ambavyo imekuwa ikichezewa kwa miaka mingi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo aliyotoa Mheshimiwa Kaboyoka kuhusu swali hili ni kama Serikali imetoa majibu tofauti na hali halisi iliyopo huko kwa maelezo ya Mheshimiwa Mbunge. Sasa, kwa sababu mimi sina hakika, Mheshimiwa Mbunge nimemsikia na Serikali nimeisikia sina hakika yupi anayesema uhalsia ulioko pale. Kwa sababu Mheshimiwa Mbunge anauliza eneo ambalo yeye analifahamu kule na Serikali imetoa majibu kwa kadri wao wanavyofahamu, nitawapa nafasi Serikali kwa swali hii mkajiridhishe kama haya majibu ndiyo yenyewe ili mlete tena hapa ndani, kama siyo yenyewe wametengeneza pengine wataalam kwenye Halmashauri halafu kule chini hawajafika ama wametengeneza Makao Makuu kule hawajafika basi mtapata nafasi ya kuyatoa majibu tena ili tuwe na uhakika na majibu kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ameleta hayo malalamiko ya jumla hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa muktadha huo, hakuwezi kuwa na maswali ya nyongeza kwenye majibu ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyakataa, ndiyo utaratibu wetu kwa sababu maswali ya nyongeza yanatokana na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa hivyo, swali hilo litapata nafasi tena na hapo baadae sasa tutajua kama majibu yaliyotolewa na Serikali yana uhalisia wa kinachoendelea kule ama hapana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mbunge wa Tandahimba, sasa aulize swali lake.

Na. 28

**Kupunguza tozo kwenye zao la korosho**

**MHE. KATANI A. KATANI** aliuliza: -

Je, Serikali ipo tayari kupunguza baadhi ya tozo kwenye zao la korosho ili kumsaidia mkulima kupata bei nzuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mbunge wa Jimbo la Tandahimba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya maboresho ya kodi, ada na tozo katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 katika kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo ikiwemo zao la Korosho. Katika kipindi cha miaka minane (2015-2023) Serikali imefanya maboresho ya ada na tozo kwa kufuta jumla ya tozo na ada 105 zilizokuwa zinatozwa kupitia bodi na taasisi zilizo chini ya Wizara ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka nane (8) Serikali imefanikiwa kufuta jumla ya tozo sita katika zao la korosho ambazo zilionekana ni kero kwa wakulima. Maboresho hayo ni utekelezaji wa Mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti na usimamizi wa biashara *(Blueprint for regulatory reforms to improve the business environment)*.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha na kuongeza uwekezaji katika sekta ya kilimo pamoja na kupunguza gharama kwa wakulima nchini, Serikali itaendelea kufanya maboresho ya kodi, ada, tozo na ushuru kwenye mazao ya kilimo, ikiwemo zao la korosho ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza mapato kwa mkulima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, swali la nyongeza.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Moja, kwa kuwa fedha za *export levy* dhamira yake ni kuendeleza zao la korosho na fedha hizo hupelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Je, Serikali ipo tayari sasa fedha zile kupeleka moja kwa moja Bodi ya Korosho ili ziweze kuendeleza zao la korosho?

Mbili, kwa kuwa Waziri mwenye dhamana ya Kilimo mara kadhaa ameshasema zimetengwa fedha shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kupeleka pale Maranje ambapo tunakwenda kujenga viwanda vya kuchakata zao la korosho na kuliongezea thamani.

Je, ni lini fedha hizo zitakwenda bodi ya korosho ili shughuli hizi ziweze kuendelea? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kurudisha fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kupeleka kwenye bodi ya korosho zile *export levy*, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Kilimo kupitia Waziri wa Kilimo pamoja na Wizara ya Fedha wameanza vikao vya kujadiliana namna bora ya kutekeleza jambo hili kwa kuwa tunaamini vitakuwa kwa manufaa ya wakulima wa zao la korosho nchini, kwa hiyo akae tu katika mkao wa kutulia kwa sababu vikao vinaendelea juu ya jambo hili ambalo amelizungumza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shilingi bilioni 10 ambazo zinahitajika kupelekwa pale Maranje, Wizara ya Kilimo kupitia Waziri wa Kilimo, tumeshaandika barua Hazina kwa ajili ya kuzipata fedha hizo na Hazina wametuhakikishia fedha hizo zitatoka. Nakuondoa shaka mchakato wa uendelezaji lile eneo unaendelea pale ikiwemo wameanza kusafisha na Mkandarasi yupo *site,* kwa hiyo na lenyewe litatekelezwa kwa sababu nia yetu ni kusaidia zao na tasnia nzima ya korosho nchini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kuna mwingiliano wa njia mbili hizi ambazo tunazitumia katika kuuza korosho yaani minada na soko la awali na hivyo kuathiri bei ya korosho ambayo anaipata mkulima. Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu swala hili?

**SPIKA:** Swali la msingi linahusu kupunguzwa kwa tozo, sasa hapa naambiwa bei ya korosho. Mheshimiwa Naibu Waziri, anataka kauli ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatambua changamoto iliyopo katika zao la korosho, hususan katika huu mkanganyiko wa minada na bei ya korosho katika masoko ya awali. Wizara ya Kilimo kupitia Waziri wa Kilimo, tumeandaa Mkutano wa Wadau wa Korosho ambao watakaa pamoja vikiwemo vyama vya ushirika ili kupitia huu mchakato wote. Kitu ambacho nina uhakika na kauli ya Serikali ni kwamba, mfumo uliopo sasa hautakuwepo baada ya hicho kikao ambacho tutakaa kupitia na kufanya tathmini hususan mkanganyiko katika minada na soko la awali ambao unaendelea hivi sasa, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu ni nini mkakati wa Serikali wa kupandisha fedha ambayo italipwa benki kwa wakulima wa kahawa Mkoani Songwe kutoka shilingi milioni moja ambayo sasa wanaona ni usumbufu kwao kufungua akaunti kwa shilingi milioni moja?

**SPIKA:** Litajibiwa kama swali la msingi. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kuna tozo nyingi zana kipindi hiki cha msimu wa kuvuna parachichi katika Wilaya ya Rungwe na Njombe. Ni lini Serikali itahakikisha tozo hizi ambazo zinatesa sana sana wakulima zinaondolewe, ikiwemo tozo ya kulipia zile bakasha ya kubebea parachichi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimwakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kila baada ya msimu wa zao, Wizara na taasisi zake huwa tunapitia na kufanya tathmini ya mwenendo mzima wa soko katika kipindi husika.

Kwa hiyo, katika mapitio yale, katika zile tozo zinazokuwa na kero, sisi kama Wizara huwa tunazichukua na baadaye Waziri wa Fedha kupitia bajeti yake huwa anazitolea ufafanuzi ikiwemo kuziondoa baadhi, nyingine kurekebisha tozo kama kiwango kikiwa kiko juu, kuzishusha na nyingine tutapokea maoni kutoka kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hilo tumelipokea na tutampa majibu wakati wa Bunge la bajeti. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Fatma Toufiq.

Na. 29

**Serikali kuunda Bodi ya zao la zabibu**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ K.n.y. MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaunda Bodi ya Zao la Zabibu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Jimbo la Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zao la zabibu ni moja ya mazao ya bustani *(horticulture)* na muhimu katika kukuza kipato na kuboresha maisha ya wananchi wa Kanda ya Kati hususan Mkoa wa Dodoma. Tofauti na mazao ya asili ya biashara (korosho, pamba, chai, kahawa, mkonge, tumbaku na pareto), zao hili pamoja na mazao ya nafaka na mazao mengine ya bustani halikuwa na bodi mahsusi kwa ajili ya kusimamia maendeleo yake.

Mheshimiwa Spika, kufuatia upungufu uliobainika, Serikali ilifanya Marekebisho ya Sheria ya Usalama wa Chakula *(The Food Security Act)* ya Mwaka 1991 kupitia Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko *(The Cereals and Other Produces Act)* ya mwaka 2009 na kuunda Mamlaka ya Mazao Mchanganyiko *(Cereals and Other Produces Regulatory Authority – COPRA)* ambayo ina majukumu ya kusimamia uzalishaji, uchakataji na masoko ya nafaka na mazao mchanganyiko ikiwemo zabibu.

Mheshimiwa Spika, mamlaka hii imeundwa hivi karibuni na Serikali imeishateua Mtendaji Mkuu pamoja na bodi ya mamlaka hiyo ambayo ilizinduliwa tarehe 18 Desemba, 2023. Aidha, Wizara

inakamilisha orodha ya mazao yatakayoanza kusimamiwa na mamlaka hiyo kwa ajili ya kuyatangaza kwenye Gazeti la Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri. Pamoja na hayo, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa gharama za uzalishaji zabibu ni kubwa, nini mkakati wa Serikali wa kuweka ruzuku katika zao la zabibu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza zao la zabibu hasa zabibu za Mezani ambazo ziko bado kwa uchache? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nashukuru kwa maswali mawili ya msingi ambayo yameulizwa na Mheshimiwa Mbunge ikiwemo gharama za uzalishaji zabibu kuwa kubwa na wameomba ruzuku iongezwe kwenye zao la zabibu. Nimwambie tu kwamba sisi kama Serikali tumelipokea na tutaenda kufanya tathmini na kuona ni maeneo yapi tunaweza tukawasaidia wakulima wa zabibu ili nao waweze kunufaika na huu mchakato. Kwa hiyo, hilo tumelipokea kama Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mkakati wa Serikali hususan katika zabibu za mezani, jambo hili tumeendelea kutoa wito kwa wakulima nchini waweze kuongeza na elimu imekuwa ikiendelea kutolewa. Kwa hiyo, kwa sababu naamini kwamba bado elimu hii haijafikia watu wengi, sisi kama Wizara kupitia Taasisi ya *COPRA* tutaongeza sasa msukumo kuhakikisha hili lengo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelisema tunalifikia, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mbunge wa Masasi Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 30

**Kuboresha Kiwanja cha Ndege cha Masasi**

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuboresha Kiwanja cha Ndege Masasi ili kitumiwe na wafanyabiashara wa Masasi, Newala, Nanyumbu na Nachingwea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza utekelezaji wa mpango wa upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Masasi ambacho kwa sasa kina ukubwa wa ekari 82.482 ambapo uthamini wa eneo la nyongeza lenye ukubwa wa ekari 217 kwa ajili ya upanuzi wa kiwanja hicho unaendelea. Pindi utakapokamilika, taratibu za ulipaji fidia zitafanyika. Aidha, Kiwanja kinachotegemewa kujengwa ni cha daraja *2C* kitakachoweza kuhudumia Ndege kubwa zenye uwezo wa kuhudumia abiria 50 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha zoezi la utwaaji ardhi wa eneo la nyongeza, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya kiwanja hicho.

**SPIKA:** Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, hata hivyo nina maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kujua *commitment* ya Serikali ya ulipaji wa fidia ikoje baada ya uthamini kufanyika na hasa kwenye mwaka huu wa fedha ili wananchi wa Masasi watulie?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, natamani kujua kwamba je, Serikali imejipanga kwenye bajeti ya mwakani 2024/2025 kukamilisha ujenzi wa *airport* hii kwa kiwango cha *level* ya *2C*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwambe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na *commitment* ya Serikali kama nilivyojibu kwenye swali la msingi ni kubwa, ndiyo maana kwanza tunaongeza ukubwa wa kiwanja na kupandisha daraja. Kuhusu ulipaji wa fidia, zitafanyika mara tu taratibu zitakapokuwa zimekamilika tukishirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza uwanja huo, mara tu kazi ya ulipaji wa ardhi ikikamilika na taratibu nyingine zikishakamilika, tutakwenda kwenye hatua hiyo ya pili kwa sababu ni mpango na *commitment* ya Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha kwamba uwanja huo uboreshwe na ujengwe kwa kiwango ambacho Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa maeneo hayo ambayo yametajwa wangependa kuona inafanyika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka miundombinu sahihi katika Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Arusha ilia basi ndege kubwa zinazoleta watalii nchini ziweze kutua hasa nyakati za usiku?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, maboresho mbalimbali yanafanyika katika Uwanja wa Ndege wa Arusha na viwanja vingine nchini. Kwa pale Arusha kwa sasa tunaendelea na ujenzi wa jengo la abiria, lakini pamoja na hoja aliyoisema, kwa kuwa eneo la Arusha ni eneo la utalii, Serikali inao mpango na itaweka taa mara tu taratibu za awali zitakapokuwa zimekamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kasinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali imefikia hatua gani katika kulipa fidia wananchi wa Kilwa Masoko kwa ajili ya upanuzi na uboreshaji wa kiwanja cha ndege?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu mkubwa wa Kiwanja cha Ndege cha Kilwa Masoko ambacho kinaenda sambamba na ujenzi wa bandari kubwa ya uvuvi, Serikali inaendelea na taratibu mbalimbali kupitia wenzetu wa Wizara ya Fedha na watakapokamilisha, tutalipa fidia ili ujenzi uweze kuendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Chinguile, swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wapo wananchi wa Jimbo la Nachingwea walipisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Nachingwea kwa muda mrefu sasa: Je, ni lini Serikali itawalipa wananchi hawa ambao walipisha eneo hili la uwanja wa ndege?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, tunaendelea kufanya mchakato na wenzetu wa Wizara ya Fedha, taratibu zitakapokamilika tutalipa fidia mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Elibariki Kingu.

Na. 31

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Singida**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU K.n.y. MHE. MARTHA N. GWAU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Uwanja wa Ndege Mkoa wa Singida?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Gwau, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia *TAA* imekamilisha tathmini ya mahitaji ya ardhi kwa ajili ya upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Singida. Hadi sasa taratibu za utwaaji ardhi zinaendelea kwa kushirikiana na Ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi wa Mkoa wa Singida. Kiwanja hicho kitakuwa Daraja 2C ili kukiwezesha kuhudumia ndege kubwa zenye uwezo wa kuhudumia abiria 50 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka ujao wa fedha 2024/2025, Serikali inatarajia kutenga fedha kwa ajili ya uhuishwaji wa usanifu wa kina ili kuwa na mahitaji ya kiufundi. Mara baada ya hatua hii kukamilika, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Elibariki Kingu, swali la nyongeza.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ambaye kwa kweli nina imani naye kubwa sana, lakini naomba nitoe tahadhari kuwa tarehe 4

Septemba swali hili liliulizwa hapa hapa Bungeni na siku hiyo ilikuwa ndiyo siku ya kwanza kwa Mheshimiwa Kihenzile kujibu maswali, jibu lililotolewa na Mheshimiwa Kasekenya ambaye alijibu kwa niaba yake, lilikuwa ni tofauti na ambalo limetolewa sasa hivi. Huo ni ukweli. Hata mimi nilishauliza swali hili miaka mitatu nyuma, *Hansard* za Bunge zipo, majibu yalikuwa tofauti.

Mheshimiwa Spika, nina imani na Serikali, ninaiomba Serikali iwe na *commitment* kumaliza ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Singida. *(Makofi)*

**SPIKA:** Una neno la kusema? Naona unaniangalia. Ameleta ombi, kwa hiyo, ni kulipokea ombi lake Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nimelipokea. Kwa kuongezea ufafanuzi kidogo ni kwamba, awali tulitegemea tuendeleze ujenzi kwenye eneo lililokuwepo ambalo lina ukubwa wa hekta 49.1, lakini kutokana na umuhimu na uzito mkubwa wa uwanja wa Singida, tumebaini kwamba wanatakiwa kupata eneo kubwa zaidi. Hivyo, mamlaka ya viwanja vya ndege inaongeza eneo lingine zaidi ili kiwanja hicho kipande daraja kutoka 1C kwenda 2C kiweze kuwa kikubwa zaidi, ndege ya Q400 iweze kutua pale, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 32

**Marekebisho ya Sheria ya Bima kwa wahanga wa ajali za barabarani**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itarekebisha Sheria ya Bima kwa lengo la kuweka kima cha chini cha malipo ya fidia kwa wahanga wa ajali za barabarani?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, anayekuja kujibu ni nani? Simwoni. Serikali, hakuna majibu ya haya maswali? Mheshimiwa Waziri wa Fedha viti hivi vimewekwa kwa ajili ya sababu hiyo. Wizara ya Fedha, swali limeshaulizwa na Mheshimiwa Mbunge. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Septemba, 2022 Mamlaka ya Bima Tanzania ilitoa Mwongozo unaotambulika kama "Mwongozo wa Viwango Elekezi vya Fidia ya Bima kwa Madai ya Majeraha ya Mwili pamoja na Vifo kwa Mtu wa Tatu Kutokana na Ajali za Vyombo vya Moto." Mwongozo huo ulitolewa kwa mujibu wa kifungu cha 6(2)(b) na 11(a) na (b) cha Sheria ya Bima Sura Na. 394. Aidha, lengo la Mwongozo huo ni kuweka usawa na ubora katika ulipaji wa fidia zitokanazo na madai ya bima.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mwongozo huo umepunguza kwa sehemu kubwa malalamiko kutoka kwa wahanga wa ajali za vyombo vya moto kwa kuwa kuna usawa katika suala la viwango vya fidia vinavyotolewa na kampuni za bima. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, napenda kutumia fursa hii kuwaasa wananchi kutunza kumbukumbu na nyaraka muhimu za rejea ili kurahisisha zoezi la ulipaji wa fidia, hususan kwa wasimamizi wa mirathi. Aidha, Serikali inaendelea na jitihada za kujenga uelewa kwa wadau wa tasnia ya bima na wananchi kwa ujumla ili kutimiza matakwa ya Sheria ya Bima, Sura 394 ikiwemo kuboresha huduma za bima na kumlinda mteja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daktari Kikoyo swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru; tatizo la kudai bima limekuwa sugu. Ningependa kujua ni nani anasimamia kikamilifu huo mwongozo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Usafiri wa anga na usafiri wa majini, sheria mama zimetaja kiwango cha fidia kwa wahanga wanaopata ajali: Je, kwa nini kwa usafiri wa nchi kavu hivyo viwango hatukuviweka kwenye sheria mama? Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri. Moja tuna *regulator* ambaye anasimamia masuala haya ya bima, na sheria hizi zimeweka wazi taratibu hizi za namna ya kufuatilia.

Mheshimiwa Spika, kinachojitokeza mara nyingi sisi kwetu Watanzania tulio wengi, tunapenda sana kuendesha mambo kwa kuaminiana. Pale kabla tatizo halijatokea, hatuweki vizuri sana kumbukumbu. Unaweza ukakuta mchakato wa kuandikisha bima haukukamilika, unaweza ukakuta kuna masuala ya ku-*update* kumbukumbu hatuku-*update,* unakuta pale tatizo limeshatokea ndiyo mtu anatafuta kufanya *post clearing* ya *information* ambazo zinatakiwa kumsaidia kulipwa. Kwa hiyo, yanajitokeza masuala haya, lakini masuala yote ya kisheria yanaenda kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kama nilivyosema kwa Watanzania kuweza kuweka kumbukumbu hizo sawa. Sheria kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, tumeendelea kuboresha, lakini *baseline* ni lazima Watanzania kwenye haya mambo yote yanayohusisha masuala ya kimalipo, ni lazima tuwe tunaweka vizuri kumbukumbu na tuzi-*align* na sheria zinavyotaka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Konde, sasa aulize swali lake.

Na. 33

**Kuongeza mapato biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara**

**MHE. MOHAMED SAID ISSA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza mapato ya biashara zinazofanyika kati ya Tanzania Bara na Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali za pande mbili zimeendelea kuboresha na kutekeleza mikakati mbalimbali kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu mbalimbali za uwekezaji na biashara. Baadhi ya mikakati inayotekelezwa ni pamoja na kuboresha na kuunganisha mifumo ya kodi ya *EFDMS* na *VFMS* ili kusomana na kurahisisha utozaji kodi, ada pamoja na tozo ili kuboresha mifumo ya urejeshaji wa kodi ya ongezeko la thamani *(VAT),* kurahisha mifumo ya utoaji vibali, leseni na ukaguzi wa mizigo.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza uwazi, Serikali kupitia Mamlaka za Usimamizi wa Mapato, zimeweka bango linaloonesha bidhaa ambazo hazipaswi kulipiwa ushuru. Aidha, pande zote zimekubaliana kuwa ushuru wa forodha unaokusanywa kwa upande wa Zanzibar, uwasilishwe kwenye mfumo wa Hazina wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ili kuongeza tija katika ukusanyaji wa mapato na ufanisi katika udhibiti wa biashara za magendo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, nilitegemea pamoja na majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri basi angeniwekea *data* kuonyesha kwamba biashara imeongezeka

lakini katika majibu yake ameniwekea maelezo na yeye ni Muhasibu. Wahasibu wanacheza na namba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo nilitamani kujua pale Zanzibar kuna mwekezaji mpya ambaye amepunguza masaa ya kazi wanaita *ZMT* ambaye ni bandari je, hapa mapato yameongezeka ama yamepungua?

Mheshimiwa Spika, lakini la pili biashara ya Zanzibar na Tanzania Bara zinategemea mipaka yetu pale kuna *TPA* (kuna bandari) na *TRA*, hawa wana husiana katika kukusanya kodi. Je, Serikali itakuwa tayari kuweka masaa ambayo yataongeza mapato kiasi ambacho kwa sasa Taasisi hizi moja inafanya nusu, saa kumi moja inafanya mpaka saa nne ya usiku. Je, itakuwa tayari kuweka masaa walau kumi na nane? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni ya msingi tutakaa pande mbili Wizara za Fedha pamoja na Uchukuzi kwa *Main land* pamoja Zanzibar ili tuweze kuchakata, tuweze kutekeleza hilo ni wazo zuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, mawazo yote mawili yamechukuliwa. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Afya, Mheshimiwa Tamima Haji Abass Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 34

**Kupinga ukatili katika Kliniki za Mama na Mtoto**

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kutayarisha Vipindi vya Elimu vya kupinga ukatili wa kijinsia katika Kliniki za Mama na Mtoto Nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tamima Haji Abass, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni wazo zuri sana kutoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia katika kliniki za mama na mtoto na Serikali imekwisha anza mkakati huo ambao siyo tu kwenye kliniki lakini pia kwa kupitia vipindi vya luninga na redio.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha hilo, Serikali inatarajia kufundisha na kulipa posho ya kila mwezi kwa wahudumu wa Afya ngazi ya jamii wapatao laki 137,294 kwa gharama ya shilingi bilioni 899.5 wahudumu hawa watakuwa wawili wawili kwa kila mtaa (mitaa yote 4,264) na wawili wawili kwa kila kitongoji (vitongoji 64,384) ili kutoa elimu ya afya, lishe na kupinga ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, mkakati huo unazinduliwa leo hii tarehe 31 Januari, 2024 na Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tamima Haji Abass, swali la nyongeza.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali ya nyongeza. La kwanza; kwa kuwa kliniki hizi zinatoa huduma za elimu mbalimbali na kama alivyosema leo mkakati unazinduliwa je, ni lini utekelezaji wake utaanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; baada ya kuanza huo utekelezaji, ufuatiliaji wa masuala hayo je, Serikali inatumbia nini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali lake la kwanza kwa sababu huo uzinduzi wa wahudumu ngazi ya jamii unafanyika leo ni kwamba Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, fedha bilioni 899.5 zimeishapatikana na mara baada ya leo Mheshimiwa Makamu wa Rais kuzindua basi mafunzo yataanza na baada ya mafunzo watu wataingia mtaani kwa ajili ya kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, inaanza mara moja baada ya uzinduzi huu wa leo.

Mheshimiwa Spika, lakini swali lake la pili ufuatiliaji mimi nikuombe sisi Wabunge suala la ukatili wa kijinsia, suala la kulinda mama na mtoto liwe ni jambo la kudumu na hoja ya kudumu kwenye Vikao vyetu vya Baraza la Madiwani lakini liwe ni suala la kijamii lisibaki kuwa suala la Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii peke yake liwe ni tabia yetu ni kazi yetu sisi kama watanzania kuliona kwamba ni kipaumbele na katika ajenda zetu liwe jambo la kutunza kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, lakini sisi kama Wizara tutasimamia na kufuatilia kwa wakati wote kupitia hawa watu ambao wanakwenda kuajiriwa kila Kitongoji na kila Mtaa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 35

**Miradi ya maji katika Halmashauri ya Kisarawe**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha wananchi wa Kata ya Masaki – Kisarawe wanapata maji safi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti, Maalam kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Wananchi wa Kata ya Masaki Wilayani Kisarawe wanapata huduma ya maji safi na salama, Serikali kupitia *DAWASA* imekamilisha usanifu wa kina wa Mradi wa Maji Kisarawe. Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 kwa gharama ya bilioni 24 na ujenzi wake unatarajiwa kuchukua miezi 18.

Mheshimiwa Spika, kazi zinazotarajiwa kufanyika katika mradi huo ni pamoja na ulazaji wa bomba umbali wa kilomita 230, ujenzi wa tenki moja lenye ujazo wa lita 1,000,000 na ujenzi wa kituo cha kusukuma maji chenye tanki la lita 540,000 kitakachofungwa pampu mbili. Mradi huo ukikamilika utahudumia Kata tano za Masaki, Msimbu, Kibuta, Kazimzimbwi na Marumbo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kauli pendwa ya Mheshimiwa Waziri wa Maji Jumaa Aweso anasema maji hayana mbadala. Unapohitaji maji upate maji, Mheshimiwa Naibu Waziri utakuwa tayari kuambatana na mimi kuelekea Masaki kwenda kuwaambia wananchi juu ya kadhia hii ya maji?

Mheshimiwa Spika, lakini swali langu la pili na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri juu ya mpango huu lakini mpango huu unaonekana kuwa wa muda mrefu. Sasa ni kwa nini Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa gari ama mitambo ya kuchimba visima kwenye kila Mkoa ni kwa nini gari hiyo isiende Masaki na kuwachimbia kisima ili wapate maji safi na salama? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Hawa Mchafu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza; ni kuambatana nae Mheshimiwa Mbunge mantahofu baada ya Bunge hili tutapanga ratiba rafiki mimi na wewe tutafika eneo la tukio lakini vilevile Mheshimiwa Jafo amesema tutaongozana pamoja.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili; Mpango wa muda mrefu wa Mradi huu wa bilioni 24, sisi kama Wizara tuna miradi midogo midogo ambayo huwa tunaitekeleza na *DAWASA* wameishajipanga kuona kwamba lazima wataendeleza miradi midogo ambayo wananchi wataendelea kupata huduma wakati tunaendelea na mradi huu mkubwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, sasa aulize swali lake.

Na. 36

**Kupanda miti ya asili kwenye vyanzo vya maji**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali isitumie *aerial seeding* kupanda miti ya asili kwenye vyanzo vya maji nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na kampeni ya upandaji miti rafiki wa maji kwenye vyanzo vya maji ili kuboresha uhifadhi wa vyanzo vya maji. Ni kweli njia ya “*aerial seeding*”

inaweza kuleta ufanisi zaidi kwenye zoezi la upandaji miti kwenye vyanzo vya maji na itapunguza uchafuzi wa vyanzo vya maji kwa kudhibiti *plastic* zinazotokana na viriba vya miche ya miti. Hata hivyo, njia hii inahitaji uwekezaji mkubwa katika hatua za awali. Hivyo, mwelekeo wa Wizara ni kujipanga ili kuanza kutumia njia ya "*aerial seeding*" hasa katika maeneo ambayo hayajafikiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza hii *aerial seeding* ambayo tunaizungumza ni usambazaji wa mbegu kwa kutumia helikopta. Serikali inajibu kwamba ni njia nzuri na ni kweli Kenya wanafanya hivyo na wamefanikiwa kwa kiwango kikubwa na sisi kama Mheshimiwa Rais ana kampeni ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Kuna upandaji wa miti kibiashara wa miti kama mi-*pine* imekuwa ikiathiri sana vyanzo vya maji. Tathimini ipi imefanyika ya Serikali kujua miti hii ama iondolewe au iendelee kupandwa kwenye maeneo ya vyanzo vya maji hususani Makete? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Serikali ina mkakati gani wa dharura kwa sababu hali ya uharibifu wa mazingira kwenye vyanzo vya maji imekuwa ni kubwa tofauti na *aerial seeding* wanamkakati gani mwingine wa kuhakikisha kwamba vyanzo vya maji vinatunzwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, Festo Sanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tathimini ya miti ambayo siyo rafiki kwa vyanzo vya maji tulishaipiga marufuku na miti ambayo ni ya kibiashara hatuipandi katika vyanzo vyetu vya maji. Kwenye vyanzo vya maji kwa sasa hivi mkakati tunaoendelea nao ni kupanda miti rafiki na kukaribisha pia kilimo rafiki cha miti kama ya matunda ambayo hautifui eneo kubwa ili kupanda lakini unachimba shimo moja unapanda. Kwa hiyo, pia auharibu uoto

wa asili wa ile ardhi kuleta mmong'onyoko, kuingiza tope kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, miti ile ya kibiashara ilikuwa ni mambo ya huko nyuma lakini kwa sasa hivi Serikali ya Awamu ya Sita ni ya kisasa tunapanda miti ya kisasa rafiki wa maji na hapo Mheshimiwa Mbunge nitakuwa nimekujibu maswali yako yote mawili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani kuna haja ya kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, watu wa *TFS* maeneo ya milima wanayopanda miti ambayo mingine ni ya kibiashara inaharibu hivyo vyanzo vya maji na kwa hivyo inahathiri hata upatikanaji wa mvua na hayo yametokea kwenye milima mingi tu wanapanda miti, wanaondoa ile asili ambayo mwanzoni ilikuwa inazalisha maji nadhani utafiti pengine haukufanyika vizuri lakini athari ni kubwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mshirikiane Wizara ya Maji siyo lazima pale kwenye chanzo lakini hoja ni kwamba miti tu upandaji wake lazima utazame kwamba eneo gani miti hii huleta mvua, miti gani na mambo kama hayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo nadhani ni muhimu Wizara hizi mbili ziwe zinashirikiana zinapotaka kufanya hayo mambo ya kupanda miti na nadhani nyuma yako tu hapo yupo Mheshimiwa Naibu Waziri, anakuja hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, hauna ahaa na mwingine yupo Wizara ya Maji haya. Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 37

**Tathimimi ya visima vya maji mijini na vijijini**

**MHE. AZIZA S. ALLY** aliuliza:-

Je, Serikali imeshafanya tathmini kujua ni visima vingapi vimechimbwa hadi sasa na kama vimetatua shida yam aji Mijini na Vijijini nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara ya maji imetambua jumla ya visima 39,659 vilivyochimbwa katika maeneo ya Mijini na Vijijini nchini hadi sasa. Visima hivi vimesaidia kutatua changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji kwenye maeneo mbalimbali hivyo kuongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia 70.1 hadi 84 vijijini na mjini kwa mwaka 2021 kufikia asilimia 77 na 88 Vijijini na Mijini Disemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, kati ya visima hivyo jumla ya visima 854 vimechimbwa mwaka huu wa fedha 2023/2024 katika maeneo mbalimbali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, swali la nyongeza.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shida ya mwananchi ni kupata maji siyo kuona kisima. Je, Serikali imejiandaaje sehemu ambayo yenye visima vimechimbwa havitoa maji mpaka sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali ilitumia busara gani ya kuchimba visima vingi ambavyo havitoi maji badala ya kuchimba visima vichache ambavyo vitatoa maji ili viwasaidie wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kujibu maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imejiandaaje kuendeleza visima vilivyochimbwa. Sisi tayari tumejiandaa na tupo kazini Mheshimiwa Aziza, visima vyote vilivyochimbwa na ambavyo havikuendelezwa tayari tunavitengea fedha ili kuona kwamba tunafanya usambazaji kuelekea kwenye maeneo ambayo yalikuwa yamefanyiwa usanifu.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuchimba visima vingi visivyotoa maji sijaelewa hapa umemanisha nini kwa sababu visima vingi sisi tulivyovichimba vinatoa maji ila vichache kutokana na mabadiliko ya tabianchi unakuta pale chini unachimba lakini maji yanapatikana machache au hakipatikani maji ni masuala ya miamba ya mabadiliko ya tabiachi.

Mheshimiwa Spika, vingi tulivyovichimba vimekuwa na msaada kubwa na ndiyo maana tunasema tuna mageuzi makubwa ndani ya Wizara ya Maji. Kwa sababu visima hivi vimekuwa ni sehemu ya vyanzo vya maji kwa maisha ya mpito wakati tunaelekea kutumia maji ya maziwa makuu lakini mito mikubwa na vile vyanzo vyote ambavyo vitatufanya tuwe na miradi endelevu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 38

**Kudhibiti Tembo Tarafa ya Nkonko – Manyoni**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza:-

Je nini mkakati wa Serikali wa kudhibiti Tembo wanaoathiri Wakulima wa Tarafa ya Nkonko - Manyoni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dustan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya migogoro baina ya binadamu na wanyamapori nchini, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kusimamia Utatuzi wa Migogoro baina ya Binadamu na Wanyamapori kwa mwaka 2020/2024.

Mheshimiwa Spika, katika Tarafa ya Nkonko yenye vijiji vya Nkonko, Mpole na Mpapa Serikali kupitia Wizara imeendelea kutoa elimu ya uhifadhi na mbinu za kukabiliana na wanyampori wakali na waharibifu hususani tembo ili kuwajengea wananchi uwezo, kutoa mafunzo kwa mgambo kumi na tano (15) na kuwapatia vifaa vya kudhibiti tembo na kuendesha doria za udhibiti wa tembo katika vijiji vya tarafa hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha udhibiti wa Wanyamapori Wakali na Waharibifu Wizara imejenga kituo cha askari katika Kijiji cha Nkonko kilichopo Tarafa ya Nkonko. Aidha, kwa mwaka 2023/2024 Wizara imepanga kujenga kituo cha Askari Makao Makuu ya Pori la Akiba la Kizigo kwa ajili ya udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu katika Tarafa zenye changamoto hiyo ikiwemo Nkonko.

Mheshimiwa Spika, aidha, jumla ya Askari wa Vijiji *(VGS)* 24 kutoka vijiji vyenye changamoto ya Tembo wanaendelea na mafunzo ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu katika Chuo cha Likuyu Sekamaganga kilichopo Mkoa wa Ruvuma. Mafunzo hayo yanatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Februari, 2024 na baada ya hapo watashiriki kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kwenye maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kuna wakulima ambao waliathiriwa na tembo na vilevile kuna wananchi ambao waliathiriwa na tendo, je ni lini Serikali itawalipa kifuta machozi na mkono wa pole wakulima na Wananchi wa Tarafa ya Nkonko Manyoni ambao waliathiriwa na tembo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; nini mkakati sasa wa Serikali wa kujenga vituo vidogo *(rangers posts)* karibu na maeneo ambayo yanaathiriwa sana na tembo ili kusogeza huduma karibu na wananchi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wapo wananchi ambao walipata madhara ya kushambuliwa na wanyama hawa. Kuanzia Mwaka 2019 hadi Mwaka 2022, Wizara tayari imeshatoa kifuta jasho na kifuta machozi kwenye eneo hili la Wilaya hii, takribani shilingi 69,350,000. Katika mwaka huu tuna matukio karibu 226 ambayo tathmini imefanyika. Kwa sasa tuko katika hatua za mwisho za uhakiki ili wananchi hawa waweze kupatiwa fidia.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya pili ya swali lake, kuhusu ujengaji wa vituo vidogo; kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi; tayari tumeshajenga kituo kimoja kwenye kata hii, tunakusudia kwenye mwaka huu wa fedha, tujenge kituo kingine kikubwa ambacho kitaweza kuhudumia eneo kubwa zaidi. Kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana tutaendelea kujenga vituo hivi kwenye maeneo haya yenye changamoto za wanyama wakali na waharibifu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Je, ni ipi mikakati mipya ya Serikali ya kupambana na tatizo la mamba katika Jimbo la Mwibara? Kwa sababu, mamba wanaua watu kila kukicha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kajege, kama ifuatavtyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa ya kufanya utafiti kuona ni vitu gani vimesababisha kuwa na ongezego la wanyama hawa waharibifu ambao wamekuwa wakiathiri shughuli za kibinadamu lakini vile vile kuhatarisha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi yetu ya *TAWIRI* imekwishakuja na mikakati na kubuni mbinu ambazo zitasaidia kupambana na tatizo hili. Mojawapo ni kuja na mfumo wa kutengeneza vizimba kwenye maeneo yenye changamoto hii. Rai yetu ni kwamba teknolojia hii inapopelekwa kwenye halmashauri zetu basi halmashauri zitenge fedha kwa ajili ya kuitumia teknolojia hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile pale ambapo wanyama hawa wamekuwa ni wengi Serikali imefanya jitihada za kuhakikisha wanawindwa ili kupunguza changamoto hii kwa wananchi wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu waiziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge nimeletewa hapa mbele hoja za Wabunge ambao niliwapa nafasi ya kuuliza maswali kwa pamoja kuhusu barabara zilizoharibiwa na *TARURA*. Wakati Naibu Waziri alipokuwa anawajibu Wabunge hao kwa pamoja akataja majimbo mawili, akataja na kiasi cha fedha kilichotengwa. Majimbo mengine yaliyouliziwa fedha hizo hakutaja kiasi kilichotengwa na kwa hivyo Wabunge wale ambao hawajatajwa Majimbo yao wakati na wao waliuliza maswali wameleta hoja zao hapa mbele, kwamba kutokutajwa kwao wananchi hawaelewi

kama na wao wametengewa au Wabunge wao wameuliza halafu Serikali imetenga tu kwa ajili ya hayo maeneo mawili. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nitampa nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri ajibu hilo swali kwa kikamilifu ili wananchi ambao wabunge wao wameopata nafasi hapa ya kuuliza waweze kupata majibu. Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nashukuru tena kwa nafasi hii nyingine.

Mheshimiwa Spika, waliokuwa wameuliza mswali yale alikuwa ni Mheshimiwa Tendega, Mheshimiwa Ndulane, Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Chege, Mheshimiwa Noah, Mheshimiwa Taletale, Mheshimiwa Flatei na Mheshimiwa Gwajima ambao walikuwa wameulizia fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mkioa na Serikali za Mitaa, tumeandika kwa wenzetu wa Wizara ya Fedha kuomba shilingi 30,000,000,000 kama fedha ya dharura kwa ajili ya kwenda kutengeneza barabara ambazo zimeharibika sana kutokana na hizi mvua za *El Nino* zinazoendelea kunyesha hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, nilimtaja Mheshimiwa Gwajima kwamba, kuna shilingi 598,000,000 ambayo imeshakwenda, vile vile kwa Mheshimiwa Noah kuna shilingi 650,000,000 ya dharura ambayo tayari imeshakwenda. Na si tu kwa hao waliokuwa wameuliza lakini na maeneo mengine tathmini inaendelea na zinaletwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Ofisi ya *TARURA*. Na pale tutakapopata tathmini hiyo inayofanyika kule, fedha hiyo itakwenda.

Mheshimiwa Spika, nirejee kuwatoa mashaka Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mwigulu Lameck

Nchemba, wanalifuatilia kwa karibu jambo hili na kuhakikisha kwamba, fedha inapatikana kwa ajili ya kuweza kutatua changamoto ya barabara hizi ambazo zinaharibika katika majimbo yetu kote nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mbeya Mjini kuna shilingi 250,000,000 ambayo imekwenda katika kuhakikisha inatatua changamoto ambazo zinajitojkeza na udharura huu wa barabara ambao upo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona Waziri wa Fedha umesimama.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nilitaka niwahakikishie na Wabunge ambao hata hawakupata nafasi ya kuuliza kwamba kadri mvua zilivyokuwa zinaendelea, Mheshimiwa Rais aliielekeza Wizara ya Fedha kuandaa fedha kwa ajili ya hii dharura; na hiki alichokisema Mheshimiwa Naibu Waziri, fedha hizo zitatoka kabla Bunge halijaisha ili barabara ziweze kutengenezwa na wananchi waweze kunufaika na fedha hizi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Kabla sijaleta matangazo niliyonayo hapa mbele, mambo mawili.

La kwanza, nimuombe radhi Mheshimiwa Condester Sichalwe, nilikuwa nimemtaja kwenye maswali ya nyongeza lakini hakuwa yeye. Aliyekuwa amesimama alikuwa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi. Lakini leo ni kwa sababu wamevaa sare, wote wamevaa makoti meupe, kwa hiyo kidogo nilimuona Mheshimiwa Condester muda fulani nikadhani ni yeye. Nikuombe radhi Mheshimiwa hukuwa wewe uliyesimama kuomba swali na nilikutaja wewe, lakini baadaye nikagundua ni Mbunge mwingine wa Muhambwe, kwa hiyo akapewa nafasi. Kwa hiyo, nikuombe radhi.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ambalo nafikiri ni la muhimu pia kuzingatia; kipindi cha maswali na majibu ni kipindi ambacho kwa kweli ni kizito kwa Mbunge yeyote na ni kizito kwa upande wa Serikali vivyo hivyo. Hii ni kwa sababu Mbunge yupo hapa kuwakilisha wananchi na Serikali iko hapa kutoa majibu kwa hoja ama maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Sasa wakati mwingine Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tunawaona Mawaziri au Naibu Mawaziri wanakuwepo kipindi cha maswali hapa basi tunatumia pia kipindi hicho kwenda kuzungumza nao kuhusu hoja zetu.

Sasa kwa sababu ya changamoto ambazo huwa zinajitokeza mara kadhaa, na ninasema mara kadhaa kwa sababu wakati mwingine swali la nyongeza linaulizwa ambalo linahusu Wizara ambayo pengine wanapaswa kufanya kazi pamoja na huyo ambaye yuko hapa mbele. Kwa hiyo, siyo swali ambalo unaweza kusema litakuja kujibiwa kama swali la msingi ama namna hiyo.

Kwa hiyo, anajikuta Waziri ama Naibu Waziri anatajwa kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, ama kwa sababu wa Elimu huwa mara nyingi anakaa hapa hawamfuati sana watu, kwa hiyo yeye kidogo anakuwa na muda wa kusikiliza; kwa hiyo, ni rahisi kumwambia Mheshimiwa Waziri wa Elimu, sikiliza swali lako hilo hebu jibu. Lakini, wengine mnakuwa mnazungumza nao hata nikimatazama naona kabisa hana utayari wa kujibu swali hilo kwa sababu hajui kilichoulizwa. Kwa nini; kwa sababu sisi Wabunge tunakuwa tumekwenda pale; na Waziri hawezi kusema ondoka, nasikiliza maswali yanayoulizwa.

Sasa hii imekuwa ikileta changamoto mara kadhaa na wakati mwingine mnasema hampati majibu yaliyo sahihi ama wakati mwingine yenye uhalisia. Kwa muktadha huo Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu kipindi cha maswali na majibu siyo kirefu sana, ni kipindi kifupi; ili tupunguze pia ile mizunguko, wapeni nafasi Mawaziri wasikilize maswali yenu, ili waweze kuyajibu. Wapeni nafasi Mawaziri, kipindi cha maswali usiende kuzungumza nao. *(Makofi)*

Wako hapa kwa ajili ya kujibu hoja za wananchi. Wote pamoja na za kwako. Lakini wewe kwa sababu umeamua kuzungumza bila kusema humu ndani, bila kusimama umeamua kwenda basi subiri kipindi cha maswali na majibu kipite, na wanapoanza michango Waheshimiwa Wabunge unaweza kwenda kumuona Waziri. Nadhani utaratibu huo utaiweka Serikali katika mazingira mazuri ili mtu asije kuwa anashtukizwa kujibu swali kwa sababu anakuwa hajasikiliza vizuri. Wakati mwingine mnakwenda kuwaongelesha hata Waziri anayekwenda kujibu maswali. Sasa unajikuta kwamba kidogo inakuwa mtihani. Kwa sababu ni kweli, hapa nilimuita Mheshimiwa Mwigulu lakini baadaye nikagundua kuna Mbunge pale alikwenda kumueleza, sasa yeye Waziri atamwambiaje Mbunge kwamba, bwana Mbunge mimi nina swali nipishe nasikiliza kwa Spika, je nimeitwa Wizara yangu au hapana? *(Makofi)*

Kwa hiyo, nafikiri ili kuondoa huo mkanganyiko na kuipa Serikali nafasi ya kusikiliza maswali yenu, msiende kwenye viti vya Serikali wakati wa kipindi cha maswali na majibu. Hiyo pia itasaidia humu ndani kwa sababu pia kunakuwa na wageni na kelele zinakuwa nyingi kwa ajili ya kuzungumza. Nadhani tukienda hivyo tutaondoa hii changamoto ya maswali yetu kutokujibiwa kikamilifu. Kwa hiyo, hilo limeshaeleweka Waheshimiwa Wabunge na sasa nilete tangazo la wageni kwenu.

Tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika; ninao wageni 73, nadhani wote hawa wamejumlishwa kwa pamoja.

Haya, tunayo Kamati ya Uanzishwaji wa *TASSIM (Tanzania Association of Small-Scale Industries and Manufacturers)* ambao wamekaa Jukwaa la Spika; hawa ni Ndugu Masoud Ali Kipanya, karibu sana. *(Makofi)*

Sasa uniwie radhi sina hakika sana kama hii Kipanya ni jina la kazi au ni jina lako halisi, lakini hapa limeandikwa kama jina halisi. Niwie radhi kama ni jina la kazi. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Bennet Kakorozya; yupo *Brigadier General* Msuya; yupo pia Ndugu Anna Urio; yupo Ndugu Sophia Jamal;

yupo Ndugu Bertha Mwaipopo; yupo Ndugu Twaha Kitogo; yupo Ndugu Steven Cornelius; yupo pia Ndugu Sayuni Madeye; yupo Ndugu Pardon Kasike; na yupo Ndugu Jackson Ruhaha, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 61 kutoka Chama cha Walimu Tanzania, Idara ya Walimu wenye Ulemavu wakiongozwa na Ndugu Ulumbi Shabani, ambaye ni Mwenyekiti. Haya karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao Madaktari Bingwa 11 kutoka Taasisi ya Mifupa *(MOI)* ambao wapo Bungeni kwa ajili ya kuelezea huduma maalumu ya matibabu kwa viongozi iliyoanzishwa na taasisi hiyo. Aidha, watatoa huduma za ushauri na upimaji wa magonjwa kama vile mifupa, magoti, nyonga, ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu, karibuni sana madaktari wetu, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Haya tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Omari Kipanga ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, na hawa ni Bi. Sumayya Suleiman Khamis, ambaye ni mke wake; ameongozana hapa na shemeji yake Ndugu Khairat Abdul-Kadir Abdalla na Ndugu Hassan Mzee Jalala, mdogo wake, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri, ni yupi hapo? Karibu sana Bungeni, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko salama, usiwe na wasiwasi. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 80 wa Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally ambao ni Umoja wa Wanawake Tanzania kutoka Wilaya ya Uyui, Mkoa wa Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Neema Lugangira kutoka Dar es salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya ambaye ni mpiga kura wake kutoka Nyasa, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Vita Kawawa ambao ni Wakaguzi wa Kampuni ya *World Financial Group* kutoka Canada, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; washirika tisa wa Jumuiya ya Samaria Ntyuka kutoka Dayosisi ya *Central Tanganyika Dodoma*, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 100 ambao ni Taasisi Isiyo ya Kiserikali ya Timu Ushindi kutoka Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Hii timu ushindi nafikiri ni muhimu sana kujiunga nayo hasa kwa zile timu zenye kushindwa sana. Sijajua ni timu ushindi wa nini lakini maadamu ni timu ushindi nadhani zile timu zinazoshindwa sana zinaweza kujiunga na hii timu ili ziwe zinashinda. Haya ahsanteni sana, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Paschal Gagara Mugodi kutoka Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndiyo wageni tulionao hapa Bungeni na hakuna matangazo mengine hivyo tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023

**Muswada wa Sheria wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 *[The Political Parties Affairs Laws (Amendment) Bill, 2023]***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma, Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, ajiandae.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, awali ya yote ningependa kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na kutujaalia kufika hapa kuzungumza na kuchangia katika mjadala huu au mijadala hii au miswada hii ambayo, ni muhimu sana katika mustakabali wetu wa kisiasa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sheria na miswada ya sheria ni mchakato *(process)*. Mchakato unatupeleka wapi na umetutoa wapi? Katika kila jambo kuna dhamira, kuna mchakato na kuna matokeo. *Stage* tuliyokuwa nayo hii ni *stage* ya mchakato. Ili tuielewe vizuri lazima tuelewe dhamira ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna walionitangulia wakazungumza kuhusu *4R* za Mheshimiwa Rais. Zile *4R* zilitokana na nini? *4R* zimetokana na hali ya kisiasa ilivyokuwa alivyoingia yeye madarakani. Hali hiyo imekuwa hivyo kwa sababu ya mambo yaliyotokea huko nyuma. Niwakumbushe, mikutano ya hadhara ilikuwa haifanyiki, yale ambayo tunayazungumza hapa yalikuwa hayaonekani kwa wananchi kwa ujumla, mijadala ya kisiasa nje ya kipindi cha uchaguzi ilikuwa ni jambo ambalo halichukuliwi kwa umuhimu. Sasa, baadhi ya wananchi wameona hili jambo ni la msingi na uongozi wetu baada ya kutathmini ikaona kweli hili jambo ni la msingi.

Mheshimiwa Spika, sasa tunafanyaje ili kuweka hali ikawa sawia na sehemu yote katika tasnia ya siasa ikawa sawa? Ndiyo ile initiative ya Mheshimiwa Rais ya R nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa katika lile tukaletewa Miswada mitatu. Muswada wa kwanza unashughulikia masuala ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Mwingine kuunda Mfumo wa Tume ya Uchaguzi na mwingine Sheria ya Kuongoza Vyama vya Siasa. Mambo yote ni ya msingi katika jamii.

Mheshimiwa Spika, Askofu Bagonza anapenda kutukumbusha siku zote kuwa amani ambayo ndiyo mtaji wetu ni tunda la haki, amani inapatikana ndani ya jamii kama kuna mustakabali mzuri na maelewano mazuri baina ya watu wote na vyama vyote. Sisi tumekuwa kisiwa cha amani kwa sababu mutakabali huo umekuwepo kipindi chote, sasa haya yote mabadiliko yameletwa ili ule uwanja wa kisiasa uwe tambarare kwa kila mtu, kila mtu aweze kucheza huu mchezo wa kisiasa bila kuingiliwa na bila matatizo. Sasa tunafanyaje? Tunafikaje huko?

Mheshimiwa Spika, kuna mambo makuu mawili; jambo la kwanza ni uwazi na la pili ni ushirikishwaji. Uwazi *(transparency)* mabadiliko yafanyike wazi watu wote wayaone na usirikishwaji kuwaleta wananchi watanzania wenyewe waje kutuambia na kutupa maoni yao. Mchakato mimi niko Bungeni na Mbunge wa Jimbo huu ni mwaka wa tatu, tumepitisha Miswada mingi, lakini hakuna Miswada, ambayo imepokea maoni mbalimbali ya wananchi kama Miswada hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji umekuwa mkubwa, nyanja mbalimbali, vyama vya siasa vyote vilikuja, taasisi na asasi za kiraia zilikuja zikaleta maoni, viongozi wa dini walikuja, viongozi wa kimila walikuja, raia mbalimbali binafsi wamekuja na wote kabisa wakatoa maoni yao na wote wakasikilizwa na tukayapokea. Sasa, *challenge* ya mambo hayo makuu, uwazi na ushirikishwaji ni lazima maoni uyapokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa maoni fulani huyaungi mkono, lakini wamekuja wengi wanayataka. Sasa

wajibu wa ushirikishwaji, *context* ya ushirikishwaji, kama mtu unaweza kusema ukadai kwamba umewashirikisha maoni lazima uyapokee. Kwa hakika baada ya kusoma mara ya kwanza na ripoti hii ni bayana kabisa kwamba maoni ya Watanzania yamepokewa na yamo yameingizwa katika hii Miswada yote mitatu, hiyo ndiyo *context* tulikotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wakati tunajadili na tunachambua na tunafikiria, alikuja akatushauri Profesa mmoja mwenye maarifa makubwa sana na uelewa mkubwa sana, Mheshimiwa Prof. Kabudi, alibahatika yeye kufanya uchambuzi wa kina juu ya mifumo ya kichaguzi na anasema kwa bahati nzuri ameweza kuchambua mifumo karibu ya ulimwengu mzima, nchi zilizoendelea na nchi kama zetu ambazo zinaendelea na kitu ambacho amekikuta ambacho ni *common ground* kote kwenye mifumo ambayo inakubalika na mifumo ambayo watu wanaifurahia kuna mambo makuu matatu, kuna uadilifu, kuna uaminifu na kuna uzalendo, hayo mambo makuu matatu ni muhimu zaidi kushinda mfumo wenyewe ulivyo *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imedhihiri kwamba hata mifumo bora kabisa iliyokuwepo kama uadilifu haupo, uaminifu haupo na uzalendo haupo mfumo hautafanya kazi. Sasa tunafanyaje? Hizo sifa ni za watu na si za mifumo, inabidi zile sifa tuziingize kadri itakavyowezekana kutengeneza mifumo ambayo italeta uadilifu, italeta uaminifu na itahakikisha uzalendo unatendeka katika uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo basi, ndiyo maana Kamati na ninashukuru sana uongozi wa Kamati pamoja na Serikali kwa kuwa wasikivu na kwa kufungua mjadala mzima na kuruhusu watu kuleta maoni na kupokea maoni hata yale ambayo, kama Kamati au mmoja-mmoja hatukuwa tunayaunga mkono kwa sababu dhamira ni ushirikishwaji. Watanzania na makundi yote ya Kitanzania maoni yao yasikilizwe na yaletwe katika hii Miswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kuyagusia hayo, ningependa kugusia vipengele vichache na sitatiririka kwa sheria

hadi sheria, nitazungumzia yale ambayo kwa kipindi kirefu wakati sisi tupo katika mchakato wananchi wengi wameyazungumza na wameona yanahitaji marekebisho ya maoni ambayo yalikuwa mengi.

Mheshimiwa Spika, suala la Wakurugenzi hili limezungumzwa kwa kina na kwa kweli Serikali yetu sikivu imepokea *proposal* ambayo ilitoka kwa watu wengi. Wakurugenzi, turudi palepale tena yale mambo makubwa matatu, tatizo siyo ofisi, tatizo siyo mtu, tatizo ni nini, uadilifu, uaminifu na uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa inawezekana kabisa Mkurugenzi akafanya kazi kwa misingi hiyo mitatu, lakini kwa sababu wadau wengi walikuja wakayazungumza, tukaona tubadili ili tutoe *comfort*. Sasa mfanyakazi yeyote Mwandamizi wa Serikali anaweza akasimamia, sasa tunaangalia sifa zake kama ana uadilifu, ana uaminifu ni mzalendo tutampa kazi ataifanya. Sasa hayo yote yalikuwa ya msingi.

Mheshimiwa Spika, suala jingine lilikuwa katika Kamati ya usaili, vilevile Serikali yetu ilikubaliana nalo. Kamati ya usaili Wajumbe hakuna hata mdau mmoja aliyezungumza akaweka dosari juu ya Wajumbe waliokuwemo katika Kamati ya usaili. Jaji Mkuu, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Majaji wote, watu wote walikuwa wako sawa, lakini Mkurugenzi karibu kila aliyekuja kuleta maoni alisema hili hapa lina tatizo.

Mheshimiwa Spika, sasa inawezekana kabisa mimi namjua Mkurugenzi wa Uchaguzi ni mtu muadilifu sana, angeweza kuifanya hii kazi kwa uadilifu, lakini hatutengenezi sheria kwa macho au kwa mtu, tunatengeneza sheria ili jamii ione kwamba, tumesikia na tume-*address*. Nayo vivyo hivyo tumekubaliana Muswada wetu utabadilika na Mkurugenzi yule hatakuwa Mkugenzi wa Kamati ya Usaili ambayo itachagua watu kwenda kwenye Tume ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maamuzi ya ndani ya Chama, sehemu ya Muswada wa Vyama vya Siasa iliweka utaratibu wa kwamba, ambao uliendana na hukumu ya Mahakama,

ilizungumzia kwamba maamuzi katika vyama vya siasa, maamuzi yakifanyika katika ngazi ndogo wale waliofanya maamuzi wasihusike tena katika ngazi kubwa katika utekelezaji wa yale maamuzi. Hii kidogo ilikuwa na mkanganyiko, Taasisi yoyote ambayo ina watu wengi maamuzi hufanywa katika kile kikao ambacho kina watu wengi. Ndani ya Bunge maamuzi Bunge ndiyo linaamua, lakini ili ufanye maamuzi lazima sisi utugawe katika vipende vidogo-vidogo, tuchakate, halafu tulete hapa kwa mapendekezo kama Kamati za Bunge. Kamati za Bunge hazifanyi maamuzi, lakini zinachakata zinaleta hapa, sisi tunafanya maamuzi, lakini tukisema wale waliokuwa katika Kamati ya Bunge wasije hapa wakashiriki katika maamuzi haya, kweli ni sawa? Siyo sawa! Kule hawajafanya maamuzi, wanaleta mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika na vyama vya siasa, Mkutano Mkuu wa Chama au Halmashauri Kuu ya Chama haiwezi ikafanya maamuzi yote, sasa kama kuna maamuzi ya kinidhamu yataanza ngazi ya tawi, wataleta mapendekezo, litakuja Jimbo, itakuja Wilaya, utakuja Mkoa, ikifika Taifa huwezi ukasema wote wale wasiingie kwa sababu wale hawafanyi maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hoja hiyo na mantiki hiyo, sisi kama Kamati, tulipinga kipengele hiki na kwa hakika Serikali ilikuwa sikivu ikasikia, lakini kwa muktadha wake ndiyo hivyo mabadiliko lazima yaendane siyo tu Katiba na sheria zilizokuwepo bali na utamaduni, mila na utaratibu wa vyama vya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ningependa kugusia suala la jinsia. Limezungumzwa sana jana na nimeguswa sana na Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, Mheshimiwa Keisha na wengine ambao wamelizungumza hili kwa uchungu mkubwa na kwa *experience* zao wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani maendeleo yakafanyika bila nusu ya Taifa, akina mama kwa kipindi kirefu wanashindana na sisi lakini ule uwanja haupo sawa kwao na kwetu kwa sababu nyingi sana za kijamii. Sasa tusione sasa hivi akinamama wa shoka wapo wengi maana kuna njia mbili za kuleta mabadiliko ya aina

hiyo, njia ya kwanza ni ya haraka ya uteuzi, Mheshimiwa Rais amejitahidi amefanya uteuzi mabadiliko yanakuwa yako juu. Kuna Waheshimiwa wengi tu hapa, kuna Mheshimiwa Angela Kairuki, Mheshimiwa Stagomena Tax Waziri wetu wa Ulinzi, kuna Mheshimiwa Spika pale na wengi ambao wana uwezo mkubwa na wako juu, lakini tukitaka maendeleo endelevu lazima yaje chini, mifumo yetu chini. *(Makofi)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, idadi ya wanawake kwenye chaguzi za Serikali za mitaa hiyo ndiyo siri kubwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdullah Mwinyi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Condester.

**TAARIFA**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwinyi amepitiwa kidogo, Spika ni Mbunge wa kuchaguliwa. *(Makofi)*

**MHE. ABDULLAH ALI WINYI:** Mheshimiwa Spika, taarifa nimeipokea.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Mwinyi taarifa hiyo.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea taarifa, sikuwa na maana ya Mheshimiwa Spika ameteuliwa ili uchaguliwe lazima vigezo uwe navyo na vigezo anavyo, na hao wote waliochaguliwa vigezo wanavyo, lakini mabadiliko makubwa ni ya kuchagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mabadiliko endelevu ya muda mrefu ni ya uchaguzi wa chini, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Madiwani, lazima tuwe tuna sera na mfumo wa maksudi kuhakikisha wanawake katika ngazi za uchaguzi wa chini wanashiriki kwa wingi mno. Sasa haya hayawezi yakaachwa kwa watu

wakajifanyia watakavyo, lazima sera na sheria iainishe umuhimu wa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, ningependa kuunga mkono hoja, nakushukuru na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira ajiandae.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kutoa mawazo yangu kwa niaba yangu na kwa niaba ya Taifa letu katika Miswada hii ya sheria iliyopo mbele yetu. Kama watangulizi wenzangu na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwanza kwa nafasi ambayo ameendelea kutupa ya upendeleo ya kuwa hai, kuwa wazima, lakini ya kuwa viongozi katika Taifa letu hili.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu uanze kujielekeza katika Muswada wa Tume ya Uchaguzi kwa haraka. Muswada huu unaonesha dhamira nzuri kabisa ya kuendelea kujenga uwazi na kuendelea kuimarisha demokrasia ambayo imekuwa ni desturi ya Chama cha Mapinduzi kilicho madarakani kutoa elimu kwa nchi nyingine zote Barani Afrika juu ya namna bora ya kutekeleza demokrasia.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umejiekeleza katika utaifa wetu, Taifa letu ni la muungano, mapendekezo haya ya maboresho yameendelea kulinda hadhi ya muungano katika muswada huu na ndiyo maana muswada unatamka wazi kwamba, tutakuwa na Mwenyekiti wa Tume akiwa upande huu Makamu wake atatoka upande wa pili wa Muungano pamoja na Wajumbe wengine.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba tuboreshe ni katika Ibara ya 18, Sekretarieti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Muundo wa Mwenyekiti wa Tume pamoja na Wajumbe wake umekaa katika taswira ya kimuungano, ningetamani Serikali ione tunavyoweza kutengeneza Naibu Mkurugenzi Mkuu atakayeshughulikia

masuala ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Muungano kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano huo upo, Mrajisi wa Vyama vya Siasa ni jambo la kimuungano, tunae Mrajisi wa Vyama vya Siasa anayeshughulikia masuala ya vyama vya siasa, lakini tunaye Naibu Mrajisi wa Vyama vya Siasa anayeshughulikia *specific* masuala ya Zanzibar katika masuala ya vyama vya siasa. Sasa ninadhani katika maboresho yetu ya muswada huu wa sheria iwepo nafasi ya Naibu Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi ambae atafanya shughuli zeke Zanzibar, atakayesimamia masuala ya kimuungano katika uchaguzi na kuyawasilisha kwa bosi wake Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatamani jingine pia kuliona katika kutekeleza majukumu ya Tume ya Uchaguzi, majukumu ya Tume ya Uchaguzi hapa yameelezwa mengi katika Ibara ya 11, ningetamani liongezwe jingine moja, kutoa elimu ya kupokea matokeo kwa viongozi wa vyama vya siasa. Nadhani viongozi wa vyama vya siasa wengine hawana elimu ya kupokea matokeo, Tume ina wajibu wa kutoa elimu hapa kwa wapiga kura ili wajue namna ya kwenda kupiga kura na wajitokeze. Sasa kiongezwe kipengele basi cha kutoa elimu ya namna ya kupokea matokeo.

Mheshimiwa Spika, kushindwa kwa baadhi ya viongozi katika chaguzi ndiyo kunaleta kitahanani katika Taifa, kumbe labda kwa sababu hawana tu elimu. Kwa hiyo, nadhani kiwekwe kabisa kipengele katika muswada huu, moja ya majukumu ya Tume ni kuwafunza wanasiasa kupokea matokeo, wakishindwa wajue huyu ameshindwa.

Mheshimiwa Spika, Chama changu cha Mapinduzi ni wazoefu wakubwa wa kupokea matokeo ya kushinda na kushindwa. Kwa hiyo, nadhani sisi ndani ya Chama chetu tumefundishwa sana pale tunaposhindwa tunahimili, tunasubiri miaka mitano tunaendelea, nina wasiwasi na vyama vingine vya upinzani kama kwao wanapeana elimu ya kupokea matokeo ya uchaguzi. Sasa nataka nione Tume ya Uchaguzi ina wajibu wa

kisheria wa kuwafundisha ukishindwa kubali, tulia, unga mkono tujenge Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, ningetamani katika sheria hii uwepo utaratibu wa siku maalum ambayo wengine wanaita *healing day*. Utaratibu huo upo katika mataifa mbalimbali, Zimbabwe upo, kampeni zinakwisha leo, kesho hapana kabisa kampeni, wananchi keshokutwa ndiyo wanakwenda kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, hiyo itasaidia nini? Kwanza kushusha joto la siasa kuelekea uchaguzi, kama kampeni tutamaliza leo, kesho watu watapumzika watafanya shughuli zao nyingine, keshokutwa wakienda kupiga kura tutashusha joto la siasa, tutawapa nafasi wananchi kufikiria namna bora ya kufanya maamuzi baada ya kusikia kauli za wanasiasa na kuona yapi ambayo yanafaa. Kwa hiyo, katika majukumu ya Tume ya Uchaguzi, itakuwa ni kusimamia uchaguzi, ningetamani na hili nalo walione katika utaratibu wao wa kusimamia uchaguzi namna bora ya kwenda nalo.

Mheshimiwa Spika, miswada yote iliyokuja katika Bunge hili ni nia njema ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, na nia njema ya chama chake kilichomuweka madarakani katika kuhakikisha Watanzania wanapata yale wanayoyatamani kuimarisha demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nia njema ya Rais ikawa nia njema ya Serikali. Serikali ikaleta muswada katika Bunge lako, nia yako njema ukaupeleka muswada kwa Kamati yetu ya Bunge, nia njema ya Kamati ya Bunge ambayo ina asili ya nia yako njema ikatoa nafasi kwa wananchi mbalimbali kuja kutoa mawazo ya namna ya kuboresha sheria yetu. Sasa wale wanaohoji nia njema wanataka nia njema gani zaidi ya hii? Nia njema ya Rais wetu, nia njema ya Serikali yetu, nia njema ya Spika wa Bunge kuupokea muswada na kuuleta katika Bunge na kuielekeza Kamati yetu ipokee maoni ya wananchi na nia njema ya kwetu sisi Wabunge kuujadili muswada huu au wanataka nia njema ya namna gani?

Mheshimiwa Spika, wapo watu wana tabia ya kutengeneza hofu katika mioyo ya watu ili kupandikiza chuki. Mara nyingi watu hawa ni sisi wanasiasa na uzoefu wangu mara nyingi hutendwa na baadhi ya wanasiasa wa vyama vya upinzani. Sasa kama umemkaribisha mgeni nyumbani kwako umemwambia karibu, nimekukaribisha nyumbani tuje tule chakula cha mchana, ilivyofika pale saa tano ukamuuliza unataka kula nini? Kwa sisi Wazanzibari akasema nataka kula wali na mchuzi kidogo. Ukamuandalia wali na mchuzi ukamkaribisha mezani, halafu bado anakuuliza hivi kweli unataka kweli mimi nile? Ndicho ambacho baadhi ya wanasiasa wa Upinzani wanataka kuwaaminisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameridhia, mawazo mbalimbali yameletwa, na Muswada ukaletwa Bungeni; Mheshimiwa Rais akaleta Miswada hii katika Bunge hili, ukaipokea. Kila anayehoji nia njema ana dhamira ya kupandikiza chuki. Nawaomba Watanzania wenzangu tusiipe nafasi dhamira hiyo, kwa sababu ni dhamira mbaya kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa hapo mwanzo wakati naanza nilizungumza majukumu ya Tume. Naomba nisisitize tena, majukumu ya tume katika kuongeza ile nafasi niliyoisema ya kupokea matokeo. Kila ambapo wapinzani walishindwa uchaguzi, basi walisema hawana imani na baadhi ya watu, mpaka sheria hii ikaenda kupendekeza kuondoa baadhi ya watendaji wa Serikali kusimamia uchaguzi. Hayo yote yanatokana na kutokukuwa na uwezo wa kuhimili kupokea matokeo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naipongeza dhamira njema ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Dhamira hiyo ndiyo dhamira ya Chama chetu cha Mapinduzi kuleta mabadiliko na kuimarisha demokrasia katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda watu wamesahau. Mwaka 1992 ni CCM hii hii iliyokuwa madarakani leo ndiyo iliyoruhusu uwepo wa vyama vingi katika Taifa hili. Ingeweza isiruhusu. CCM hii hii iliyoruhusu uwepo wa vyama vingi ndiyo hiyo hiyo iliyosababisha

baadhi ya Wabunge humu ndani wakawa wapinzani. Tusingeruhusu wasingekuwepo. Ni CCM hii hii imeielekeza Serikali yake kupitia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, leo imeleta Muswada huu kwa maslahi ya Watanzania, kwa sababu CCM wajibu wake ni kulinda maslahi ya Watanzania. Hivyo, Rais wetu na Chama cha Mapinduzi, kina dhamira njema katika kuboresha maslahi ya Watanzania na demokrasia katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie katika masuala ya kijinsia. Mimi nina Watoto, na watoto wangu wengi ni wa kike, warembo kweli kweli, *Mashallah*! Kuna nyakati nikikaa huwa nawatazama hivi; wakubwa wana miaka nane, ni mapacha. Huwa nawatazama na nasema ah, Mungu ameumba viumbe vizuri sana katika dunia hii. Mwenyezi Mungu awajalie kila la heri. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Amen!

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Spika, ni lazima sasa masuala ya kijinsia yawe katika makosa ya kiuchaguzi. Kila ambalo linatendeka la kudhalilisha jinsia ya mtu wakati wa uchaguzi, dhamira yake ni kumwondolea kura yule mgombea. Sasa tukiacha jambo hili lishughulikiwe katika utaratibu wa kawaida, hapana. Mwanasiasa anaposimama katika viriri, katika majukwaa ama nje ya majukwaa, akamwongolea kwa kumdhalilisha jinsia, iwe mwanamke iwe mwanaume, dhamira yake ni moja tu. Kumwondolea kura na asishinde uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini kosa hili lisiingie katika makosa ya kiuchaguzi? Kwani nani hajui kama rushwa ni kosa wakati wote? Kwa nini rushwa imeingia katika makosa ya kiuchaguzi? Kwa nini udhalilishaji wa kijinsia usiingie katika makosa ya kiuchaguzi? Japo wanaume wanadhalilishwa lakini kwa uchache, wanawake wanadhalilishwa sana katika masuala ya kiuchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatutakuwa na Taifa lililo imara kama mikono ya mwanamke itakuwa inachafuliwa kwa makusudi, eti

kwa sababu asishinde uchaguzi. Hili lazima liingie. Napendekeza sana Bunge lako na Serikali yetu Tukufu isikie, rushwa, hongo ni makosa wakati wote, lakini pia ni makosa ya kiuchaguzi. Dhambi ni nini masuala ya udhalilishaji wa kijinsia ukiingia katika makosa ya kiuchaguzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. Naunga mkono hoja pamoja na Marekebisho. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, ajiandae.

**MHE. ELIBARIKI I KINGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kabla sijaanza kutoa mchango wangu, naomba sana Bunge lako Tukufu na wananchi waliko nje wanaofuatilia mijadala ya Bunge kuhusiana na Miswada hii mitatu, kwa sababu najua vipindi hivi vinaangaliwa na Umma wote, wananchi wa Tanzania kule nje wajue nini Serikali ilichokileta Bungeni na nini Wabunge wao ambao ndio Wawakilishi wa walipakodi kule nje wanachokijadili *whether* kina maslahi kwao ama hakina. Kwa hoja zangu nitakwenda kujibu hayo maswali mawili niliyoyaweka.

Mheshimiwa Spika, toka Taifa letu lipate uhuru mwaka 1961, tumekuwa na Serikali ambayo mifumo yake ya kisiasa ilikuwa ni mfumo wa chama kimoja. Mabadiliko yaliyofanyika kuanzia miaka ya 1990 – 1995 yalisababisha Taifa letu kuingia katika mfumo wa Siasa za Vyama Vyingi katika ushindani wa siasa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, yamekuwepo malalamiko mengi ya baadhi ya vyama vya siasa kutaka uwanja sawa wa kiushindani katika siasa. Vyama vya siasa vimekuwa vikilalamika juu ya kitu kinachoitwa Tume Huru ya Uchaguzi; na pia vyama vya siasa vimekuwa vikilalamika namna gani Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi wanavyopatikana, wanavyoweza ku-*reflect independence* yenyewe ya Tume hiyo ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, ukiachilia mbali hilo, pamekuwepo na malalamiko pia huko pembeni na huko mtaani ambayo yamekuwa yakionesha huenda labda kuna namna fulani ya uonevu ambao unafanywa kwa vyama vya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, nataka niliambie Bunge lako Tukufu kwa dhati ya moyo wangu, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika suala zima la kuleta *reforms* ambazo zimetajwa katika zile R4 ambazo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa akizisimamia kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikupe mifano ifuatayo: Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 74, ukiisoma Katiba hii, imempa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka ya kumteua Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, lakini kwa kuona dhamira safi ya Rais huyu, Rais Samia anakuwa Rais wa kwanza Mwanamama kwenye Taifa letu na Ukanda wa Afrika Mashariki kuamua kuyapunguza madaraka yake na kuruhusu sheria itungwe itakayotoa utaratibu wa kupatikana kwa Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi tofauti na ilivyokuwa mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikupe mfano. Mataifa mengi hususan Barani Afrika, yanaingia kwenye migogoro ya kivita kwa sababu ya viongozi kutokuwa wasikivu. Rais Samia amesikilia kilio na *demand* ya vyama vya kisiasa Tanzania. Rais huyu amepewa mamlaka Kikatiba lakini bado ametumia hekima ya kuyapunguza mamlaka yake ya kuteua watu moja kwa moja na kuruhusu sheria ziundwe za kutengeneza utaratibu wa namna ya kupatikana kwa Wajumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais Samia anaingia katika historia ya kukumbukwa kwa kuandika kitu ambacho kinakwenda kuacha *legacy* ya utulivu wa kisiasa katika Taifa letu. Maneno haya nayasema kwa sababu, kwa dhamira hiyo njema, kuna watu wanatoa mifano ya mataifa; sitataja taifa lolote, lakini kuna watu wanatoa mifano ya mataifa ya nje.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Ibara ya 74(9), Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa ufafanuzi wa namna ambavyo maamuzi yatafikiwa na Tume. Leo tunapozungumza, kuna mataifa huko nje wanakubaliana Wajumbe wawili wanafanya maamuzi na imetoka hiyo, lakini Rais Samia ameleta sheria kwenye Bunge hili. Watanzania wasidangwe nje. Mabadiliko makubwa ambayo yamepigiwa kelele, Serikali ya Rais Samia imesikiliza na imeleta mapendekezo ambayo yatakwenda ku-*harmonize political atmosphere* ya Taifa letu huko nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nayasema haya, kuna baadhi wanalalamika na wananchi nje watusikilize. Kuna baadhi wanasema, inakuwaje Rais anapewa madaraka ya kuteua Wajumbe? Nenda kasome *Malawi Electro Commission* inavyopatikana. Tume ya Uchaguzi ya Malawi, Rais amepewa mamlaka ya kumchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti. Nenda kasome *Electro Commission* Zambia, Rais amepewa mamlaka ya kumchagua Mwenyekiti na Makamu Mweyekiti, kwa Sheria Na. 5 ya mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, nataka niwatoe hofu Watanzania wanaofuatailia mijadala ya Bunge, wajue ya kwamba kilio ambacho Watanzania walikuwa nacho, ambacho kilikuwa kinatamka kwamba Tume hii siyo huru, ukisoma katika mapendekezo haya, kwanza ukienda katika hiyo Ibara ya 74 (7), uhuru wa Tume umefafanuliwa. Ukienda katika mapendekezo ya ibara hizo, *funding* ya Tume, mambo ya mapato na mambo ya shughuli za Tume zitakuwa *funded* na *Consolidation Fund*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo inaonesha ya kwamba hata fedha zitakazokuwa zinatumika, zimewekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali *(Consolidation Fund)*. Hii ni kudhihirisha kwamba Rais Samia amedhamiria kwa dhati kuleta mabadiliko ya kweli na kuifanya Tume hii iweze kuwa chombo huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, ukienda katika hiyo hiyo Ibara ya 74 (9) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nitasoma, inasema: "Tume ya Uchaguzi yaweza

kutekeleza shughuli zake bila ya kujali kwamba kuna nafasi miongoni mwa Viti vya Wajumbe au Mjumbe mmoja hayupo, lakini kila uamuzi wa Tume ya Uchaguzi ni lazima uungwe mkono na Wajumbe walio wengi." Hii inaonesha *independence* ya Tume hii ambayo Rais Samia ameruhusu sheria ziletwe Bungeni. Kwa kweli kwa dhati tunapaswa kumsemea Rais huyu na Umma wajue upotoshaji unaofanyika nje na kwamba kilicholetwa kina maslahi mapana ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, mimi naungana na Wabunge wenzangu, jambo la unyanyapaa, sijui unyanyasaji, sitaki kuzungumzia sana kwa upande wa *gender* ya wanawake, kwa sababau linafanyika kwa *pande* pande zote. Kwa hili ninaungana na Wabunge wote kwamba lazima tuingize vipengele vitakavyotoa adhabu kwa watu wanaopenda kuchafua iwe akinamama au akinababa wakati wa uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayasema haya, wewe usingekuwa mwanamke jasiri, wewe usingekuwa kiongozi shupavu, yale tuliyokutana nayo kwenye uchaguzi wako wa Bunge la Dunia, leo hii nakwambia ungetuambia turudi Tanzania umenyanyua mikono. Ni kwa sababu ya ujasiri wako uliweza kuhimili, kumudu kashfa, matusi na kejeli ambazo zilikuwa zinafanywa na baadhi ya Watanzania wenzetu ili wewe usichaguliwe katika nafasi ya Kiti cha Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu, kwa nafasi hiyo uliyokuwa umeomba, ilikuwa ni nafasi inayokwenda kulipa heshimiwa Taifa letu. Nafasi inayokwenda kuenzi misingi ya Taifa hili lililoasisiwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Ulitukanwa sana. Kwa Ushahidi, tunazo *message* tuliziona, tuliona *voice notes* zikikukashifu, lakini ulisimama imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu sio wote wana uimara kama wako, tutunge sheria zitakazowa-*protect* wanawake pamoja na makundi yote ya walemavu na watu wengine ili tuweze kuleta heshima na ku-*harmonize political atmosphere* katika Taifa letu. Nayasema haya nikitambua kazi kubwa na

mchango mkubwa unaofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata juzi, kwa mara ya kwanza mimi kama kiongozi katika Taifa hili, nimeona Rais ameleta uhuru wa kisiasa katika nchi hii. Watu wanaandamana, wanapewa mpaka *ambulance* za kuwalinda wakiangua waweze kupewa *Panadol*. *What kind* ya uhuru ambao Rais wetu alioutengeneza? Kwa hiyo, kwa mazingira hayo, hizi *reforms* zinazofanyika lakini bado Rais wetu amekuwa *champion* wa kubeba *reconciliation* kubwa huko nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge hili tuunge mkono Miswada hii, tumpe heshima Amiri Jeshi na Rais wetu katika kuhakikisha kwamba analeta *reforms* katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spia, baada ya kusema hayo, naomba niseme ya kwamba, naunga mkono Miswada. Mengine nitachangia kwa maandishi. Kubwa nililotaka kulisema, kwa niaba ya Mataifa yote ya Afrika, tulikuwa hatujapata nafasi ya kuwashukuru; ninawashukuru sana Mataifa yote ya Afrika yaliyoonesha msimamo na umoja katika kuliunga mkono Taifa la Tanzania katika nafasi kubwa ya Kiti cha Urais wa Bunge la Dunia. Wametutia moyo Mataifa ya Afrika, Mataifa ya Asia, Mataifa ya Ulaya, Asia *Pacific* wametuunga mkono na mataifa yote duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba salamu hizi ziyafikie Mabunge yote kwa niaba yako dada yangu na kwa niaba ya Wabunge wa *IPU*. Wametupa heshima na unaendelea kuupiga mwingi dada yangu shikamoo, Mungu akubariki, uendelee kuchapa kazi na kulijenga Taifa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, ahsante sana. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo. Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika Miswada hii inayohusu

masuala ya uchaguzi na siasa. Napenda kuanza kwa kumtambua Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kama mwanademokrasia wa kwanza hapa nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu, hiki kinachofanyika leo hapa Bungeni, kujadili Miswada ya Sheria zinazohusu uchaguzi na siasa ni kuishi falsafa za *4R* za Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuko kwenye ile 'R' ya tatu ambayo inahusu mabadiliko. Hiki tunachokifanya hapa Bungeni ni mabadiliko ya sheria. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliahidi jambo hili mbele ya dunia katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa, mwezi wa Tisa mwaka 2021 kwamba Serikali yake inakwenda kufanya michakato ya kuboresha na kuimarisha sheria ambazo zitapelekea kuimarisha usawa wa kijinsia katika nyanja mbalimbali ikiwemo na siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni mtetezi namba moja wa haki za binadamu hapa nchini Tanzania. Nasema hivi kwa sababu, mwaka 1995, Mheshimiwa Rais Samia Sululu Hassan, alikuwa miongoni mwa Watanzania wachache waliokwenda kushiriki Mkutano wa Beijing ambao uliweka msingi na mwongozo kwamba, katika jambo lolote linalohusu maamuzi, lazima maamuzi yale yafanyike kwa kuzingatia jinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa tutambue ya kwamba, haki za wanawake ni haki za binadamu. Kwa hiyo, huwezi kutenganisha suala la haki za binadamu na haki za wanawake. Ni vyema tutambue, hatuwezi kuimarisha demokrasia iwapo hatutahakikisha kuna ushirikishwaji imara wa wananchi. Ushirikishwaji imara huo wa wananchi lazima uzingatie ushirikishwaji imara wa wanachama katika vyama vya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu vyombo vya siasa ndiyo uwanja wa siasa. Vyombo vya siasa kwa maana ya

vyama vya siasa, vinaweza kusababisha aidha kuimarisha demokrasia au kuififisha demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa najielekeza katika Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa. Katika Muswada huu wa Sheria, kwanza naipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuzingatia Masuala ya Jinsia na ujumuishwaji wa makundi maalumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 13 inayoongoza Kifungu *10 (c)*, Kifungu Kidogo cha (b), sheria hii imeweka takwa la kisheria kwamba kila chama cha siasa kiwe na Sera ya Jinsia na Ujumuishwaji wa Makundi Maalumu. Wote tunafahamu, vyama vya siasa vinafanya kazi kwa kuzingatia kilichomo kwenye Katiba. Kwa hiyo, kwa kuacha hivi, sera hiyo inaweza ikawa inaelea. Ni muhimu Kifungu hiki kikaboreshwa ili kuhakikisha ya kwamba Katiba za vyama vya siasa na zenyewe zifanyiwe marekebisho ili ziongezewe vifungu vinavyohusu Masuala ya Jinsia na Ujumuishwaji wa Makundi Maalumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika katika Ibara hiyo hiyo ya 13 Kifungu 10 (c), 1 (f), kinaelezea kwamba, vyama vya siasa vinatakiwa viwe na vigezo na mwongozo wa namna ambavyo vitateua wagombea wa chaguzi za ndani za chama cha siasa, kwa maana ya *intra Party*.

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea uchaguzi, tuna chaguzi za aina mbili; tuna uchaguzi ndani ya vyama vya siasa na tuna uchaguzi baina ya vyama vya siasa, kwa maana ya uchaguzi wa kutafuta dola. Hii ni *Intra Party*. Sheria hii katika Kifungu hicho imeongelea tu kuzingatia vigezo vya kutafuta wagombea katika chaguzi za ndani ya chama cha siasa. Kwa hiyo, lazima katika Kifungu hiki tuongeze takwa ambalo litavitaka pia vyama vya siasa kuweka sheria hizi na miongozo na kanuni zake katika chaguzi baina ya vyama vya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa pia ni lazima vyama vya siasa viwe vimejiwekea mwongozo na utaratibu, vitafanya vipi teuzi zake kwa kuzingatia jinsia ili tuweze kufikia 50% kwa 50%?

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu ninukuu katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, Kifungu 231 (j) kinasema kwamba, "Chama Cha Mapinduzi kitabuni na kutekeleza mikakati inayoongoza ushiriki wa wanawake katika maamuzi ya uongozi, kwenye nyanja za kisiasa na kiuchumi, hadi kufikia 50% kwa 50%". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huu wa ahadi iliyopo kwenye ilani ya Chama Cha Mapinduzi na kwa rejea mbalimbali ambazo amezifanya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika eneo hili ni zahiri kabisa endapo tutaacha kifungu hichi namna kilivyo, inamaana hatutimizi dhamira ya dhati ya kuimarisha demokrasia. Kwa sababu hatutakuwa na miongozo ya kufikia hamsini kwa hamsini.

Mheshimiwa Spika, niendelee, naipongeza sana Serikali kwa kutambua umahususi wa makosa ya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia katika vyama vya siasa hadi kupelekea kuanzishwa kwa dawati la vyama vya siasa. Dawati la jinsia katika vyama vya siasa, lakini kwa jinsi ilivyowekwa na ikiachwa hivyo inamaana madawati haya yatakuwa yameachiwa vyama vya siasa yenyewe yafanye kazi kwa hiari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napendekeza, madawati haya ya jinsia katiaka vyama vya siasa lazima yaunganishwe na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ili aweze kuripoti katika Baraza la Vyama vya Siasa. Kwa sababu Baraza la Vyama vya Siasa lina jukumu la kuangalia mienendo inayofanyika katika vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo itaimarisha madawati haya ya kijinsia, kwa kufanya hivyo itawezesha Baraza la Vyama vya Siasa kupokea taarifa kutoka kwenye vyama vya siasa na kufuatilia utekelezaji wa malalamiko yanayowasilishwa katika madawati ya jinsia kuhusiana na uzalilishaji na ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imetambua umahususi wa kosa la ukatili wa kijinsia katika siasa, hadi kusababisha kuanzishwa kwa dawati la jinsia katika vyama vya siasa.

Inashangaza na kusikitisha kwamba nimepitia sheria nzima hii, Muswada wa Sheria wa Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani hakuna mahali popote ambapo Muswada huu umezingatia vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia kama kosa la uchanguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili hali Serikali hii hii imetambua kosa hili hadi ikasababisha kuanzisha dawati la jinsia katika Muswada wa Sheria wa Vyama vya Siasa. Kwa hiyo, ninachotaka kusisitiza kwanza nakubaliana kabisa na kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Joseph Mhagama kwa kuhakikisha ya kwamba katika mapendekezo yao ya marekebisho wametambua kwamba hii kuacha eneo hili ni kutoitendea haki demokrasia na *4R* ambazo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, anazipigania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitarejea hivi karibuni Mheshimiwa Mwenyekiti wa UWT Taifa, mama Mary Chatanda. Pamoja na Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, mama Zainabu Shomari, wamefanya ziara katika mikoa 17, wilaya 85, kata 845. Kila mahali wanapokwenda wanahamasisha wanawake wajitokeze kugombea katika uchaguzi wa Serikali za mitaa na katika uchaguzi mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 90 ya wanawake wanawaambia viongozi wetu wa UWT, sisi tupo tayari kugombea lakini nani atatulinda dhidi ya vitendo hivi vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia? Wanahoji viongozi wetu wa UWT, nani atatuhakikishia tutapata haki, nani atatuhakikishia fedhea, matusi na kuvuliwa nguo hakutatokea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jawabu pekee ni kuhakikisha katika sheria hii ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, vitendo vya ukatili wa kijinsia wakati wa uchaguzi vinatambulika kama kosa la uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kutambuwa hili kama kosa la uchaguzi. Kwa sababu pale ambapo awe ni mwanaume au mwanamke katendewa vitendo hivi, ikiwa ni kipindi cha uchaguzi hawezi kupata haki yake. Pale unapomchelewesha mtu kupata haki yake ni kwamba umemkosesha haki ya msingi ambayo ipo kwenye Katiba yetu, ni haki ya kuchaguliwa na haki ya kuchaguwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasisitiza ni lazima kama wabunge, tuhakikishe tunazipigania *4R* za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ikiwemo kuimarisha mazingira ya demokrasia na kama hatutatambua kosa la unyanyasaji na ukatili wa kijinsia katika chaguzi kama kosa la uchaguzi tutakuwa hatujatenda haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nielekee kwenye eneo la Tume ya Uchaguzi *(NEC)* lakini katika sheria hii hii ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Mwezi wa 11 mwaka jana, Jumuiya ya Tume za Uchaguzi Afrika, ambapo Tume yetu ya Uchaguzi Tanzania ni mjumbe. Wamepitisha mwongozo wa matumizi ya mitandao ya kijamii katika uchaguzi. Nakala ninayo hii hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwa namna ambavyo unatuimarisha, nilipata mualiko nikashiriki jinsi walivyokuwa wanaandaa mwongozo huu. mwongozo huu umepitishwa Novemba 2023, moja ya maeneo ambayo mwongozo huu umeelezea ni kwamba, mwongozo utakapopitishwa na umepitishwa Novemba, 2023 na jumuiya hii. Lazima *NEC* kwa maana ya tume zote za uchaguzi Afrika ziuhishe masuala ya matumizi ya mitandao kwenye sheria zao za uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, sisi ndiyo tupo katika fursa hii tunarekebisha sheria yetu. tukiendelea kutogusia eneo hili yatatokea madhara makubwa. Kwa haraka haraka natoa mifano miwili, mwezi wa 10 mwaka jana ilizunguka *clip* ikimuonyesha Rais wa Zambia akitangaza kwamba hatagombea tena uchaguzi 2026. Baada ya siku chache Ikulu ya Zambia ikatoa tamko kwamba *video* hiyo ni *fake* imetengenezwa kwa akili mnemba *(artificial intelligence)*.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu mwezi wa kwanza, sasa hivi kule New Hampshire kulikuwa kuna uchaguzi. Imezunguka sauti ya Rais Biden, Rais wa Marekani akiwaambia wanachama wa chama chake cha *Democratic* wasiende kupiga kura sasa hivi wasubiri kupiga kura Novemba jambo ambalo limetumika kwa kutumia *artificial intelligence*.

Mheshimiwa Spika, sasa ni lazima katika Sheria hiyo ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani tutambue pia na tuongeze ibara itakayotambua vitendo vya kutumia teknolojia, digiti na mitandao ya kijamii ikiwemo akili mnemba *(artificial intelligence)* kwa lengo la kupotosha, kuchafua, kufedhehesha na kuharibu michakato ya uchaguzi kama kosa la uchaguzi, tusipofanya hivyo tutakuja kupata madhara makubwa sana na isitoshe hili tayari ni jambo ambalo Jumuiya ya Tume za Uchaguzi Afrika limeshapitisha na mwongozo wake ulipita mwaka jana mwezi Novemba, 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe mwenyewe kama Spika wetu na kama mlezi wetu kwa namna ambavyo umeendelea kutuongoza na kutuimarisha na namna ambavyo umeendelea kuunga mkono jitihada zetu mbalimbali. Jitihada za kuchambua hii Miswada, tulianza toka Aprili, 2022 na mkutano wetu wa kwanza wa Wabunge wanawake kujadili masuala ya wanawake katika siasa wewe mwenyewe ndiyo ulikuwa mgeni rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakushukuru sana kwa namna ambavyo unaendelea kutuimarisha na kutupa ujasiri wa kuendelea kupambania hoja za msingi ambazo zitapelekea kufikia hamsini kwa hamsini ambayo hata Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akiirejea mara nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha kwa kumnukuu Mwenyekiti wetu wa UWT Taifa, Mama Mary Pius Chatanda, amesema katika moja ya mikutano yake kwamba wakati wa Mungu kwa wanawake ni sasa, kwa sababu tunaye Mheshimiwa Rais, mwanamke, tunaye Spika mwanamke, tunaye Katibu wa Bunge mwanamke, tunaye Waziri anayesimamia dhamana ya

Miswada hii mwanamke na tunaye Waziri wa Katiba na Sheria mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunawaahidi hatutawaangusha, tupo tayari kuendelea kupambania ajenda hii na niwashukuru sana Wabunge wote wanaume wanaoendelea kutuunga mkono. Kwa sababu ajenda ya mwanamke haiwezi kufanikiwa bila kuungwa mkono na wanaume, kwa maana ya *he for she*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kusisitiza tunaiomba sana Serikali ichukue maoni yetu…

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kumpa taarifa Mbunge makini Mheshimiwa Neema kwamba vitendo hivi vya udhalilishaji wa kijinsia havibagui. Miaka ya 2000 aliyekuwa Spika wa Bunge hili, Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, alikuwa anagombea kutetea kiti chake cha Ubunge katika jimbo lake, mmoja wa wagombea wa vyama vya upinzani, alichukua picha moja ya Mama Anne Makinda aliyokuwa amepiga wakicheza muziki na Waziri wa rika lake na miziki ile wakati ule ni ya *blues,* mtu unamshika mwezako mabega, lakini akaichukua ile na kuitafsiri kwa namna hasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri Wabena wale hawakusikia vitimbi hivyo wakamchagua Mheshimiwa Anne Semamba Makinda kuwa Mbunge wao mpaka alipoamua kustaafu mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo vitendo hivi havina ubaguzi wa kuiangalia nafasi yako ni vizuri Bunge hili liungane na waliyopendekeza kwenye sheria iingizwe ni vifungu ambavyo

vitawabana watu ambao wanazalilisha wengine, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hii kwa mikono miwili na unyenyekevu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kusema kwamba tuendelee kuhakikisha tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais katika *4R* na *4R* ni pamoja na kuhakikisha tunaimarisha demokrasia na kuweka mazingira ambayo yatawezesha jinsia zote mbili kwa maana ya mwanaume na mwanamke kushiriki katika chaguzi kwa njia mbili; kuchaguliwa au kuchagua.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana na naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mheshimiwa Omar Ali Omar, ajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya mimi kuchangia miswada hii mitatu ambayo ipo mbele yetu. Mimi nitachangia kwa ujumla wake bila kuchambua mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa niaba ya Serikali nzima kwa kuona wakati muafaka umefika sasa ili tuweze kufanya mabadiliko haya makubwa na muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu. Niwapongeze hasa Mwenyekiti wa Kamati ile ya Utawala, Katiba na Sheria pamoja na Kamati nzima kwa mapendekezo yao, maoni na uchambuzi waliofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze wadau wote ambao walikuja na walitoa maoni yao na niwaambie wale wenzetu katika majadiliano yoyote au mashauriano lazima ukubali

kupokea na kutoa. Nilikuwa nasikiliza takwimu jana kwamba katika mapendekezo 83, mapendekezo 61 yamepitishwa, halafu watu wanaandamana, nafikiri bado wanahitaji kupata elimu zaidi ya namna ya kuridhiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuridhiana siyo kukubaliwa kila kitu, ni kukubaliwa kiasi na wewe ukubaliane na yale ambayo wenzako wameona siyo muhimu kwa wakati huo. Nimpongeze Mheshimiwa Rais ambaye ndiyo chanzo kabisa cha mabadiliko haya. Niseme tu ni mabadiliko muhimu kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema nitakwenda kwa ujumla na nianze na kipengele cha kupita bila kupingwa. Nipongeze kazi yote iliyofanyika kuanzia Mahakama iliyotoa *judgement* ile ambayo imepelekea sheria hii ije, Serikali namna walivyoliweka pamoja na Kamati.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye *practicability;* wakati wa uchaguzi ninajua bado vyama vingi hivi ambavyo vinapambana na chama chetu havina uwakilishi maeneo yote na haviwezi kuwa nayo kwa haraka ni hatua. Sasa eneo ambalo wao hawana mgombea, busara imetumika kwamba ifanyike ile kura ya ndiyo au hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najaribu kujiuliza sasa mawakala wa upande wa pili watakuwa ni wa nani? Kwa sababu hivyo vyama havina uwakilishi, maana yake mawakala watakuwa wa hicho chama ambacho ndiyo kina mgombea. Sasa utaona tu kwamba *practicability* ni tofauti. Maana yake meza ndiyo itaamua au itakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuonesha tu kwamba ni mawazo mazuri, lakini *practicability* yake inaweza ikawa na shida. Ninaweza ku-*predict* kabisa kwamba maeneo ambayo mgombea ni mmoja siyo rahisi watu wajitokeze wale ambao wanakuja kupiga kura ya kupinga. *Automatically* wanaona kwamba ameshashindwa, kwa hiyo, ionekane ni namna gani itafanya kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maoni ya Kamati kwenye ukurasa ule wa 12 kipengele 2.2.4. wameweka yale mambo muhimu waliyoyaona na niyataje mawili kwa umuhimu wao. Suala la wakala, wameelezea kama mambo muhimu wanayoyaangalia. Sasa nitumie uzoefu wangu wa uchaguzi, kwenye uchaguzi uliopita ni vizuri tume iwe na uwezo wa kuhakikisha na ikiwezekana kusimamia mawakala waweze kulipwa haki zao.

Mheshimiwa Spika, vipo vyama kwenye uchaguzi uliopita hasa kwenye Jimbo la Moshi Mjini, mawakala walichukuliwa wakaahidiwa kulipwa, walipokuwa wameshindwa mawakala mpaka leo hawajalipwa na wamenifuata wanalia. Sasa ni vizuri hilo lichukuliwe na tume kwamba hawa mawakala, haki zao wanazostahili uchaguzi umeisha, umeshinda au umeshindwa mawakala haki zao wanaweza kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye eneo hilo hilo ukurasa wa 12 wa maoni ya Kamati kwenye yale mambo ya muhimu; zile sifa za uteuzi wa viti maalum, wamesema tume itashirikiana na chama kuziweka sawa, nafikiri ilitakiwa tuwe na *standard at least* ya kuanzia ambayo itakuwa ipo pale kwamba viti maalum baada ya uchaguzi wanapatikanaje, kuwe na *standard procedure* na sifa ili tuondoe mambo ya *nepotism* pale, mambo ya watu kuweka watu wanaowataka kwamba zile sifa ziwepo labda ya kwanza ni elimu, ya pili sijui uzoefu, sijui na nini ziendee na ushiriki na nini ili kuweza kuwapata viti maalum, isiachwe tu kwamba mwisho tutashauriana na tume. Nadhani hilo ni suala la muhimu sana la kuweza kuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili suala la uwakilishi wa *gender,* nadhani ni suala muhimu sana kwa karne ya leo. Kwa sisi nchi ya Tanzania tuna bahati kwa kipindi hiki tunaona uongozi wako, tunauona uongozi wa Mheshimiwa Rais na tunaona namna ambavyo unatija siyo kwamba ile mingine haikuwa na tija, lakini hii tumepata tija zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kwenye miradi mimi sina hata cha kuficha miradi ni mingi zaidi kuliko kipindi kingine chochote. Ni vizuri kwa sababu dunia ilianza kwa mfumo dume. Tuendelee

kuongeza *confidence* hasa kwa *gender* Ke. Mfano mdogo, ukifanya *research* duniani madereva wazuri wa magari ambao hawana ajali sana ni wanawake. Ukifanya *research* ya ma-*accountant* au watunza fedha wazuri ambao siyo wezi sana utakuta ni wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye *google* ukatafuta nchi zenye furaha zaidi halafu upande wa pili ukachukua nchi ambazo zina uwakilishi mkubwa zaidi wa wanawake katika *system* yao ya uongozi utaona zile zenye furaha zaidi kwa haraka haraka zile zenye furaha zaidi zile zenye uwakilishi wa wanawake zaidi zipo kwenye *top ten* na ndiyo nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na kwamba kwenye Katiba bado tupo kwenye *one third* na kwa sababu tunaamini tumeshaanza na mchakato wa Katiba ni vizuri twende kwenye *standard* ya 50/50 huko mbele itakuwa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa ambao wameaminiwa wameshaonesha uwezo mkubwa sana ambao hatuna sababu ya kurudi nyuma. Naona hilo ni eneo la muhimu sana la kuwekea mkazo.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye ukatili wa kijinsia na nadhani hili ni eneo la muhimu sana. Niwapongeze sana Kamati wamesema pale kwenye ile Ibara ya 134 kiongezwe kifungu cha 135. Niseme huu unyanyasaji wa kijinsia ni pande zote na hata wazungumzaji jana waliongelea habari za ushoga, watu wanasingiziwa, lakini hata kama tu umetoka kwenye ndoa moja unaenda kwenye nyingine unaonekana unatatizo.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa *experience* uchaguzi wa mwaka 2015 Moshi Mjini tulikuwa tuna mgombea mmoja wa Udiwani wa *gender* Ke, alifanyiwa udhalilishaji mkubwa sana na alikuwa mtu mzima na ana familia. Watu walichukua nguo ya ndani ya mfano, kwa sababu na yeye alikuwa na umbo kubwa wakaitundika kwenye mti wanaonesha kwamba ni nguo yake, alichukuliwa jana, wakapaka huko na vitu vya ajabu, kwa hiyo, utaona ni jinsi gani yanafanyika mambo ya kikatili ambayo hata

kwenye maisha ya familia ile yanaenda kuwa ni doa moja kwa moja. Kwa hiyo, nadhani hii sheria sidhani kama tunahitaji kujadili sana. Serikali niwaombe, Sheria ya Unyanyasaji wa Kijinsia iingie moja kwa moja kwa sababu ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasema hivyo kwa sababu ndiyo imesababisha uwakilishi wa Ke umekuwa mdogo, uthubutu wa Ke kwenda kuchukua fomu kushiriki umekuwa mdogo kwa sababu unyanyasaji ni mkubwa zaidi kwao.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka tuliangalie kabisa kwamba hili liwe lina kipengele maalum, isisubiri kuja kuchukuliwa hatua kule mwisho baada ya uchaguzi, kwa sababu mtu anakuwa ameshakuwa *damaged* hata kama wakati kampeni zinaendelea hilo suala likijitokeza kuwe na *provision* ya kulishughulikia na ku-*disqualify* watu pale pale.

Mheshimiwa Spika, nimeona zimeandikwa faini pale sijui shilingi milioni mbili na sijui kifungo cha miezi 18 bado hata hizo hatua ni ndogo sana ilitakiwa kinyimwe hicho chama kuendelea na kampeni na kukitoa kwenye uchaguzi. Nadhani hilo lingekuwa ni jambo la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye ile Ibara ya 13 ya Sheria ya Vyama vya Siasa yapo maeneo mawili muhimu sana; hilo moja nimeshaliongelea kwenye kile kipengele cha 10C waliongelea ile *gender and social representation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo suala la *ideology;* unajua kuna vyama mpaka vinaenda kwenye uchaguzi havijui *ideology* yake ni nini. Ndiyo maana sasa vinafika kwenye uchaguzi badala ya kusema *ideology,* wanaangalia kupambana na *character* ya mtu, wanafanya *character assassination* kwa sababu *ideology* yao hata wao wenyewe hawaijui.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tuelezee kwamba katika mikutano ya kampeni chama ni kwa kiasi gani kielezee *ideology* yake badala ya kupambana na kutukana watu na kutafuta tu mapungufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri hili ni eneo lingine ambalo pamoja na kwamba lipo kwenye sheria ya vyama vya siasa, ije pia iletwe kwenye kampeni ili iweze kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nadhani kwa leo inatosha ni mchango wangu naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, atafuatiwa Mheshimiwa Omar Ali Omar, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, ajiandae.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, pia, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia miswada hii mitatu ambayo ni muhimu sana na imebeba mustakabali wa Taifa letu katika namna mbalimbali. Ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ni kwa mapenzi yake leo hii kama Bunge tumefika hapa kwa ajili ya kujadili miswada hii ambayo imepita katika michakato mbalimbali. Nikushukuru wewe kama Mheshimiwa Spika wetu; na nimshukuru kipekee kabisa Mheshimiwa Rais, wetu Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye hiki ambacho tunakijadali leo kinaakisi dhamira yake ya dhati ya kuleta Taifa letu pamoja kama jamii moja, kama familia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siasa ni utamaduni, siasa ni namna ya watu wanavyohusiana katika maisha ya kawaida. Ukitaka kuona jamii ambayo imestaarabika angalia jinsi gani watu wanavyoheshimiana, watu wanavyoshauriana na wanavyokosoana. Yote hayo wanayafanya katika nia njema ya kujenga. Ndiyo maana sisi kwa Waafrika, Kiafrika tunaamini kabisa jamii zetu za Kiafrika zilikuwa na demokrasia, ndiyo maana tulikuwa tunafundishwa namna bora ya kukaa na kusikiliza mawaidha ya wazazi, rika lakini pia ushauri kwa namna tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa kuliko yote, tulifundishwa heshima na adabu kwa wote ambao wametuzidi umri. Hayo tulikuwa

tumefundishwa kitamaduni lakini tumefundisha pia Makanisani na Misikitini. Ndiyo maana moja ya amri kuu ambazo tunaweza kuziona kwenye Biblia, Waefeso 6:2-3 tunaambiwa, waheshimu baba na mama yako ili upate miaka mingi na heri nuniani. Ni amri pekee ambayo imebeba ahadi, kumuheshimu baba na mama. Ahadi yake utapata fanaka na kuishi miaka mingi hapa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, demokrasia yetu imekuwa ni kichaka cha baadhi ya watu kwenda kinyume na maadili ya utamaduni wa Kiafrika ambayo inasisitiza amani kama mhimili wa tamaduni zetu katika jamii zetu. Watu wamefikia hatua hata kusema uongo wa kusema kwamba hiyo ni siasa, kukashifu hiyo ni siasa na vitu vingine. Hali hiyo imetufikisha mahali ambapo mambo ya ajabu yalikuwa yanaonekana ni kawaida. Kwa hiyo, ninaamni kabisa ujio wa Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa wakati huu Mungu analitakia mema sana Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zile *4Rs* ambazo Mheshimiwa Rais, amezitengeneza ama amezitohoa kama mihimili yake ninaamini kabisa anaturudisha kwenye Uafrika wetu kwamba turudi kwenye kuridhiana, turudi kwenye kustahimiliana na tukubali kubadilika. Lakini kubwa ni kwamba, hata ile imani ya wana CCM inasema kwamba kukosoa na kukosolewa ndiyo njia ya kujenga Taifa letu. Kwa hiyo, kujijenga upya ni moja ya *pillar* ambazo Mheshimiwa Rais, wetu anaamini kabisa kwamba  zinaenda kujenga Taifa letu upya, na sisi kama Bunge tunapaswa kuunga mkono kwa dhati kabisa dhamira njema ya Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, na ndiyo maana tunaona katika miswada hii mitatu ambayo ni zao la hizi *4Rs.* Ni zao la mawazo mtambuka kutoka kwa wadau mbalimbali. Kwanza vyama vya siasa, kikosi kazi ambacho kilifanya kazi kwa miezi tisa ambacho kilikuja na mapendekezo 83, 64 kati ya hayo Serikali imeyafanyia kazi, 12 kwenye *process* na saba yanahitaji mjadala mpana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona kabisa mapendekezo ya wadau mbalimbali ya kutaka kuboresha mazingira ya kisiasa na

tathmini ya Kidemokrasia. Tunaona kwamba wadau waliomba Serikali, kwamba Serikali ilete Muswada wa Sheria za Uchaguzi na Sheria hizo zisije kwa hati ya dharura. Haya yote Serikali imeridhia, na haya yote yanaonesha nia njema ya Mheshimiwa Rais wetu kutaka kujenga jamii mpya, ya Watanzania wapya ambao wanaheshimiana, wanastamiliana ambao wapo tayari kujenga Taifa lao katika hali ya maridhiano. Sisi kama Bunge jukumu letu ni kuunga mkono jitihada hizi za Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna masuala ambayo yamezungumzwa; na mimi natokea Morogoro mama yangu ni Mluguru mchanganyiko wa Kivudunda. Kule tunasema mjomba ni mama, na hiyo inaonesha nguvu ya mwanamke katika jamii ya Kiluguru. Mama ana nguvu, mama ana heshima ya kipekee.

Mheshimiwa Spika, na Mwenyezi Mungu alinijalia nikaenda kupata elimu nakuishi katika nchi za Scandinavia, kule Finland kwa miaka zaidi ya 17. Kule haya ambayo tunazungumza kuhusiana na suala la ushiriki wa wanawake katika siasa si jambo ambalo wanalizungumza, kwa sababu tayari lilishafanyiwa kazi tangu Mwaka 1934. Wakati nchi ile inaingia vitani na Urusi wanawake wote walikuwa na kazi ya kuzalisha chakula, mavazi, silaha na kuendesha nchi wakati wanaume wakiwa vitani. Hata wanaume walioprudi walikuta kwamba wanawake wanaendesha nchi vizuri kabisa. Ndio maana leo hii tunasema Finland ndio nchi ya kwanza wananchi wakiwa na furaha kuliko wote Duniani. Siingii katika mjadala wa *definition* ya maana ya furaha. Ukiangalia jamii ambayo imesimama kiuchumi, kifamilia na vitu vingine unaona kabisa hawa wapo vizuri kwa sababu ya uongozi wa wanawake katika jamii ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijamtendea haki marehemu mama yangu na wanawake wote kama nisipojikita mchango wangu katika suala zima la *gender,* ama jinsia. Ibara ya 13 ambayo wenzangu wamezungumza imetoa sharti kwa vyama vyetu kuona namna bora ya kuzingatia sera ya kijinsia ndani ya vyama; na hili mimi pia ninaliunga mkono. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge, si kwamba tunapolizungumzia suala hili hatuzungumzii kwa sababu tunawapenda sana mama zetu na

dada zetu; hatulizungumzii hili, kwa sababu tunawapa hisani tunafanya hili kwa ajili ya hatma ya watoto wetu hasa wa kiume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi, ninaomba nitoe mfano, mimi nimegombea Mikumi, mama yangu anatokea hapo, nimezaliwa hapo, nimekulia hapo na wazazi wangu wamefanya makubwa sana hapo. Nilipoanza kugombea nikaambiwa huyu ni mama yake tu, anatoka hapa. Hilo lilijengwa kama ajenda ya kisiasa ndani ya uchaguzi, ndani ya chama changu na nje ya chama change. Kuna kosa gani kuwa na mzazi wanamke ambaye anatoka kwenye asili ya hapo? Hakuna. Lakini mimi kama mtoto wa kiume niliathiriwa kwa sababu mama yangu anatokea hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili tunalifanya kwa nia njema kwa ajili ya kulinda watoto wetu wa kike na wa kiume ili wahukumiwe kwa matendo yao na si kwa jinsia ya wazazi wao ama jinsia zao wenyewe. Katika hili katika sehemu pili ya Muswada inayoainisha makosa ya uchaguzi, mimi ninaomba kiongezwe kifungu kingine ambacho kitaja kosa la ukatili wa kijinsia kuwa kosa la uchaguzi. Hili likifanyika ni muhimu kuwa kosa mahususi katika chaguzi zetu, kwa sababu linaweza kabisa kubainisha vitendo ambavyo vitatafsiriwa kuwa ni ukatili wa kijinsia katika kipindi cha uchaguzi na kuweka adhabu ambazo zitalingana na uzito wa kosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mtu ambaye anatumia jinsia ya mtu kwenye uchaguzi maana yake ana nia moja tu ya kumfedhehesha, kumdhalilisha na kumpunguzia kura, kumuondolea uhalali kwenye macho ya wapiga kura. Adhabu yake inapaswa apatiwe pale pale na adhabu ioneshwe kabisa katika sheria zetu. Hili litakomesha vitendo vya udhalilishaji. Kwa wale ambao ni mbilikimo wa kufikiri na pimbi wa mawazo kutumia *gender* ya mtu kama kigezo cha kumpunguzia kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ilani yetu inasisitiza kuongeza idadi ya wanawake kushiriki katika kupiga kura. Kama Sheria hii isipo kuwa inaeleza kinagaubaga makosa ya ukatili wa kinjisia nina wasiwasi

kwamba yale malengo ambayo tunasema kwamba tunaenda kuongeza uwakilishi wa wanawake katika siasa zetu hatutafikia kwa sababu wengi ambao wana uwezo wanogopa kuingia kwa sababu ya hawa ambao hawana hoja watatumia jinsia yao kama kigezo cha kuwaondolea uhalali kwenye macho ya wapiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ingawa siyo kwa umuhimu; mimi sijawahi kuwa na kiongozi ambaye *boss* wangu ambaye ni mwanaume. Miaka yangu tangu nimemaliza shule ma-*boss* wangu wote ni wanawake na kimsingi wamenisaidia sana kufika hapa nilipo. Hata wewe ambaye umekaa hapo kwenye kiti kwa namna moja ama nyingine hata uwezo wangu umeongezeka kwa sababu ya *confidence* ambayo unatupa sisi Wabunge. Kwa hiyo, inadhihirisha nguvu ya mwanamke, sawa mwanamke katulea, kutusimamia na kuongoza. Kwa niaba ya Mikumi ninaunga mkono hoja ili tuunge mkono *4Rs* za Mheshimiwa Rais, wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Ali Omar, atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, ajiandae.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa kuchangia katika Miswada yetu hii adhimu katika Bunge letu hili tukufu.

Mheshimiwa Spika, mimi ninataka nianze kwa kusema kwamba Tanzania wengi wetu tuna dini zetu, na katika dini zetu tunaongozwa na misingi mitatu mikubwa. Msingi wa kwanza ni uadilifu, msingi wa pili ni uaminifu na msingi wetu wa tatu ni ukweli wa dhati. Tukiogelea katika maeneo hayo, basi ni imani yetu kwamba Tanzania itaendelea kudumu na amani na utulivu na wananchi wetu wataishi katika maisha ya raha na furaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini niyaseme haya? Ninayasema haya kwa sababu Miswada hii imeletwa katika muda muafaka muda ambao karibu tutainga katika michakato ya uchaguzi. Chaguzi za Serikali za Mitaa. Pia, ukichuguliwa na Uchaguzi Mkuu wa Tanzania wa Rais, Wabunge pamoja na viongozi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba sheria zetu zinalenga sana kuangalia haya mambo ambayo nimezungumzia mwanzo. Hasa katika kipindi cha uchaguzi ni kipindi ambacho kina kuwa ni kigumu sana kwa Tanzania. Ni kipindi ambacho tunapitiwa na majaribio makubwa kabisa katika Tanzania. Kwa hiyo, lazima tuangalie sana wakati tunapotunga sheria zetu kuwazia wale ambao wana dhamira ya kuhakikisha kwamba Tanzania inaendelea kuingia kwenye machafuko katika pindi hasa cha uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nijielekeze katika kuangalia zaidi kwenye Tume Huru. Kama tunavyozungumza, Miswada hii imezungumza sana kuhusu Tume Huru. Kwanza, ninaipongeza sana Serikali kwa kuufanyia marehkebisho Muswada huu na kuona kwamba kuna haja sasa Tanzania kuwa Tume Huru ya Uchaguzi. Lazima tuangalie, sheria siyo ukuta. Kuna watu kwa dhamira yao ya makusudi wanapanga makusudi kuvunja sheria ua kupindisha sheria. Wanapopindisha sheria matokeo yake yakuwa ni mabaya zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapokuwa na Tume Huru lazima iwe Tume Huru kweli. Tume hii lazima tuiwezeshe kuweza kufanya kazi bila ya kuingiliwa na chombo chochote kile cha Serikali, kwa sababu tutakapoiwezesha Tume hii basi ni imani yangu kwamba Tanzania tutaweza kuendelea zaidi. Kwa mfano, Tume Huru kama ikiwa utainyima fedha tayari ile itakuwa siyo Tume Huru. Kwa hiyo, Serikali inangalie sana wakati tunapoiunda Tume hii Huru. Basi iwe ni Tume Huru kweli ambayo haingiliwi na chombo chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nizungumze suala zima ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumza, suala la udhalilishaji wa kijinsia. Kwa kweli hili ni suala tete sana, nitatoa

mfano, katika kipindi ambacho kina kuwa cha Uchaguzi ukiangalia hasa kule Pemba ninakotoka kwenye majimbo yetu. Katika kipindi cha uchaguzi wanawake wanadhalilika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyozungumza kuna wanawake wana watoto walemavu wanawatunza, hivi tunavyozungumza kuna watoto yatima wanawatunza, hivi tunavyozungumza wanawake wanahangaika kutafuta chakula cha watoto wao, kwa sababu ya uchaguzi. Kwa hiyo, kipindi cha uchaguzi wanawake wengi wanapoteza nafasi zao, wanapoteza waume zao, watoto wanakuwa yatima.

Mheshimiwa Spika, hii nikuonesha kwamba suala zima la unyanyasaji wa kijinsia lina kwenda katika nyanja nyingi. Haliendi kudhalilisha wanawake wanaogombea tu lakini linakwenda mpaka kwa wanawake ambao wanaishi katika nyumba zetu, na ndio hao Wapiga Kura wetu wanaotusadia katika kuhakikisha kwamba wanapata viongozi. Hii ni kuoneshwa kwamba suala hili kuna haja Serikali izingatie kuweka kifungu maalum kitakachoweka mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba matukio katika kipindi cha uchaguzi hasa katika jinsia ya wanawake wanabaki wakiwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nizungumze kuhusu suala zima la upatikanaji wa maafisa waandamizi wa Tume. Kwa kweli hata mkurugenzi ni mwandamizi wa Serikali. Anaweza kuwa mkurugenzi yule yule akabadilika akabadilisha mazingira ambayo hayatakuwa salama na hayatakuwa rafiki katika Uchaguzi. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe kwamba tunapowapata hao maafisa waandamizi tunawapata kwa utaratibu utakaowezesha kuwa wazi kabisa. Kwa kupitia vyama vyote na bila ya kuwa na ubaguzi, kwa sababu ubaguzi ukianza hapa ndio vurungu zinaanza kuendelea katika uchaguzi wetu. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe maafisa hawa waandamizi wanafanya kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu ambazo tumezipanga katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote ninaomba sasa tujielekeze sana katika Muswada huu kufauta sheria zaidi, kwa sababu kuandika Sheria siyo tatizo. Tanzania ina sheria nyingi nzuri na ina sheria ambazo kwa nchi nyingine wanaziiga sheria hizi na wanazifuata Sheria hizi hizi tunazozitunga Tanzania. Jinsi ya Serikali kuzisimamia kuhakikisha kwamba mwenye haki anapata haki yake na asiyekuwa na haki anakoseshwa haki ambayo siyo ya kwake. Hapa tutaweza kufika pahala pazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Miswada hii kwa kweli itatibu vile vidonda na majeraha ambayo tunayapata hasa katika kipindi cha uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, atafuatiwa Mheshimiwa Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa nafasi ya kuchangia katika mada iliyopo mbele yetu ambayo ni Miswada mitatu. Kwanza kabisa nishukuru Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuona ni muda muafaka kuleta Miswada hiyo naikaweza kujadiliwa katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu, chini ya dada yetu na Jemedari wetu Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu. Pia, Naibu Waziri dada yetu Ummy Nderiananga, Katibu Mkuu pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, mchakato huu mimi kama Mjumbe wa Kamati na Makamu Mwenyekiti, umekuwa ni mchakato ambao kwa kweli ni wa kipekee. Tangu tunaanza kupitia Miswada hatujawahi kupokea Miswada ya namna hii ambayo ina mwitikio mkubwa wa kijamii.

Mheshimiwa Spika, pia tunakushukuru wewe, ofisi yako ilijikita vizuri katika kutoa matangazo na kuweka mazingira mazuri ambayo yalifanya tukapata wadau mbalimbali kwa ajili ya kutoa maoni.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuja na falsafa ya *4R* ambayo inatupeleka nchi katika maridhiano, usitahimilivu, mabadiliko na kujange nchi upya. Tunaona mkakati huu wa *4R* unalenga sana kuimarisha utawala bora ndani ya nchi yetu, kuimarisha demokrasia na uchumi pia kufungua milango ya mazungumzo na vyama vya siasa, asasi za kiraia na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia miswada hii, maboresho yake yote ambayo yamefanyika yanaleta mageuzi makubwa ya kisheria na kimfumo. Tunaona ambavyo italeta uhuru katika uchaguzi, imeongeza ushiriki wa wanawake vijana na watu wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, katika utangulizi wangu huu, tunaona miswada hii inaenda kufanya chaguzi ziwe ni chaguzi ambazo ni jumuishi zaidi, chaguzi za uwazi zaidi, chaguzi za haki zaidi na usawa zaidi. Kwa nafasi ya pekee najikita katika muswada mmoja mmoja,Muswada wa kwanza ni Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Nitaongelea tu Ibara ya tano ambayo inaelezea muundo na uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Tume.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mabadiliko ambayo yamekuja katika muswada huu na majadiliano ya Kamati lakini pia makubaliano yetu na Serikali kwa kweli yanaweka mustakabali mzuri wa nchi hii. Tunaona katika Ibara ya 74 Kifungu Kidogo cha Kwanza, ambapo imempa mamlaka Mheshimiwa Rais kuteua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume kwa kuwa na uwiano wa kimuungano. Tunaona mapendekezo yanakuja na mustakabali mzuri, kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuteua kwake kuwepo na chombo au mamlaka fulani ambayo inampendekezea hao watu wa kuwateua. Nao tunaona Serikali inakuja kwa kuungana nasi kwa kumtumia Jaji Mkuu wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania baada ya kushauriana na Jaji Mkuu wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika utawala wa kawaida na sisi wenyewe kama Wabunge katika Majimbo yetu au katika maeneo yote tunayoyatawala, inakuwa ni sehemu ambazo ni nadra sana kiongozi akasema baadhi ya mamlaka yangu watu wanisaidie halafu waniletee mimi nithibitishe. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais. Hii ni kwamba, Mheshimiwa Rais wetu kila alichokitambua na kukiishi cha maridhiano, ustahimilivu, mabadiliko na kujenga nchi upya anakiishi kwa matendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo tunaona Kamati ya Usaili ambayo inaundwa na viongozi wetu ambao tunawaamini kutoka katika Mihimili tofauti, tunae Jaji Mwenyeiti wa Tume, tunaye Makamu Mwenyekiti wa Tume, tunao Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Haki za Binadamu na Utawala Bora na mtu mwingine ambaye Mheshimiwa Rais anamteua kwa kuzingatia jinsia. Hao ndiyo wanaunda Kamati ya Usaili. Wao kwa nafasi walizopewa wanapendekeza Wajumbe ambao watakuwa ni Wajumbe wa Tume baada ya kumpelekea Mheshimiwa Rais yeye mwenyewe akateua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa mustakabali mkubwa, kwa kweli Mheshimiwa Rais ameamua kwa moyo wa dhati kuhakikisha kwamba anaishi katika falsafa yake ya *4R* ya mabadiliko katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaangalia katika *context* kubwa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, tumeona hata jana katika vyombo vya habari, wanatoa taarifa kama vile Kamati ilichobadilisha ni kuweka jina tu Tume huru, ukiangalia undani wa mabadiliko yote yaliyoko mle ndani na ninaomba Waandishi wa Habari wanaandika habari wakiwa katika nchi ya amani, wasipotoshe kuona *context* kubwa iliyopo katika mabadiliko ya sheria hii na kuita kwamba kitu kilichobadilishwa katika sheria hii ni neno Tume Huru ya Uchaguzi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia pia katika Ibara ya 74 Kifungu Kidogo cha Saba, Tume hii ilishaonesha kwanza wazi naomba kurejea kwamba: ‘‘Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake yaliyoainishwa katika Ibara hii, Tume ya Uchaguzi itakuwa ni idara huru inayojitegemea”. Kwa hiyo, haya mambo yote yamekuwa yakiishi katika Tume hiyo na sasa tumeboresha mustakabali wa jinsi ya kupata viongozi na wajumbe wetu wa Tume, mustakabali wa kupata namna njema ambayo Rais atateua Mkurugenzi Mkuu wa Tume, hii yote haiwezi kutupeleka pengine tofauti na kutupeleka katika Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kuna wengine ambao walisema labda jina hili linavunja Katiba. Ukiangalia katika Kifungu cha 74 (1), inasema kuanzishwa kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, katika eneo hili haikutoa jina. Ukiangalia katika taasisi zingine za Serikali wakati zinaanzishwa, nikiangalia Tume ya Utumishi wa Mahakama Ibara ya 112 (1), kwa ridhaa yako naomba nikirejee hapa ukisoma utaona Katiba ilitunga hiyo Tume pia ilielekeza jina liitweje. Naomba kurejea Ibara ya 112 (1), kutakuwa na Tume ya Ushauri na Uteuzi wa Majaji na ajira ya Mahakimu wa Mahakama za Tanzania Bara ambayo kwa Katiba hii itaitwa Tume ya Utumishi wa Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda Ibara ya 129 na yenyewe wakati wa kuanzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na yenyewe imeongea wazi kwamba, kwa mujibu wa Katiba hii kutakuwa na Tume itakayoitwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, lakini katika eneo la Tume ya Uchaguzi ilitaja kutakuwa na Tume. Kwa hiyo, leo tunapokuwa tunaita Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, hakuna uvunjifu wa Katiba tuliyo nayo. Kwa hiyo, mimi kwa mchango wangu pia na kwa mchango wa Wajumbe wa Kamati, tunaona kwamba ni jina zuri linaloakisi mabadiliko yote yaliyotokea ndani ya muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikienda katika Muswada mwingine wa Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Mimi katika eneo hilo nitajikita tu katika Ibara ya 6 ambayo muswada ulikuwa ukitaja kwamba kila Mkurugenzi wa Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya atakuwa msimamizi wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, niki-*declare* kwamba, katika maisha yangu nilipata kuwa mtumishi katika ngazi wa Ukurugenzi wa Wilaya na nilipata kusimamia uchaguzi. Katika eneo hili, upo utaratibu mzuri wa Serikali. Kwanza, unakula kiapo cha kutunza siri, lakini unakula kiapo pia cha kukana Chama chako kama wewe ni mwanachama wa chama chochote cha siasa katika kipindi chote unachosimamia uchaguzi. Katika eneo hili hatukuwahi kupata maelekezo yoyote nje ya utaratibu wa maadili ya utumishi wa umma ya kufanya tofauti na tulivyoelekezwa na sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeangalia katika eneo hii kwa sababu wakati tunapokea maoni kwa kweli eneo hili lilikuwa ni eneo lililoleta malalamiko makubwa na likawa linaongelewa sana kuhusiana na Wakurugenzi wa Wilaya. Mimi nikaenda ndani kuangalia, pamoja na maoni mengine yaliyotolewa na viongozi wa vyama vya siasa waliokuja kutoa maoni tukaona tatizo ni nini na limetoka wapi?

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika chaguzi zilizopita, nikianzia tu hapa karibu mwaka 2010, tunaona katika eneo hili na katika Bunge lako Tukufu humu tulikuwa na Wabunge 88 kutoka vyama rafiki, ukitoa sehemu ya Wabunge hawo ambao ni wa Viti Maalum, waliobaki ni wa Majimbo ambao walitangazwa na Wakurugenzi. Mwaka 2015 Wabunge wa vyama rafiki waliongezeka ambao walifikia 116 ambapo sehemu kubwa ya Wabunge hao ni Wabunge wa Majimbo ambao walitangazwa na Wakurugenzi hao. Ilivyokuja mwaka 2020 wote tunajua kwamba kulikuwa na kushuka kwa Wabunge wa vyama rafiki lakini sababu ni nini?

Mheshimiwa Spika, tukiona mwaka 2015 maana yake kulikuwa na hamasa kubwa katika vyama hivyo, kwanza wenyewe waliungana na kuwa na msemo wa pamoja na kusimamisha viongozi wanaokubalika katika jamii lakini mwaka 2020 ilikuwa ni tofauti. Kwa hiyo, unaweza ukatafuta sababu ukaangukia katika sababu ambayo haitakusaidia. Leo hata tukileta malaika kutoka mbinguni wasimamie uchaguzi katika

Majimbo, kama zile sababu za msingi, vyama hivyo havijazitibu haiwezi kusaidia katika kufanikiwa. Kwa hiyo, mimi nawaomba sana waangalie sababu ambayo ni ya msingi iliyosababisha kushuka na kupata viti hapa katika Bunge lako. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kyombo, kuna taarifa kutoka kwa Mweshimiwa Ole-Sendeka.

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa mzungumzaji makini taarifa fupi tu, kwamba katika suala la nani anasimamia uchaguzi na ameteuliwa na nani, uzoefu wa dunia unaonesha kwamba ushindi unatokana na umakini wa chama chenyewe kilivyojitambulisha kwa umma.

Mheshimiwa Spika, ukienda nchi ya jirani ya Zambia, Rais aliyeko leo amepatikana chini ya uongozi wa Tume ambayo hakuiunda yeye, iliundwa na uongozi ulioangushwa. Ukienda nchini Kenya Rais aliyeko leo ametangazwa na Tume ambayo hakuiunda yeye iliundwa na Mheshimiwa Rais ambaye alihama kwenda huko kwenye upande wa pili.

Mheshimiwa Spika, ukienda nchi nyingine zote ambazo mabadiliko yamefanyika ikiwemo wakati wa kuondoka kwa Serikali ya *KANU*, Moi ndiye aliyeunda Tume ya Uchaguzi na aliondolewa na Mwayi Kibaki wakati yeye mwenyewe akiambulia asilimia 25. Kwa hiyo, suala kubwa ni kuvipanga vyama vya siasa, kuvijenga vyama vinavyojitambulisha na waliowengi na siyo kufikiri kwamba kuwepo kwa sheria au Tume Huru inatosha kuingiza chama ambacho hakijajipanga madarakani, haiwezekani kamwe! *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa sababu inaboresha mchango wangu na ndiyo hali halisi ya dunia ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo hilo Kamati tumependekeza na kukubaliana na Serikali kwamba, ili tuondoe wigo mpana wa Serikali kuteua wasimamizi wa uchaguzi katika Majimbo na maeneo ambayo yatakuwa na uchaguzi basi tuwe na Afisa Mwandamizi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliongea hili kwamba miongoni mwa Maafisa Waandamizi hata Wakurugenzi wako ndani ya maeneo hayo. Kwa hiyo, tusije tukaja baadae tukaona Wakurugenzi wameteuliwa kusimamia uchaguzi mtu akasema sheria ilipitisha Maafisa Waandamizi. Wakurugenzi na wenyewe ni sehemu ya Maafisa Waandamizi pale Tume itakapojiridhisha Mkurugenzi ana *conduct* nzuri na maadili mazuri, atateuliwa kusimamia uchaguzi kwa mujibu wa taratibu za Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa hiyo, katika eneo hili naomba tuliweke sawa na usimamizi wa uchaguzi unaenda kwa uzalendo na utiifu wa sheria na siyo cheo cha mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo la muswada huu tumeona katika maeneo mbalimbali na Ibara mbalimbali ambazo tumeongelea *gender*, tumeongelea jinsi ya kupata wagombea wanawake wa viti maalum, katika eneo hili tunahitaji kuona akina mama wakiongezeka. Ipo mifano mizuri imetolewa katika nchi yetu, utawala ambao unaongozwa na akina mama tumeona mifano mizuri. Kwa hiyo, katika maeneo hayo zipo Ibara nyingi ambazo tumeweka jinsi ya kuhakikisha kwamba, tunapokuwa katika michakato ya uchaguzi basi akina mama waweze kupewa kipaumbele katika Ibara hizo.

Mheshimiwa Spika, pia tumeweka Kifungu na Ibara maalum ambayo inaelezea makosa ya unyanyasaji wa kijinsia hasa wakati wa uchaguzi. Naomba akina mama kwa kweli kwa miswada hii, wengi mtembee mkiwa mnajiamini, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshaweka mazingira mazuri ya ninyi kuhakikisha

katika chaguzi zinazokuja basi mnakuwa hamna uoga wowote kwenda kukabiliana na uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo langu lingine ni Sheria ya Marekebisho ya Vyama vya Siasa katika eneo hili nitaongelea sehemu ndogo ya ruzuku kwa vyama vya uwakilishi katika. Tunaona Serikali imekuja na utaratibu mzuri ambao tuliuunga mkono, mwanzo ilikuwa baada ya uchaguzi kila chama kinapata ruzuku yake kutokana na matokeo iliyopata, hiyo ni kura za Wabunge na Madiwani na katikati hapo ilikuwa ikitokea tena uchaguzi mwingine, labda kiti ambacho kilikuwa chama kingine kikahamia chama kingine ile ruzuku ilikuwa haibadiliki.

Mheshimiwa Spika, kwa umahiri wa Mheshimiwa Mama yetu ambaye anataka maridhiano, ustahimilivu, mabadiliko na kujenga nchi yetu upya, akaona hii siyo sawa. Pale tunapokuwa na uchaguzi mdogo ikaonekana uongozi labda kiti kimoja kimehamia chamba kingine, basi huo uongozi mpya unahama na ruzuku yake. Kwa hiyo, kila mtu *at pointing time* watakuwa wanapata ruzuku kulingana na uwakilishi wao walionao.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiangalia haya yote kwa kweli ni upendo mkubwa wa Mheshimiwa Rais wetu ambaye anaona kwamba, kwa kuishi hivi na kustahimiliana nchi yetu itaendelea kuwa ya amani, itandelea kusonga mbele kiuchumi na wote tutaendelea kusikilizana.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili vyama vingi viliomba…

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili imegonga.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nakushukuru kwa nafasi na ninaunga mkono hoja katika Miswada yote mitatu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kuna wageni ambao waliingia Bungeni baada ya tangazo la wageni la kwanza tuliowatangaza, hawa ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria ni wanakwaya wa

kwaya ya Mahakama ya Tanzania ijulikanayo kama Ng'aring'ari *choir one* kutoka Dar es Salaam. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Yahaya Omary Massare tutamalizia na Mheshimiwa Stella Martin Manyanya.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, tunazo sheria mbele yetu na kwa bahati nzuri mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati iliyochakata sheria hizi, ninataka niseme kwamba, naomba Waheshimiwa Wabunge wakubali mchakato huu ulikuwa wazi na huru wapitishe sheria hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama nchi tulikotoka na tulipo tuna mwendelezo mzuri sana wa sera za siasa ambazo Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere ametupa misingi bora sana katika nchi hii. Tumeshuhudia nchi ikiwa katika chama kimoja lakini hatimaye maoni ya asilimia chache ya wananchi wanaohitaji vyama vingi yalichukuliwa na hatimaye mwaka 1995 tukarudi tena katika uchaguzi wa vyama vingi kama ilivyokuwa miaka ya nyuma kule kabla ya uhuru.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na sheria mbili za uchaguzi wa Mheshimiwa Rais na Wabunge na Sheria ya Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji ambayo ilikuwa inasimamiwa na Wizara yetu ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Tunapokwenda kuunganisha sheria hizi, kufanya sasa tuwe na sheria moja ya Mheshimiwa Rais, Wabunge na Madiwani tunaenda kuipa Tume wajibu wa kufanya kazi yake vizuri na kwa weledi mkubwa. Maana yake ni nini? Tunakwenda kusaidia na kuondoa ombwe lililokuwepo kwamba, katika uchaguzi mmoja kuna kundi moja linasimamiwa na taasisi nyingine na kundi lingine linasimamiwa na taasisi nyingine. Kwa hiyo, tunapokwenda katika uchaguzi ujao wa mwaka 2025 maana yake Rais, Wabunge na Madiwani watasimamiwa na sheria hii ambayo leo tunakwenda

kuipitisha tunaenda kuomba Bunge lako Tukufu hili likapitishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika sheria hii kuna jambo ambalo bado Kamati iliona lina ukakasi. Tunapoenda ku-*merge* sheria hizi, katika sheria ya mwanzo ambayo inaenda kuungana sasa tupate sheria moja ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ilikuwa kama kuna nafasi ya wazi ya Diwani ikitokea inatangwazwa na Mheshimiwa Waziri na ndiyo anayepeleka kwenye Tume ili itangaze kwamba nafasi hii iko wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imeona kutokana na mashauriano, kama lilivyo Bunge kwamba Spika wa Bunge ndiyo anapeleka taarifa kwenye Tume kwamba, Mbunge fulani aidha kwa namna yoyote amefariki au kiti chake kiko wazi Spika ndiyo anayepeleka. Tumeona mlolongo wa kwamba Mwenyekiti wa Halmashauri amwandikie Mheshimiwa Waziri, ndiyo Mheshimiwa Waziri apeleke kwenye Tume tunaona ni *process* ndefu na sheria hii tumeiona, naomba Bunge lako Tukufu likubaliane na Kamati kwamba sasa Mwenyekiti wa Halmashauri husika ndiyo amuarifu Mkurugenzi wa Tume kwamba kiti cha Diwani wa Jimbo fulani au kitu cha Diwani wa Viti Maalum katika eneo lake kipo wazi ili aweze kutangaza, hii itapunguza majukumu ya Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambapo ana majukumu mengi ya kufanya kuliko hili ambalo lilikuwa katika mikono yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 57 ya Muswada huu inajadili na kuona namna gani maandishi ya nukta nundu yatakuwepo katika karatasi za kupigia kura *(ballot paper)*. Naomba Waheshimiwa Wabunge walione ni jambo ambalo ni mahususi na lijadiliwe kwa maslahi mapana ya nchi na jamii yetu kwa watu ambao wana uoni hafifu na wasioona kabisa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 112 na 113 inahusisha namna gani masharti ya uteuzi wa wanawake katika nafasi maalum. Ibara hizi za Muswada, lakini pia imetajwa katika Ibara za Katiba, wengi walitamani kwamba kuwe na mfumo maalum wa vyama vyote kuwa na mfumo mmoja, lakini bado tunaona Muswada huu

uko sawa kwa sababu vyama vya siasa vyenyewe vitaona namna gani iliyo bora uteuzi wa wanawake katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, wengine walitamani katika maoni ya wadau kwamba kuwe na mfumo maalum. Naamini katika chama changu, Chama cha Mapinduzi kuna mfumo ambao ni mzuri sana na kama wengine wanaweza kuiga, basi itakuwa ni jambo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuna mengi na wadau walijitokeza kwa wingi sana. Wengine wanadhani uhuru wa Tume ni neno tu. Uhuru wa Tume ni mfumo mzima na Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi atateuliwa na Mheshimiwa Rais, lakini miongoni mwa Majaji. Kwa hiyo, ni taasisi ambayo muhimili wa kutoa haki ndiyo utahusika na Tume hii. Kwa hiyo, tutakuwa na Tume ambayo itakuwa na watu wenye weledi wa kutosha lakini Makamu wake pia atakuwa ni miongoni mwa Majaji wanaotokea katika upande wa pili wa Muungano kama mmoja atatoka upande mmoja wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, neno 'uhuru' tu pekee yake haitoshi kama hatutakuwa na watu wenye dhamira ya kweli ya kutenda haki na kutoa uhuru wa kweli na wale waliopewa dhamana watasimamia kwa maslahi mapana ya Taifa. Hapa maana yake ni nini? Wale Wajumbe ambao watapita kwenye Kamati ya Usaili ambayo Mwenyekiti wake atakuwa Jaji Mkuu, Kamati hii ya Usaili itakuwa na Wajumbe wengine na Makamu wake atakuwa ni Jaji wa Zanzibar. Maana yake ni kwamba *judiciary* wanahusika moja kwa moja katika kuchakata wale Wajumbe watano ambao watateuliwa na Tume kuwa Wajumbe wa Tume.

Mheshimiwa Spika, hapa sheria inaenda kumwondoa Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi asiwe Katibu wa ile Tume, kwa sababu wale watakaoteuliwa atakuja kufanyanao kazi. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba Tume sasa inaenda kuwa huru zaidi kutokana na mchakato huu ambao unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuna maneno alikuwa ananiambia hapa Mheshimiwa Shamsi, kule Zanzibar wanasema kwamba unaweza

kuwa na paka mwizi lakini ukampa jina zuri, bado atakuwa ni mwizi yule yule, paka anayedokoa mchuzi. Kwa hiyo, hapa sisi tunaenda kutengeneza watu wenye maarifa na weledi wakutosha kusimamia Tume hii ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa hiyo, tunaomba jamiii ya Watanzania waone kwamba Kamati yako ya Bunge imefanya kazi kubwa ya kuhakikisha watu watakaotokana na Tume hii ya Uchaguzi na hasa wale watakaoomba pia wanakuwa ni watu mahiri na pia *gender* itazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Vyama vya Siasa kuna mambo yamezungumziwa sana, lakini tunatamani kuona viongozi wa Vyama vya Siasa ambao hatimaye watakuja kuwa viongozi wa nchi, nao wanaangaliwa kwa mtazamo mpana. Ni vyama vichache ambavyo viongozi wake wa vyama vya siasa ambao wanaingia kwenye uchaguzi wana weledi wa kutosha kuongoza nchi. Maana yake uchaguzi unaweza kuamua miongoni mwa mtu yeyote katika cha chochote akawa Rais au akashinda Urais. Sasa hapa napo panatakiwa kuangaliwa vizuri, wale viongozi wa Vyama vya Siasa ambao vyama vyao vinaingia katika uchaguzi, weledi wao na ubora wao na uzalendo wao kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii tumerithi kutoka kwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere; Rais wa pili Mheshimiwa Ally Hassan Mwinyi; Rais wa tatu, Mheshimiwa Mkapa; wanne na watano na sasa tuko Rais wa sita, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameendelea kuimarisha amani, umoja wetu kama Taifa na mshikamano wetu. Haya ndiyo mambo yatakayoongoza Kamati kuhakikisha wanatunga sheria ambazo zitakuwa bora na nzuri ambazo zimeletwa katika Bunge lako hili Tukufu. Hata yale ambayo tumepishana na Serikali yalikuwa na maana njema ya kujenga kwa maana maslahi mapana ya nchi yanazingatiwa katika utunzi huu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, umoja wetu kama Taifa na Muungano wetu ambao nchi nyingi za kiafrika na hata huko duniani zilijaribu na zikashindwa na leo Tanzania, Tanganyika na Zanzibar zilipoungana, bado ni nchi moja yenye Serikali mbili, Serikali ambazo zina makubaliano, lakini chini ya chama kimoja

ambacho kilisimamia; na leo tuna vyama vingi ambavyo nchi inatawalika na hakuna fujo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata juzi tumeona watu wakiandamana kama walivyosema wenzangu lakini wakilindwa na Polisi na kuhakikishiwa usalama wao na afya zao kama kutatokea changamoto yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia tena kuwaomba Wabunge wenzangu waunge mkono hoja hizi zilizoletwa mbele yako za sheria hizi tatu ili zipite na zikafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Kamati zetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stella Martin Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi. Kwanza nami niungane na wenzangu kuanzia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku hii ya leo. Pia kwa namna ya pekee kabisa namshukuru na kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kukubali kuleta Miswada hii hapa Bungeni, na kwa jitihada kubwa anayoifanya kuhakikisha kwamba Taifa letu la Tanzania linaendelea kuwa na amani, linaendelea kuwa imara, linaendelea kuwa na mshikamano na pia kufanya marekebisho yote yanayostahili kwa mustakabali mpana wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia wanaomsaidia; Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu pamoja na Naibu wake, Mawaziri waliosaidia katika kuleta sheria hii, ndugu yangu, mdogo wangu, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu wake na Mawaziri wote walioshirikiana na wadau wote kwa ujumla wake ambao leo tunataka kuleta mwarobaini wa changamoto zinazowakabili wananchi kwa ujumla wake kuhusiana na masuala mazima ya kisiasa na hasa katika maeneo ya uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sijui kama nitaweza kuongea vizuri kama wenzangu waliotangulia, kwa kweli wameongea mambo mengi mazuri. Binafsi naunga mkono kwanza suala la kuweka kifungu kinachodhibiti uzalilishaji katika sheria hii. Udhalilishaji tunaouzungumzia sio wa wanawake tu, hata wanaume, hata watu kwa umri wao; jinsia za aina nyingi, wale watu wenye ulemavu, yaani mtu anaweza akamwona mtu mwenye ulemavu anagombea, akasema "na huyu naye anahaingaika nini?" "Huyu mzee naye si apumzike tu!" Yaani mambo ni mengi. Au mwingine tu akatungiwa neno, "huyu shoga huyu." Mambo mengi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naungana na wenzangu kusema kifungu hiki kiwepo, kisaidie kuhakikisha kwamba kinadhibiti vitendo vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi wakati mwingine wanaotumiwa kufanya kazi hiyo ya udhalilishaji au uchafuaji kimaneno ni vijana ambao hata wenyewe hawaruhusiwi kupigakura. Wanaambiwa, nenda kafanye hiki na hiki, matokeo yake wanajikuta wanaingia kwenye makosa bila sababu yoyote ile. Kwa hiyo, hicho kifungu ni muhimu kiwepo.

Mheshimiwa Spika, la pili, niseme pia kuhusiana na Tume. Tume Huru maana yake siyo kwamba imefungiwa uhuru Serikali isiweke mikono yake, lakini watu, mataifa ya nje yaweke mikono yao. Huru, huru kweli katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kuwa na utulivu na amani yake. Kwa hiyo, ili iwe huru pia, suala la wanawake kuwemo katika Tume hiyo ni muhimu sana. Hapa haijatamka bayana. Tunahitaji kama ambavyo sasa hivi tunahakikisha tunafanya mambo ya kusawazisha, Tume hii pia ijioneshe wazi itakuwa ni ya kutenga haki tutakapoona wanawake wa kutosha. Kama wako watano, basi asilimia 40 au 60. Maana yake kwenye tano huwezi kugawa kati, basi (ke) na (me) ziwe zinaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye Muswada wa Vyama vya Siasa. Hapo naenda kwenye Kifungu kilichozungumziwa pia na wenzangu hiki cha 13 ambacho kipo kwenye Muswada mpya na hasa kwenye haya marekebisho yanayoingia. Naipongeza sana

Serikali na wadau kwa kuona umuhimu wa Vyama vya Siasa kuwa na sera maalum zinazohusu masuala ya jinsia na kuweka usawa unaotakiwa katika jamii zetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba zitaweka, bahati nzuri nilikuwa Mbunge katika Bunge la *SADC* kwa takribani miaka 10. Masuala hayo ya jinsia yamezungumzwa kwenye nchi hii kwa muda mrefu sana. Nikirudi moja kwa moja kwenye masuala ya wanawake kupata nafasi za uongozi na maamuzi, yamezungumziwa kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Beijing mwaka 1995 sasa hivi ni miaka 29, akina Mama, Bibi Titi, wameanza kuzungumza masuala hayo toka kipindi cha uhuru, lakini sisi wenyewe Tanzania tumeridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa. Mkataba mmojawapo ni Mkataba wa *SADC* unaohusiana na masuala ya jinsia na maendeleo, ambao tuliupitisha humu Bungeni tarehe 22 Februari, 2013. Miaka yote hiyo tunaimba jambo hilo hilo, hatufiki mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa uchunguzi wangu na hata tulivyokuwa tunajadiliana, changamoto kubwa inayosababisha kushindwa kufikia hasa katika masuala haya ya kisiasa ni kwenye vyama. Vyama vya Siasa vimeweka taratibu ambazo zinatuchelewesha kufika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imemwekea mipaka hata Mheshimiwa Rais. Atateua Wabunge 10; watano wanawake, watano wanaume. Katiba yetu ilipoona tunachelewa, ikaamua kuweka nafasi za Wabunge Wanawake wa Viti Maalum ilimradi angalau kuziba mapengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kila wakati imekuwa idadi ya Wabunge wa Viti Maalum inaongezeka labda kutoka 50, 75 sasa hivi 100. Sasa tutakuwa tunaongeza idadi ya Wabunge wa Viti Maalum ili kufikia usawa wa kijinsia, matokeo yake itabidi tuongeze na ukubwa wa ukumbi huu kwa sababu kwenye Majimbo kumebakia vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani tufike mahali tukubaliane, kwa sababu hatuna mpango wa kurekebisha Katiba sasa hivi, turudi kwenye sheria. Sheria hii itamke wazi, ielekeze Vyama vya Siasa kutenga angalau asilimia 30 ya wale watakaogombea kwenye Majimbo ya Uchaguzi au kwenye Kata za Uchaguzi au nafasi zile za Uchaguzi ikiwemo na ndani ya vyama.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani! Huyu mwanamke ni kiumbe gani ambaye kila siku anazungumzwa lakini haifiki? Hawapo wanawake! Nimefuatilia kwenye Sensa ya Mwaka 2012, Sensa ya Mwaka 2022, ukiangalia mgawanyiko *(distribution)* wa wanawake, tunaposema kwamba ni asilimia 52 wanawake, sio tu kwa ujumla wake, labda pengine Mkoa wa Dar es Salaam una idadi kubwa, mwingine kidogo, ndiyo maana tukapata wastani huo, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefuatilia nimekuta kwamba hata ukienda kimkoa, utakuta mgao ni hivyo hivyo. Ukienda kwenye Kata, mgao ni hivyo hivyo; ukienda kwenye umri, mgao ni hivyo hivyo. Kwa hiyo, hiyo ni *formular* ambayo Mwenyezi Mungu aliiweka. Kwa nini tunapingana nayo? *(Makofi)*

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi…

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Manyanya, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Edwin Swalle.

**TAARIFA**

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kumpa taarifa *Engineer* Stella Manyanya, ambaye anachangia vizuri sana, ambaye anapendekeza kwamba angalau asilimia 30. Nampa taarifa kwamba, mtu yeyote ambaye amekaa miezi tisa

kwenye tumbo la mwanamke akiwa hana choo na hawezi kula, hana sababu ya kupinga usawa wa kijinsia katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, badala ya asilimia, hatuna sababu ya kuona aibu kuweka asilimia 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Nembo yetu ya Taifa imetuelekeza hapo mgongoni kwako; mwanaume na mwanamke. Kwa hiyo, ni mambo mengi yana uhusiano. Isipokuwa mimi nilikuwa nasema angalau asilimia 30 kwa sababu Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari imetuwekea siyo chini ya asilimia 30 ya Wabunge watatokana na Viti Maalum. Kwa hiyo, nikaona kwa sababu ile kikatiba haitakuwa imeondolewa, basi na sisi sio lengo letu tukae sisi wanawake peke yetu tuwaache wanaume, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi hatutaki kutengeneza kosa lingine lililotokea miaka mingi, tunawahitaji sana wanaume kuwa nao katika kushirikiana, ndiyo maana tukasema kwamba kwenye vyama watuletee angalau asilimia 30. Tukipita kwenye uchaguzi huko tutakavyoenda tukapata kitakachotoka, ukijumuisha na wale wa Viti Maalum, tutajikuta tunakaa tumeshanyooka, mambo yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ya kuendelea kubembelezana kila siku, vyama vitakuwa na sera, wataleta Sera ya Jinsia; hizo sera ziko miaka yote, hawaoni. Kuna vyama vingine vinaenda mbali zaidi, hata namna ya kuwapata hawa Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum, hakueleweki eleweki. Ndiyo maana tunasema kwamba Tume imepewa kazi hiyo kikatiba kuweka utaratibu. Kwa

nini haiweki utaratibu namna ya kupatikana Wabunge wa Viti Maalum? Tume iliacha majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunasema Tume iweke utaratibu lakini kwa kutushirikisha tuweze kuona unakuwa utaratibu upi wa wazi, kwa sababu kama hakuna uwazi, hata yale tunayosema ya udhalilishaji mengine yanatoka humu humu. Jamani dunia ina mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi katika suala la mwanamke au katika suala la kijinsia, hatuangalii huyu ni wa chama gani, huyu ni wa chama kipi? Tunasema wanawake wote wasipitie kitendo chochote kinacholeta udhalilishaji au usumbufu au shida katika kuwazuia kuingia katika maeneo ya uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, sensa inaonesha wazi, umri wa watu wazima idadi yao wako wangapi? Watu wenye ulemavu wako wangapi? Kwa hiyo, ile asilimia tuione ikijitokeza hata kwenye ngazi zetu za maamuzi, jinsia hizo zijitokeze. Tunaposema jinsia, hatumaanishi tu wanawake na wanaume, hata hayo makundi maalum yaonekane yakishiriki inavyotakiwa. Hii ndiyo itakuwa nchi salama ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa leo, kwa kweli hasa msisitizo wangu ni huo. Nakushukuru sana na ninaomba asilimia hiyo ionekane kwenye sheria ikiwaelekeza vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kukutana kwetu leo.

Sasa niyasome majina ya baadhi ya Wabunge ambao tutaanza nao mchana; Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mheshimiwa Francis Kumba

Ndulane, Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza na wengine wataendelea kutajwa kadiri muda utakavyokuwa unakwenda.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023**

**Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 *(The Political Parties Affairs Laws (Amendment) Bill, 2023)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Tutaanza na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa na mimi fursa niweze kuchangia katika Miswada yetu hii muhimu kwa mustakabari wa maendeleo na ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia kwanza nikuombe kwa ridhaa yako nitoe pole kwa wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini na waislamu na Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na Sheikh wetu ambaye alikuwa ni Sheikh maarufu sana Maalimu Mkoani Singida Sheikh Khamis Nkungu ambaye alifariki hapa hospitali ya Benjamin Mkapa na hatimaye kuzikwa leo asubuhi pale katika Kijiji cha Mwandumo Mghamo Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, nawapa pole sana wananchi wenzangu sijaweza kushiriki lakini tupo pamoja ni kwa sababu ya majukumu haya. Naomba tena nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ameendelea kuliheshimisha Taifa letu, ameendelea kuwatumikia Watanzania kwa moyo wake wote na kwa unyenyekevu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kipekee sana niseme tu hapa kwamba kwa wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini hapa tunapoongea Mheshimiwa Rais ametumwagia fedha shilingi bilioni moja, milioni mia tano, kumi na saba na laki sita kwa ajili ya vyumba vya madarasa katika shule za Sekondari, vyumba vya madarasa 53 na matundu ya vyoo 152 hizi hela zimeingia juzi na sasa kazi inaenda kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu siyo tu kwenye demokrasia, siyo tu kwenye utawala bora lakini hata kwenye sekta mahususi kama hivi elimu tunaona Mheshimiwa Rais anavyowahudumia Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nikirudi sasa kwenye Miswada yetu ningependa sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania kwa ujumla wangefahamu na kufuatilia ipasavyo mjadala huu ambao Mheshimiwa Rais ameuasisi na kuuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ameupeleka kwa wananchi na sasa tunao hapa Bungeni kwa ajili ya kujadili na kupitia ku-*review* Sheria yetu ya uchaguzi wa Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa

Wabunge na Waheshimiwa Madiwani lakini pia ku-*review* Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi lakini pia na Sheria ya vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, hizi ni Sheria ambazo zinaleta ustawi wa Taifa letu. Zinaleta maelewano, zinaleta maendeleo na pia zinaleta uchangamano kwa wananchi wetu. Pia ningesema tu kidogo kwa upande wa Tanzania hasa wa vyama. Hii ni fursa muhimu ambayo Mheshimiwa Rais ameiweka mezani kwa kupitia zile *principals* zake zile za *4R* za upatanishi, *reconciliation, resilience*, ustahimilifu, *reforms* pamoja na *rebuilding*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningefurahi sana kama Watanzania wangezielewa hizi *elements* au hizi *4R's* za Mheshimiwa Rais halafu tuzitafsiri katika maisha yetu ya kila siku zingeweza kutusaidia sana kulijenga hili Taifa upya na kuhakikisha tunaleta maendeleo hasa upande wa demokrasia. Tunafahamu *dynamics* ambazo tumepitia tangu kuwe na mfumo wa vyama vingi.

Mheshimiwa Spika, leo Mheshimiwa Rais ameleta mjadala hajaleta uoga, hajaingiza uoga amejiamini. Unafahamu kumekuwa na *tendence* katika jamii nadhani ni Waafrika labda kwamba wanawake hadi wawezeshwe ndiyo waweze lakini Mheshimiwa Rais ameonyesha kuweza bila kuwezeshwa. Amejiamini, ameleta hii Miswada hapa mbele yetu tujadili kwa watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati sasa sisi Watanzania kwa ujumla pamoja na wale wanaompinga waone kwamba Mheshimiwa Rais hana ubaya, hana ubaguzi anawapenda Watanzania wote nani mpenda demokrasia, mpokea mawazo. Kwa hiyo, tutoe mawazo katika njia rasmi ili Mheshimiwa Rais wetu aweze kuzifanyia kazi. Huu siyo wakati wa kwenda barabarani kuandamana kwa sababu wewe ukiandamana watu wanatunga Sheria inakuwa haina msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye Miswada kwenye maeneo mahususi nikianza na huu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge na

Waheshimiwa Madiwani ningependa kwenda kwenye Ibara ya 6 ya Muswada ambayo inazungumzia na ambayo ilikuwa ina hisia kubwa hata kwenye kupokea maoni wale watoa maoni, wananchi waliokuja kutoa maoni vyama vya siasa, taasisi za dini, watu mmoja mmoja, taasisi za kiraia, *NGO's* na kadharika.

Mheshimiwa Spika, wengi hawakuacha hichi kipengele kilichokuwa kinagusa eneo la Wakurugenzi wa majiji, wa halamshauri hima kusimamia ama kutokusimamia uchaguzi. Eneo hili lilileta hisia nyingi labda kwa sababu ya *dynamics* ambazo demokrasia katika nchi yetu inapitia. Lakini nilipenda maoni ya baadhi ya watoa maoni ambao walifanya *analysis* ya chaguzi ambazo tumepitia miaka mbali mbali kuanzia 2005, 2010, 2015 mpaka hivi 2020 chaguzi zote zile zilisimamiwa na Wakurugenzi.

Mheshimiwa Spika, chaguzi zote zile zilisimamiwa na Wakurugenzi. chaguzi zote zile zilileta matokea ambayo hapa unaona katika Bunge letu kwa nyakati tofauti tofauti kumekuwa na Waheshimiwa Wabunge wa chama tawala na Waheshimiwa Wabunge wa upinzani. Kwa hiyo, hapa shida siyo nafasi ya Mkurugenzi, siyo Mkurugenzi kama nafasi pengine wengine walikuwa wanaona shida labda ipo kwenye *personalities*, mtu kwa hiyo, isitugawe hili eneo lisitugawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatazama eneo hili kwamba tunatakiwa, hata Serikali imeleta maoni, Kamati imechambua na ikaangalia pia maoni ya wale wadau waliokuja. Kwa mtazamo wangu ninavyotazama kwa ku-*refer* pia majadiliano tuliyokuwanayo kwenye Kamati, Wakurugenzi siyo tatizo nafasi ya Mkurugenzi kama nafasi siyo tatizo, tatizo tumesema ni watu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninataka niishauri Serikali hapa nina afiki mapendekezo yaliyoletwa hapa kwamba anayependekeza sasa siyo lazima awe Mkurugenzi *it is ok, I am ok, I appreciate* lakini tunasema tuwe na mapendekezo ya mtumishi wa umma mwandamizi ambaye kwanza atakuwa ni *vetted*, atakuwa ni mtu mwenye sifa, ambaye ana uadilifu, mzalendo hataangalia upande wowote kwa sababu yeye ni refa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaungana na hii hoja hapa kwamba sasa uteuzi wa watu hawa wanaokwenda kusimamia uchaguzi ili kuondoa mashaka, ili kuondoa hofu kwa wadau mbalimbali wa chaguzi hizi katika nchi yetu wawe ni watu ambao ni bobezi, watu waliotumikia jamii yetu katika utumishi wa umma, wana uzoefu ni waadilifu ni waaminifu na ni wazalendo kwa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii itawaondoa hisia labda kwamba huenda mtu akiwa Mkurugenzi ndiyo shida. Naomba niendelee kuishauri Serikali hapa kwamba maoni iliyokujanayo ni mazuri na naomba yakafanyiwe kazi ipasavyo isiwe tu kwenye maandishi. Yanaweza kuwa kwenye maandishi alafu baadaye ikawa tatizo.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na pacha wake ambaye wanafanana kwa maoni hayo waliyokujanayo na tunawaomba wakayafanyie kazi ipasavyo kwenye utekelezaji ili zile *4R* za Mheshimiwa Rais zionekane kwenye vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niende kwenye Ibara ya 8 ambayo inazungumzia uteuzi wa waratibu wa uchaguzi ambapo kulikuwa kuna maoni kutoka kwa wadau mbalimbali na hili liligusa sana na wale wadau waliokuja kutoa maoni hasa kwamba kuwe na sifa kwa Watanzania waliopo nje ya nchi waweze kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kulikuwa kuna wadau waliotoka nje ya chi kuja kutoa maoni hapa kutoka Marekani wamekuja kutoa maoni kwenye eneo hili ili na wao waliopo ughaibuni kule waweze kupiga kura. Pia hapa ninaona Serikali na yenyewe imelipokea jambo hili na imesema inaenda kufanya utafiti ili liweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa utafiti huo ambao Serikali imesema inaenda kuufanya usichukue muda mrefu ili Watanzania wenzetu walioko huko nje ya nchi nao waweze kutekeleza haki yao ya kuweza kupiga kura na kuchagua viongozi wao. Hapa tuangalie pia mifumo mizuri ambayo itawezesha hili kwa eneo hasa la teknolojia kwa maana ya *IT*, uaminifu na uzalendo kwa

wenzetu wakiwa kule nje ya nchi lisichukuliwe tu *for granted* tuangalie hawa wanaokwenda kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wakitoka kule wakati mwingine huwa tunabadilika mioyo. Kwa hiyo, iangaliwe vizuri, tukalichambue, tulipembue, tulifanyie upembuzi yakinifu ni vigezo gani ambavyo tutajiridhisha, tutavitumia kujiridhisha ili wenzetu wanapopata hii fursa isije ikawa *misused*, isije ikatumika vibaya.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa kuna maoni na hapa pia kwenye Ibara ya 20 na Ibara ya 21 ambayo pale ambapo tunaeleza kwamba ule utaratibu wa kupata kadi ya mpiga kura endapo itapotea, kufutika ama kuharibika pamoja na kuondoa zile ada kulikuwa kuna maoni kwamba Serikali ilikuwa inashauri pengine kuwe na ada mwananchi anapopoteza ile kadi yake basi anapotaka kuirejesha kuwe na ada Kamati ikashauri, tukashauri kwamba tunafahamu hali za Watanzania, tunafahamu hali za wananchi wetu kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, unaposema shilingi elfu moja au elfu mbili ukiwa hapa Dodoma umepiga suti kama mimi shilingi elfu moja ni ndogo lakini kule kijijini kule Singida Kaskazini kule Modeda kuipata shilingi elfu moja mwananchi wa kawaida siyo rahisi kuipata. Naishukuru Serikali naipongeza kwa kupokea maoni ya Kamati kwamba kusiwe na gharama mwananchi anapopoteza kadi au inapoharibika irudishwe *for free* hii naipongeza Serikali na naomba hili lichukuliwe. Kuna eneo hili la… *(Makofi)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa…

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, kumbe dakika 15 ni chache. Eneo jingine nataka nimalizie hapa kwenye Ibara ya 112.

**SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, muda umeisha kabisa?

**SPIKA:** Ndiyo.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, basi nakushukuru sana kwa nafasi lakini yale makosa ya kijinsia yale kwenye uchaguzi naomba hiyo ni Sheria kosa yale makosa ya unyanyasaji wa kijinsia isiwe tu kijinsia iwe ni makosa ya uchaguzi kwa hiyo mtu yoyote anayetoa lugha chafu, kutishiana, kashfa yaingizwe kwenye Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nikushukuru sana kwa nafasi nilifikiri dakika 15 ni nyingi kumbe ni chache. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa ajiandae.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi katika kuchangia siku ya leo katika Miswada mitatu ambazo imewasilishwa mezani kwako, Miswada ya Uchaguzi wa Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge pamoja na Waheshimiwa Madiwani. Muswada wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Muswada unaohusu Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nipende kutumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuonyesha utayari wake wa kuruhusu jambo hili liweze kujadiliwa kwa mapana yake bila kuwa na utayari huo nafikiri Muswada huu usingekuwepo leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, tumeona vikosi kazi mbali mbali vimekaa, vyama vya siasa vimejadili, tumeona makongamano mbalimbali lakini hatimaye tumeona wewe mwenyewe baada ya kufika Bungeni kuruhusu na kuruhusu Kamati ya Katiba, Utawala na Sheria kuweza kuupokea Muswada huu lakini pia Kamati kuruhusu wadau kuweka maoni yao na kuwasilisha na kuchambuliwa na hatimaye leo unaletwa Bungeni kwa ajili ya Bunge zima sasa kuujadili Miswada hii na hatimaye tupate Sheria ambayo

itasababisha kuweza kuunda Sheria ambazo zitaweza kusimamia uchaguzi wetu.

Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi sana kwako kwa zoezi hili lilivyoendeshwa. Ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Utawala na Sheria nimeshiriki kupokea maoni ya wadau wa muda wa siku nne hapa Dodoma na kwa mara ya kwanza tumeshuhudia wingi wa wadau kuwepo katika kuwasilisha mawazo yao katika Kamati yako.

Mheshimiwa Spika, tumekaa asubuhi mpaka jioni tumejaa katika ukumbi wa Msekwa. Siku ya kwanza, siku ya pili, siku ya tatu, siku zote nne wadau wamejaa na tumewasikiliza kwa maoni yao kwa upana wao na katika kupokea mawazo yao hatukuwahi kukataa wazo lolote kwa sababu lilikuwa jukumu la Kamati kupokea mawazo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini wakati tukiendelea kupokea mawazo hayo vipo vyama vingine rafiki vilikuwa vikitangulia mbele kutengeneza siasa ambazo hazikuwa na afya. Mfano tulikuwa na vyama ambavyo vilikuwa vinawasilisha siku ya kwanza wametoa mawazo yao, siku ya pili wametoa mawazo yao, siku ya tatu wametoa mawazo yao na siku ya nne wametoa mawazo yao.

Mheshimiwa Spika, lakini wanatoka kwenye vyombo vya habari wanasema Kamati hii ya Bunge haikutupa nafasi ya kutoa mawazo yetu au wamekataa mawazo yetu kwao kwa hiyo ilikuwa ni kupotosha umma. Hata hivyo katika kupokea na kujadili tuliyapokea na tukawa na muda wa kuyachambua mawazo yote na kuyachakata kwa kina bado wenzetu walienda mbele na wakatangaza kwamba mawazo yetu yamekataliwa, twende barabarani tukaandamane kwa sababu Mawazo yetu yamekatiliwa. Kitu ambacho hakikuwa sahihi ilikuwa ni upoteshaji mkubwa kuwahadaa watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mawazo yote ambayo yalikuwa yameletwa pamoja na wadau wengine, moja, katika mapendekezo yao walikuwa wanapendekeza hata jina la tume;

kwamba jina hili la tume libadilishwe liwe Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, jambo ambalo Kamati imelichukua na leo umeweza kuona katika mapendekezo ya Kamati jina hilo limewasilishwa; lakini wanageuza wanasema hawa wameamua kutuwekea jina ili kutufurahisha.

Mheshimiwa Spika, sasa hawa watu, tumeruhusu watuletee mawazo yao, tumeyapokea na tumeyawasilisha lakini wanageuza na wanabadilika. Lakini, katika hoja zote ambazo zimeonekana kubwa hoja takriban 83 mawazo yao na hoja zao, hoja 64 kati ya 83 zimechukuliwa na Kamati, zilizobaki ni hoja 19. Kumbe kamati imefanya kazi kubwa katika kuchukua mawazo ya wadau wote kuhusiana na hii miswada yote mitatu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Kamati yako imefanya kazi kubwa na Watanzania wanapaswa kuelewa kwamba kazi imefanyika. Lengo ni jema, kwa sababu Taifa letu hatuwezi tukawa tunaenda duniani tunasema Tanzania ifanane na Kenya, ifanane na Afrika Kusini au ifanane na Marekani, haiwezekani. Kila nchi ina tamaduni zake na sheria zake. Tuna namna ambavyo tumepata uhuru, tunatofautiana. Leo ukiniambia Tanzania ifanane na Kenya, Kenya walipata katiba mpya, lakini baada ya uchaguzi pamoja na kwamba walipata katiba mpya tumeona wameingia barabarani na tumeona migogoro mikubwa imetokea.

Mheshimiwa Spika, tumeona watu wakipoteza maisha yao. Tumeona biashara zimebadilika. Hatuwezi kusema tunataka tufanane na wao. Mnataka tufanane kwa kuvunja amani ya nchi yetu? Tufanane kwa kuandamana kuzuia watu wasifanye biashara? Haiwezekani. Wanatuambia tufanane na Marekani?

Mheshimiwa Spika, Marekani wamepata uhuru wa Taifa lao mwaka 1774 tangu miaka ile zaidi ya miaka 200 Taifa hilo. Tunazungumza marais 45, leo unataka ufafananishe na Taifa lenye marais watano haiwezekani. Pamoja na kwamba wana marais wote hao, juzi uchaguzi ule wa mwaka elfu na uchaguzi ule wa akina Trump na Bidden tumeona migogoro, maandamano na vurugu mpaka wamepelekana mahakamani. Kwa hiyo

unaweza kuona Taifa kubwa duniani bado wanapeleka masuala ya uchaguzi kwenye Mahakama.

Mheshimiwa Spika, sisi tutakwenda kulingana na sheria zetu na watanzania walio wengi tumewasikia wakisema. Nimewasikia wakisema, Watanzania walio wengi wanataka hili. hao Watanzania walio wengi ni Watanzania gani? Maana Watanzania waliowengi hapa, sisi wote ni wawakilishi wa hao Watanzania. Wabunge wote tuliopo humu ndani tunaishi kwenye majimbo yetu nani hao hao ndio waliotuchagua tuje humu Bungeni; ndio hao Watanzania walio wengi. Hao Watanzania wengi walioko nje ya jengo hili maana yake tunakwenda kinyume.

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu nikipongeze Chama Cha Mapinduzi. Leo tuna miaka 62 toka tangu uhuru wa Taifa hili hatujaingia vitani. Taifa lina amani, Taifa lina uhuru kila mmoja ana uhuru wa kutembea na kuzurula tunakotaka. Hatujawahi kuvunja amani yetu. Leo tunataka tuvunje amani hii. Nipongeze vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuendelea kudumisha amani na utawala bora katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Watanzania, sisi leo hapa tunazungumza namna gani ya kuufanya uchaguzi uende vizuri, kusiwe na migogoro, lakini kuna watu wanaibuka wanasema haiwezekani. Mfano, tukizungumzia hii miswada, tumezungumza Muswada wa Tume ya Uchaguzi, wamedai tubadilishe jina tumebadilisha. Wamedai hata wale wajumbe wote wasiteuliwe na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, tumepunguza idadi ya wajumbe kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kutoka wajumbe saba ambao wanateuliwa na Mheshimiwa Rais hadi wamebaki wajumbe wawili ambao Mheshimiwa Rais anawateua, na hawa wanateuliwa kwa sifa zao. Kwanza Mwenyekiti wa Kamati na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni Majaji ambao wamepitia kwenye michakato mbalimbali mpaka kufikia nafasi ya kuwa Jaji. Kwa hiyo anapokuwa Jaji peke yake na Tume zote zinaongozwa na Majaji, ukienda Kenya, ukienda Afrika Kusini

ni majaji, hata sisi watanzania tunaongozwa na hao hao majaji ambao tayari…

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo.

**TAARIFA**

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Naomba kumpa taarifa mchangiaji ambaye anachangia vizuri, kwamba wale wajumbe wote wa ile Tume watapita kwenye usaili. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais amekuwa mwanademokrasia kweli kweli. Mwenyekiti na Makamu wake nao watapita kwenye usaili.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Nashukuru sana Mjumbe mwenzangu wa Kamati.

**SPIKA:** Subiri kwanza Mheshimiwa Gulamali. Nimepitia hapa mapendekezo, kwanza nimetazama jedwali ambalo Serikali imeleta, nimetazama pia jedwali lililoletwa na Kamati na nimepitia taarifa ya Kamati. Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, watapitia kwenye usaili? Mheshimiwa Ighondo, haya naona Mwenyekiti amesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Mheshimiwa Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mapendekezo ambayo pia Serikali imeona inafaa ni kwamba, Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume kwa kuzingatia hadhi zao za Ujaji au kuwa Mawakili yatatolewa mapendekezo na si usaili. Kamati ya usaili itatoa mapendekezo ya majina matatu na kwa nafasi ya uenyekiti majina matatu na kwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti na Mheshimiwa Rais atateua kutokana na mapendekezo atakayoyapokea, ahsante.

**SPIKA:** Sawa, kwa hivyo kamati itasaili wajumbe wengine wa tume wakati Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, kwa mapendekezo kwa sababu bado Bunge halijaanza kutunga sheria. Sasa hivi tuko tunachangia.

Waheshimiwa Wabunge, mapendekezo yaliyopo hapa mbele ni mawili. Moja ni kwamba ile kamati ya usaili ipendekeze kwa Mheshimiwa Rais na kwa upande mwingine, Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kwa Muswada ulivyo sasa hivi, ni kwamba wateuliwe moja kwa moja na Mheshimiwa Rais lakini kwa mapendekezo yaliyoletwa kwa upande wa Serikali ni kwamba Jaji Mkuu wa Muungano wa Tanzania wapendekeze hayo majina, kwa hiyo hayo yote tunayatazama. Nilitaka taarifa tu ya Mheshimiwa Ighondo ikae vizuri isije ikampoteza mchangiaji. Wale wawili bado hakuna sehemu ambayo imesema watapitia usaili isipokuwa ni hayo mapendekezo na siku ya Ijumaa tutajua sasa ni lipi litakalopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naamini pia muda utazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 74(1) inampa mamlaka Rais, Mwenyekiti pamoja na Makamu Mwenyekiti, lakini hata hivyo wakati tukiendelea kupokea maoni ya wadau. Wadau walisema wakurugenzi wa uchaguzi katika maeneo yetu wasiwe watumishi wa umma au wasio wakurugenzi. Tukahoji je, mnataka wawe wakina nani? wakasema wawe huru. Huru inakuwaje, maana yake hiyo huru yenyewe ikoje? Tafsiri yake inakuja kwamba tutawaajiri, tukauliza wataajiriwa, na nani atawalipa mishahara maana yake inakuja ni Serikali. Ukilipwa mshahara na Serikali unakuwa nani; maana yake unakuwa mtumishi wa umma. Mtumishi wa umma unamkwepaje kwenye zoezi zima la kusimamia uchaguzi?

Mheshimiwa Spika, zoezi la kumkataa mtumishi wa umma kwenye usimamizi wa uchaguzi haliepukiki kwa namna yoyote ile. Mtumishi wa umma atasimamia uchaguzi na Watanzania

wanapaswa kuelewa kwamba zoezi la usimamizi wa uchaguzi watumishi wa umma ndio watakao simamia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tumeona tume za uchaguzi ambazo zimeteuliwa, Kenya Zambia na nchi zingine zinateuliwa na Marais walioko madarakani lakini hata vyama vya upinzani vinashinda kupitia Tume za Uchaguzi zilizoteuliwa na Rais aliyepo madarakani. Kwa hiyo kuwepo kwa tume haizuii kupigiwa kura na kushinda kwenye uchaguzi. Kwa hiyo, Watanzania wanapaswa kuelewa kwamba jambo hili lina nia njema na wanapaswa kuliunga mkono.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine kwenye vyama vya siasa. Katika Muswada uliopo tunapendekeza namna ya kupatikana kwa Wabunge wa Viti Maalum na Madiwani wa Viti Maalum. Mwongozo uelekeze maana kuna maeneo mengine kupitia mwanya huu akina mama au akina baba wanapitia unyanyasaji katika upatikanaji wa nafasi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka kuondoa hili jambo ili kuwepo na usawa kwa vyama vyote, upatikanaji wa madiwani na wabunge wa viti maalum mwongozo wake uwekwe sawa na wazi.

Mheshimiwa Spika, pia hata katika Muswada huu wa vyama vya siasa, tumependekeza kesi za uchaguzi zianzie ngazi ya Mahakama ya Mwanzo kabla ya kufika kwenye Mahakama ya Wilaya. Hii yote ni kuwapa nafasi wadau ambao wanaweza kupeleka malalamiko yao katika Mahakama ya Mwanzo na kusikilizwa na kupatiwa ufumbuzi wa kesi zinazohusu uchaguzi katika *level* ya kata.

Mheshimiwa Spika, pia katika Muswada ambao unahusu Uchaguzi wa Urais, Wabunge na Madiwani; unaweza ukaona katika Ibara ya 20 na 21, unaweza kuona hata upatikanaji wa kadi ya kupigia kura tumeondoa tozo; mpiga kura atapata kadi ya kupigia kura bure, hakuna malipo yoyote na hata ikipotea anaweza kupata nyingine bure.

Mheshimiwa Spika, unaweza kuona muswada huu ulivyo rafiki kwa wapiga kura, ulivyo rafiki kwa Watanzania, kumwondolea gharama ambazo mpiga kura haitaji kuzibeba. Miswada hii yote inahusu masuala ya uchaguzi wa sisi wanasiasa, kwa sababu ninaamini Watanzania walio wengi ukiwauliza watasema hii miswada ni ya vyama vya wanasiasa sio masuala ya siasa. Wenyewe watakuuliza habari ya sukari kupanda bei ishuke, watakwambia wapate umeme wa uhakika, watakwambia wapate barabara bora, wapate shule nzuri. Hayo ndiyo masuala ya Watanzania. Lakini haya masuala ya miswada ni masuala mazima ya uchaguzi, na sisi wanasiasa ndio tunatumia fursa hii ya kuhakikisha tunapita salama kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuleta zoezi hili. Wao wanasema wanataka katiba mpya. Kama wanataka katiba mpya tafsiri yake tuwaulize je, wako tayari watupe tena muda wa miaka mitatu bila uchaguzi wa mwaka 2024 na 2025 tuanze mchakato wa kutengeneza katiba mpya, je, Watanzania wako tayari? Kama hawako tayari maana yake tunatengeneza muswada huu ili tuvuke kwenye uchaguzi wa mwaka 2024 na uchaguzi wa mwaka 2025. Halafu tukishavuka kwenye uchaguzi wa mwaka 2024 na mwaka 2025 ndipo tutakuja sasa tuzungumze habari ya kutengeneza katiba, kwa sababu muda utakuwepo wa kutosha, elimu itakuwepo ya kutosha, Watanzania watashiriki wengi na masuala mengine yataweza kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Watanzania wapokee hii Miswada mitatu ili tuweze kushiriki kwenye uchaguzi tukiwa wa moja, tukiwa na amani na tukiwa na usalama.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo ambayo nimeweza kupata nafasi ya kuchangia ninaomba kuwasilisha, pia nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwa siku ya leo. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuruhusu mjadala huu uweze kujadiliwa ndani ya Bunge lako, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza ajiandae.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye sheria hizi muhimu ambazo ziko ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika miswada yote mitatu ya sheria kadri ambavyo muda wangu utaniruhusu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kama ambavyo wengi wamesema, nitumie nafasi hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na Amir Jeshi Mkuu wa Nchi yetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninampongeza kwa sababu gani? Miswada ambayo leo iko mbele ya Bunge lako Tukufu imekuwa ni kilio cha muda mrefu cha Watanzania walio wengi, iImekuwa ni kilio cha wanasiasa na imekuwa ni kilio cha wanademokrasia na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Rais amekwenda kujibu kilio hicho kupitia miswada hii ya Serikali, Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri sana kupitia Serikali yake. Hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesoma Miswada yote mitatu. Msingi wa Miswada hii, kwanza imelenga kulinda usawa wa kijinsia kati ya mtoto wa kike na wa kiume lakini dhana ya pili ya Miswada hii imelenga kupanua dhana ya demokrasia, umoja wa kitaifa na ustawi wa nchi yetu. Jambo la tatu Miswada hii imelenga kufanya kwa vitendo na kudhihirisha dhahiri kwamba Mheshimiwa Rais anatembea katika maneno yake. Madam *President is walking on her talk. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amesema anaamini katika *4Rs*, *Reconciliation, Resilience, Reforms* na *Rebuilding*. Ukisoma Sheria hizi unaona dhamira njema ya Mheshimiwa Rais ya kuliweka Taifa pamoja. Na kwa sababu sheria hizi zimelenga

kuleta umoja na utulivu wa kitaifa ni kwa msingi huo mimi kama Mbunge ninaunga mkono asilimia mia moja Miswada hii ya Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono maoni ya Kamati ya Utawala Katiba na Sheria ambayo yamesomwa vizuri sana na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama. Pamoja na kuunga mkono maoni hayo, naomba kuboresha maeneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza, nataka niweke msingi ndani ya Bunge lako. Nikiwa kama kiongozi wa kitaifa ninafahamu nchi nyingi za Afrika na nchi nyingi za dunia za ulimwengu wa tatu zimekuwa na ugumu wa kuelewa maana ya msingi wa jinsia na hii imetokana na historia ya jamii zetu za kidunia.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba kusema maneno yafuatayo; mtu pekee anayeweza kupinga au kubisha kuhusu usawa wa kijinsia ni yule ambaye hajazaliwa na mwanamke. Lakini, kama umezaliwa na mwanamke, kama unaye mtoto wa kike, kama unao dada zako, kama umekaa kwenye tumbo la mwanamke kwa miezi tisa, umekula chakula kupitia tumbo la mwanamke huna sababu ya kupinga usawa wa kijinsia katika jamii zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, tangu jana Waheshimiwa Wabunge wengi ndani ya Bunge lako wamesema, wakisisitiza uwepo wa usawa wa kijinsia katika vyombo vya maamuzi ili wanawake na wanaume washiriki vizuri kwenye kufanya maamuzi ya nchi yao. Nimesoma taarifa ya Kamati ya Bunge ya Utawala, Sheria na Katiba, kwenye Ibara ya 69 Kamati imesema vizuri kwamba inapendekeza kuanzishwa kifungu kipya kinachosema unyanyasaji wa kijinsia na ukatili wa kijinsia liwe ni kosa la kiuchaguzi. Na nimekwenda kusoma kwenye Jedwali la Marekebisho la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Kifungu hicho ambacho kinapendekezwa kimewekwa kwenye Kifungu cha 135, kifungu hiki kinaanzisha ukatili wa kijinsia kama kosa la jinai na sio kama kosa la kiuchaguzi. Hapa naomba mnisikilize vizuri; tusipoliweka vizuri jambo hili kelele zote za

kupigania usawa wa kijinsia tutakuwa tumetwanga maji kwenye kinu.

Mheshimiwa Spika, wanachokiongea Wabunge kosa la ukatili wa kijinsia liwe kosa la kiuchaguzi siyo tu liwe kosa la jinai, sasa kwenye Sheria yetu ya Uchaguzi, ukienda kwenye Sura ya Saba ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sura ya Saba ndiko ambako inaanzisha makosa ya kiuchaguzi. Kwa maana hiyo, ninalishauri Bunge lako Tukufu kosa hili la unyanyasaji na ukatili wa kijinsia pamoja na kwamba limewekea Kifungu kipya cha 135 pia yafanyike mabadiliko kwenye makosa ya kiuchaguzi kwenye Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, ikikaa hivyo tutakuwa tumejibu kilio cha watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vema jamii ikajua tunapozungumza usawa wa Kijinsia, hatuzungumzi kumtetea mtoto wa kike peke yake. Juzi Mheshimiwa Rais wakati akihutubia kwenye hafla ya kumuingiza kazini Askofu wa KKKT Dkt. Alex Malasusa alisema jambo moja kubwa sana, alisema zaidi ya asilimia 60 ya vijana wa Kitanzania ambao wana sifa ya kuoa hawajaoa. Tafsiri yake ni nini? Wapo wanawake pia kwa asilimia hiyo hawajaolewa.

Mheshimiwa Spika, kwenye chaguzi tunajua, vijana wengi tuko humu ndani, ukigombea kijana hujaolewa ama hujaoa unaambiwa hufai kuwa kiongozi katika nchi hii. Uwe wa kike au wa kiume, Mgombea anapoenda kwenye jukwaa anamshambulia mtoto wa kike au wa kiume eti kwa sababu hana ndoa. Tunataka Watoto wa Kitanzania washindane kwenye chaguzi kwa hoja na siyo kwa sababu ya maumbile yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapotetea jinsia na mtoto wa kike, mimi nina mtoto wa kike lakini pia mimi ninaye dada yangu na Wabunge wengi humu ndani mnao ndugu wa kike, Sheria hii Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania angekuwa hana dhamira njema ya kulisaidia Taifa angeweza kuacha kwa sababu yeye amekwishakuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria hii inaletwa Bungeni kufanya *reform* ya kitaifa, ninawasihi Waheshimiwa Wabunge mlioko ndani ya Bunge hili tulichukue jambo hili katika mtanzamo chanya. Sioni kwa nini Watanzania wawe na hofu ya usawa wa kijinsia, sisi Taifa ambalo tumeonja na kupata fursa ya kuongozwa na mwanamke, tumeona raha na faida ya kuongozwa na mtoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu mko ndani ya Bunge hili, mnatokea kwenye Majimbo yenu, tuseme ukweli Rais Dkt. Samia amepeleka miradi kwenye Vijiji na Kata ambazo hakujawahi kuwa na miradi. Amepeleka Shule kwenye vijiji ambavyo hakujawahi kuwa na Shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Majimbo yetu kwa mara ya kwanza kazi zimekuwa nyingi kuliko wakandarasi, nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? Hilo halitoshi pale Mbeya walifanya majaribio ya kumchagua mwanamke kuwa Mbunge wao kwa mara ya kwanza Mbeya wanapata mikopo ya bodaboda kwa Tulia *Trust*. Kama hilo halitoshi tumechagua mwanamke kuwa Mbunge amekuwa Rais wa *IPU* duniani. Tuna sababu gani ya kuogopa usawa wa kijinsia katika Taifa letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mdogo, Mimi katika familia tuko watoto watano, mtoto mmoja ni wa kike Dada yangu anaitwa Leina Enosy Swalle, sisi watoto wa kiume wote hatujawahi kufikiria kupeleka umeme nyumbani, kwa mara ya kwanza mtoto wa kike Dada yangu alifunga umeme wa *solar* nyumbani. Waheshimiwa Wabunge, hatuna sababu tena ya kuogopa kuweka usawa wa kijinsia katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakuomba sana kwa kuwa tunazungumzia usawa wa kijinsia, alisema jana Wakili Edward Olelekaita ndani ya Bunge lako tusiruhusu tena kutunga sheria isiyokuwa na jicho la kijinsia. Pia, ninakuomba Spika tunazo Kanuni zako za Bunge hapa ndani za kuhusu Wenyeviti wa Kamati, ikikupendeza tufanye marekebisho pia kwenye zile Kanuni, Mwenyekiti akiwa (KE) Makamu anakuwa (ME). Mimi ni Mjumbe

wa Kamati yako ya Kanuni za Bunge, ukiita kikao hicho mimi sihitaji posho kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme pia kidogo kuhusu hofu ya vyama vya upinzani. Nimesikia mjadala kuhusu hofu ya uteuzi wa Wajumbe wa Tume. Hatuwezi kupata Tume Huru nje ya watu ambao tunao kama jamii. Nimesoma kwenye hii taarifa ya Kamati ya Bunge na bahati nzuri Mheshimiwa Jenista Mhagama kwenye jedwali lao wamekubali wanapendekeza kwenye Kifungu cha 102 kwamba wakala wa kila chama kwenye kila kituo cha uchaguzi atapewa fomu yake ya matokeo. Kila wakala wa chama kwenye kituo cha uchaguzi atapewa nakala yake ya matokeo ya uchaguzi. Tafsiri yake ni nini? Kila mgombea atakuwa na matokeo mkononi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Tume haitakutangaza, Mahakama zipo utashinda. Tumeshuhudia vyama vyote vimekwenda mahakamani vimeshinda kwenye kesi za uchaguzi, kwa hiyo, hofu ya nani ameteuliwa hii siyo hoja ya msingi, ninawasihi Watanzania tujipange kushiriki uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nataka nitumie nafasi hii kuwapongeza timu ya wanawake wa UWT Taifa, kwa mara ya kwanza tangu nimezaliwa, nimeona wanawake wa UWT wakisimama kidete kupigania haki za wanawake wa Tanzania bila kujali vyama vyao. Ninakuomba Mheshimiwa Mary Pius Chatanda na timu yako ya akina Hawa Ghasia na Mama yangu Mlezi wa CCM Mkoa wa Njombe, Mama Halima Mamuya, kazi hii ya kupigania wanawake endeleeni nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako wanawake kwenye vyama vya siasa wanateseka sana na wanawake wengine wako ndani ya Bunge hili wamepigania vyama vyao kwa damu na jasho, leo wanaitwa *Covid-19*. Ninawasihi wanawake wote wa Tanzania wajiunge na UWT kutetea haki zao za msingi hapa nchini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pia natoa wito kwa Chama cha CHADEMA kama hakijui maana ya maridhiano kijifunze kwa

jemedari Samia Suluhu Hassan. Huwezi kwenye Sheria kuna kitu kinaitwa *when you come to equity, come with clean hands.* Hawa wenzetu wanapigania maridhiano, hivi wanajua maana ya maridhiano? Wamekanyaga haki za wanawake miaka minne sasa, kwa nini wanashindwa kuridhiana kwenye Chama chao wasamehe wanawake hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kuwasihi UWT tembeeni kifua mbele, teteeni wanawake wa vyama vyote nchini ikiwemo wanawake wa CHADEMA, *ACT* na kadhalika. Kwa kufanya hivyo, mtakuwa mmetenda haki kwa kizazi hiki na kizazi kijacho. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsanteni sana. Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnesta Lumbert Kaiza, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii nzuri uliyonipatia ya kuchangia katika miswada hii mitatu. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii ya pekee ambayo anatupatia sasa ya kutoa michango yetu kwa ajili ya haki na miswada hii ambayo itaenda kuiendesha nchi yetu kwa miaka kadhaa hapa.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maono makubwa ya Falsafa ya *4R*, wote tutakumbuka kwamba kumekuwa na falsafa ya Mheshimiwa Rais, hata ukifungua kwenye mitandao utaona wameandika *4R Samia's Philosophy* (Falsafa ya Mheshimiwa Rais). Aliongelea Habari ya *reconciliation* ambayo ni maridhiano, akaongelea habari ya *resilience* ustahimilivu, akaongelea habari ya *reform* ambayo ni mageuzi na *rebuilding* ambayo ni kujenga upya. Kila mmoja haya anayajua na yamesemwa nafikiri kuanzia jana tunaendelea kuyasema hadi leo.

Mheshimiwa Spika, ninampomngeza Mheshimiwa Rais kwa maono haya makubwa na falsafa hii kubwa ambayo itandelea kuwepo ndani ya nchi yetu na itafanya tufikie maridhiano,

ustahimilivu, mageuzi na baadaye kujenga pale panapokuwa pameharibika.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu Dada yangu Jenista Mhagama na Msaidizi wake ambao nawaona wanaendelea kupiga makofi pale. Ninampongeza sana ndugu yangu Mwenyekiti wangu wa zamani kidogo Mhagama, kwa kazi kubwa aliyoifanya ya *presentation* hapa. Tumesikia mambo mengi na tumepitishwa katika miswada yote mitatu na mimi kama Mtanzania na Mwakilishi wa watu wa Busanda, nimeridhika kwamba miswada hii inaweza kwenda kuwa sheria kwa ajili ya kuanza kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kabla sijasemi mengi kwamba wawe sehemu ya kuunga hoja ili kuhakikisha kwamba tunafanikiwa katika hili kwa sababu nchi yetu ilikuwa na ombwe la haya ambayo tunayasema, tunatakiwa sasa kulijaza ili kuhakikisha kwamba tunakwenda kwenye ukamilifu wa utekelezaji wa sheria hizi tatu ambazo zimesemwa hapa.

Mheshimiwa Spika, nikuombe tu uniruhusu niseme maneno haya machache kama utangulizi. Tarehe 15 mpaka 17 Desemba, 2021 Mheshimiwa Rais aliita mkutano wa maridhiano hapa Dodoma na waliuita Mkutano wa wadau wa Demokrasia. Wajumbe wengi walikwenda bila kujali dini zao, vyama vyao na bila kujali makabila yao, na mwisho wa kazi hiyo kulipatikana kikosi kazi ambacho kilikuwa na watu 24, watu 16 kutoka Tanzania Bara na Nane kutoka Tanzania Visiwani, kiliandaa mapendekezo ambayo sasa tunapokwenda kwenye maridhiano ni vitu gani tunakwenda kuvifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo hayo yalipatikana mapendekezo takribani 83, katika hayo yanaonekana tayari mapendekezo 64 yamefanyiwa kazi, mapendekezo 12 yanaendelea kwenye *process* ya utekelezaji wa kufanyiwa kazi na mapendekezo yaliyobaki yanaendelea kufanyiwa kazi kwa utaratibu kwamba, kuna vitu vingine ambavyo inawezekana

vilitakiwa kuzungumziwa awali havijazungumziwa ili yaweze kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa hesabu ya kawaida hii utekelezaji wake ni zaidi ya asilimia 80. Sasa, huwezi kwa wale wenzangu waliobahatika kusoma hesabu kidogo kama umefaulu kwa asilimia 80 nafikiri hii ni "A". Kwa hiyo, niseme wazi kwamba, Mheshimiwa Rais katika maridhiano haya na utekelezaji wa Serikali ikiwemo Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria wamekwenda zaidi ya asilimia 80. Sasa, hauwezi kufika mahali hapa ukasema bado kuna mahali fulani tumeshindwa kufanya vizuri. Hii yote ni katika kutekeleza hiyo *philosophy* ya *4R*. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais katika hili kwa sababu ametutoa katika hatua moja kwenda kwenye hatua nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uniruhusu nipitie Tume ya Uchaguzi na nipitie maneno machache ambayo nitayachukua kama *quotation* kwa yale ambayo yameoneshwa kwenye Tume ya Uchaguzi. Katika Ibara ya 6 (1) imesema: Tume itakuwa ni chombo huru na kinachojitegemea na maamuzi yake hayataingiliwa na chombo chochote au kulazimika kufuata maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali au maoni maoni ya chama chochote cha siasa. Hiki ndicho kilichoandikwa hapa, kwa hiyo, tulipokuwa tunazungumza mimi nikaona niufuate muswada umeandikwa nini?

Mheshimiwa Spika, wanaposema kwamba hii Tume siyo huru ni kweli inawezekana mtu mmoja kwa mawazo yake anafikiria hivyo lakini imesemwa Tume hii itakuwa huru na ndicho ambacho tutakwenda kukizungumzia kwenye Muswada huu, sasa sijaona mashaka yako wapi. Itakuwa huru na haitaingiliwa na chombo chochote, haya ndiyo yaliyoandikwa humu.

Mheshimiwa Spika, nikaenda tena sehemu ya pili naomba nisome kuhusu sifa za Wajumbe wa Tume. Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume watapaswa kuwa ni Majaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani au kuwa na sifa ya Wakili na

amefanya kazi hizo kwa muda usiopungua miaka 15 hata kwenye Katiba imeandika hivyo.

Mheshimiwa Spika, mtu aliyefanya kazi Mahakama ya Rufani ni Wakili ambaye amefanya kazi zaidi ya miaka 15, ndiye anayetoa maamuzi ya kesi nyingi ndani ya nchi hii anakosaje kuaminika? Kama hiyo ndiyo *composition* ya Tume, hao ndiyo viongozi wake wa juu anakosaje kuaminika huyu? Kwa sababu tukishindwa hawa na hawa ndiyo wanaoitwa *learned people,* tukishindwa hawa labda tuwaombe Malaika washushwe hapa tuwape nafasi hii na hatuwezi kuwapa Malaika kazi hii, lazima tuwape hawa hawa tulionao ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo Wajumbe wengine ambao wametajwa hapa na sifa zao, awe raia wa Tanzania na vitu vingine ambavyo tumesema watapita kwenye Kamati ya usaili. Naomba niipitie Kamati ya usaili imeandikwa nini. Kamati ya usaili hii inaonesha wazi kwamba ule muundo wake ukoje.

(a) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa ni Mwenyekiti.

(b) Katika Ibara hiyo ya 9 Jaji Mkuu wa Zanzibar ambaye atakuwa ni Makamu Mwenyekiti.

(c) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora.

(d) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Mheshimiwa Rais kwa kuzingatia jinsia. Sasa hii miamba mitatu iliyotajwa pale juu tuna mashaka gani na Kamati ya usaili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora unakuwa na mashaka naye? Hawa ndiyo wanakwenda kusaili, maana yake kama tuna mashaka na hawa na sisi tutiliwe mashaka, kwa sababu kama huyu ndiye Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, hii ndiyo *composition* ya Kamati ya Usaili, ndiyo tumesema

itakwenda kutupatia sasa hawa Wajumbe ambao wametajwa hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba nirejee kwenye maneno yako kwamba, bado hatujawa na majibu sahihi ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kama watakuja kwenye Kamati ya Usaili. Japokuwa ndugu zetu wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria tayari wamekwishapendekeza kwamba ni vizuri majina yao vilevile kutoka kwenye Tume hawatasailiwa, kwa sababu kumsaili Jaji wa Mahakama ya Rufani sasa atakuwa anakwenda kwenye cheo gani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunataka tu wapendekezwe ili majina yao yapendekezwe na Mheshimiwa Rais asifanye kazi kubwa ya kuanza kutafuta hovyo hovyo, awe na watu ambao sasa hivi wamepelekwa kwamba hawa watatu wanaweza kuchaguliwa wakawa Mwenyekiti na mwingine Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilitaka kusema katika mazingira hayo tutoane hofu, tupitishe Muswada huu wa Tume Huru ya Uchaguzi ambao utatupeleka kuhakikisha kwamba, maamuzi yetu sasa ya uchaguzi yatapita kwenye Tume salama.

Mheshimiwa Spika, haya mambo yalikuwepo, ukienda kwenye Katiba ibara ya 74 utagundua haya mambo yalikuwepo. Marekebisho kadhaa ndiyo yamefanyika na ndiyo sababu tunasema tunakuja na Muswada mpya ili tuweze kuupitisha kwa ajili ya uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, katika haya machache ambayo nimeyasema hapa, nizungumzie kidogo Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Hii nayo ukisoma katika Ibara ya 6(1) ambapo ndipo mahali pamekuwa panazungumziwa sana, kwamba kwa madhumuni ya uchaguzi utafanyika chini ya Sheria hii, kila Mkurugenzi wa jiji, Mkurugenzi wa Manispaa, Mkurugenzi wa Mji na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya atakuwa Msimamizi wa Uchaguzi kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika Jimbo na Kata na msimamizi huyo wa uchaguzi anaweza kuwa Msimamizi wa Uchaguzi kwa Jimbo zaidi ya moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ndiyo kila mmoja alikuwa anajiuliza, wenzetu wamefika mahali wamekuja na wazo zuri kwamba wataweka kuwa Afisa Mwandamizi; ni kweli, lakini bado hata Mkurugenzi ni Afisa Mwandamizi. Kwa hiyo, naomba tu tuangalie vile vile kipengele kinachofuata kwenye Ibara hiyo ya 6(2) kinasema hivi; "bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha kwanza, Tume inaweza kuteua kwa kuzingatia nafasi aliyonayo mtu katika Ofisi au kwa jina kutoka miongoni mwa Watumishi wa Umma wenye sifa sawa na za Mkurugenzi aliyopewa katika kifungu kidogo cha kwanza. Idadi ya wasimamizi wa uchaguzi au wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika Jimbo na Kata." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado Tume ina *option two*, haiendi na *option* moja ambayo ndiyo kila mmoja ndio ana mashaka nayo. Wanaweza wakachagua mtu yeyote kwa jina kutoka kwenye Ofisi ya Umma. Sasa sijaona kwamba mahali hapa huu Muswada una tatizo gani? Kama 'A' umesema haifai, basi chagua 'B,' kama 'B' haifai hapa ziko *option* tatu kwenye Muswada huu, lakini nashangaa kila mmoja anaangalia *option one. Okay, option one* ina shida, tumesema Afisa Mwandamizi. *Option two,* kwa sababu hatujawekewa *restriction* kwamba lazima iwe *option one,* tunaweza kwenda kwenye *option two,* Afisa wa Umma anaweza kufika mahali akateuliwa na akafanya hii kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme Muswada huu ni mzuri, wala tusiwe na mashaka kwamba wataalamu, viongozi wa Serikali wameuleta, ukiwa umesomwa vizuri, ninaamini kabisa hakuna kinachoharibika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika sheria hii ambayo tumeizungumza, Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani na Wabunge, kuna mahali tena nilitaka nipaseme katika Ibara Na. 54. Ibara Na. 54 inasema, "endapo kutakuwa na mgombea mmoja halali wa nafasi ya Ubunge aliyeteuliwa, msimamizi wa uchaguzi atamtangaza mgombea huyo kuwa mgombea pekee wa nafasi ya Ubunge.

Mheshimiwa Spika, hili nafikiri limetolewa majibu yake Mahakamani muda siyo mrefu, kwamba tutafanya sasa badala ya kuwa na mgombea ambaye anaonekana ameshinda bila kupingwa, tutakuwa na wagombea ambao watapigiwa kura za Ndiyo na Hapana. Ukisoma hapa chini kwenye hesabu, utagundua kuna jibu la *50%+1* kwamba lazima ili wewe ushinde kura za 'Ndiyo' ziwe zaidi ya nusu za kura zilizopigwa. Kwa maana hiyo, ni *50%+1, (51%)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa Muswada huu umezingatia mambo mengi ambayo tulikuwa tunayahitaji kwenda katika kile ambacho Mahakama imesha-*rule out,* lakini katika lile ambalo sasa vilevile linatakiwa kwenye jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, ukienda Ibara namba 124 ambapo nafikiri na ndugu yangu alikuwa anapasema hapa, "Makosa Mengineyo ya Uchaguzi," hapa ndipo mahali ambapo nafikiri wengi wanasema kwamba tumetoa makosa haya ya uchaguzi tukayapeleka kwenye jinai, ukienda Polisi unaambiwa hii kesi ni ya uchaguzi, kwa hiyo, inabidi waanze uchunguzi, na inaweza ikachukua miezi mitatu wakati umeshashindwa uchaguzi mwanamke umetukanwa, au umedhalilishwa au mwanaume kadhalilishwa, bado kesi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikafikiri kwamba hapa kwenye Makosa Mengineyo ya Uchaguzi, kwenye Ibara namba 124 tuwe na nafasi ya kuweka hiki kitu. Kama kuna mahali kuna makosa ya uchaguzi yako hapa, Ibara ya 124 hapo, tuone kuna mahali gani tunaweza kuweka pamoja na hayo ambayo yameandikwa hapa. Mtu ambaye kwa kukusudia anatoa ushahidi wa uongo au maelezo ya uongo katika tamko lililotolewa chini ya kifungu Na. 87, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini. Sitaki iwe faini, ata…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, ajiandae.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami kwa uchache niweze kuchangia katika Miswada hii mitatu iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kupitia Bunge lako hili Tukufu nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uthubutu wake wa kukubali Miswada hii iweze kuletwa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema kwa uthubutu kwa sababu ni Rais wa kwanza ambaye amethubutu kukubali Miswada hii iletwe Bungeni na hatimaye tutunge sheria ambazo zitasimama kwa ajili ya demokrasia hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema nampongeza kwa sababu kwanza ni mwanamke na wanaume msini-*quote* vibaya, wengi wamepita huko ni Marais tena wale ni ma-*giant* ambao leo tunaongea kwamba waondoe mfumo dume, hatujawahi kuona Miswada ya aina hii inaletwa Bungeni kwa ajili ya kutungiwa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wakati mjumbe mwenzangu Mheshimiwa Gulamali anaanza kuchangia, alianza kwa *introduction,* na kati ya mambo ambayo aliyasema, alitolea mfano wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo jinsi ambavyo waliandamana, na akaenda mbali akasema hawakufanya jambo ambalo lilikuwa ni sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunatambua kwamba kuandamana ni takwa la kisheria. Kuandamana siyo makosa. Nilitegemea Mheshimiwa Gulamali kwanza ampongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa sababu yeye ndiye ambaye ameruhusu maandamano haya yafanyike ambayo ni ya kikatiba. Sasa hapo hatuangalii kwamba walikosea kuandamana

au hawakukosea, lakini tunaangalia ile nia njema ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuruhusu demokrasia ambayo hatujawahi ku-*experience* kwa kipindi cha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda kwenye vifungu, mimi niliwahi kuandamana wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopita na niliwahi kuandamana mara mbili. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kilichokutokea?

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, kilichonitokea anajua Mungu. Kwanza, yale maji ya washawasha yaliniwasha mpaka nikashindwa kuelewa ninakoelekea ni wapi?

Mheshimiwa Spika, wakati naandamana, maana yake hapa najitolea mfano mwenyewe, wakati naandamana, badala ya Jeshi la Polisi kutulinda, yaani wale walikuwa wanatukung'uta virungu, yaani *nding! nding!* Unapigwa mpaka unakiona cha moto.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Uchaguzi Mkuu wa 2020, mimi nilikuwa ni Mratibu Mkuu wa timu ya Mgombea Urais wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo. Nilizunguka nchi nzima. Niliyoyaona kule ndugu zangu, aisee, Mheshimiwa Rais Samia apewe maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niendelee kuchangia. Nitaanza na Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa 2023. Ibara ya 6 ya Muswada inatambua Wakurugenzi kuwa kama Wasimamizi wa Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria. Kama Wajumbe, tulikaa kwa muda wa kutosha kabisa kudadavua Ibara hii ya 6. Kabla hatujaenda kuwasikiliza wale wadau, sisi wenyewe tulijifungia kwanza kutafakari, hawa Wakurugenzi kweli wana sifa ya kusimamia uchaguzi ambao Mheshimiwa Rais kwa jinsi unavyomwona mwelekeo wake, anahitaji demokrasia, anahitaji haki kutendekeka, lakini pia

hahitaji kuona Wasimamizi wa Uchaguzi wanakuwa na upendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wajumbe kwa nia moja tulikubaliana tukasema hawa Wakurugenzi wanapaswa kutosimamia uchaguzi; kwa maana ya nafasi zao za Ukurugenzi, hawapaswi kusimamia uchaguzi. Kwa sababu uchaguzi uliopita wa 2020 tulishuhudia kwa macho jinsi ambavyo Wakurugenzi hawa waliharibu uchaguzi kabisa, kabisa, kiasi kwamba hata wale wagombea ambao walishinda kihalali, leo hii huko nje unasikia unaambiwa hukushinda, hukushinda, hukushinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe ni shahidi, pamoja na kwamba ulipambana na kupambana kuhakikisha unashinda Jimbo la Mbeya Mjini, unaweza kujikuta uko kwenye ile *pull* ya kwamba hukushinda, wakati ulishinda. Hii inatokana na nini? Inatokana na Wakurugenzi *the way* walivyoendesha uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wakati tunapokuwa tunaendelea kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa, tunaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu na Mama yetu Samia Suluhu Hassan ameonesha nia njema ya kuruhusu demokrasia…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, Uchaguzi wa mwaka 2020 ni uchaguzi kama zilivyokuwa chaguzi nyingine zilizotawaliwa na Sheria na Katiba ya nchi. Wote waliotangazwa kuwa wameshinda, walishinda kwa mujibu wa sheria na kura zilihesabiwa. Mtu ambaye hakuridhika, Sheria ile ya Uchaguzi ilikuwa inatoa mwanya wa mtu yeyote kukata rufaa kwenda Mahakamani. Uzoefu unaonesha kwamba vyama vyote;

Chama Tawala na vyama vingine viliwahi kupeleka kesi Mahakamani na waliokuwa wameshinda kwa njia zisizokuwa sahihi, chaguzi zilitenguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tukiendelea kusikia lugha ya kwamba kuna watu walishindwa lakini wakatangazwa wameshinda, huwa hizi ni *propaganda* ambazo hazina ushahidi wowote wa kisheria. Nami ningetaka kumwambia, ni vizuri tukazungumza mambo ambayo tuna uhakika nayo badala ya kuzungumza lugha ya kudhani, vinginevyo ingependeza haya mambo yakawa bayana zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa acha kutonesha vidonda! Kama umeshinda wewe…

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, utulivu muhimu. Mheshimiwa Agnesta Lambert, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, hiyo taarifa naikataa, ni kwa sababu pia namheshimu kwa umri wake. *Ningeweza kumwambia kwamba inawezekana unajitetea sana, huenda wewe ndiye mtu wa kwanza ambaye hukushinda. (Kicheko/Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Ngoja, ngoja, ngoja. Eeh, lazima mambo haya yakae sawa sawa.

Mheshimiwa Agnesta Lambert alichokisema Mheshimiwa Ole-Sendeka yuko sahihi, kwa sababu ukisema jambo kama hilo, maana yake utatakiwa ulete uthibitisho, na sidhani kama unao wa kuthibitisha kwamba Wabunge hawa waliokaa humu ndani hawakushinda. Kwa sababu hiyo, kuliko tuanze kwenda huko kwenye wewe kuleta uthibitisho ambao utakuwa huna; maana kuna kesi moja, si inajulikana jamani! Kuna kesi moja, Mbunge wa Busokelo alishitakiwa na Mahakama ikatoa uamuzi, lakini maeneo mengine sijui kama kulikuwa na kesi. Huko nako ushahidi

uliopelekwa ulionekana hautoshelezi, kwa hiyo, ndiyo maana Mbunge bado yuko humu ndani.

Sasa kwingine kote, maana yake, anachosema Mheshimiwa Ole- Sendeka ndio yuko sahihi. Kwa nini? Kwa sababu mfumo wa uchaguzi ndani ya nchi upo na Mahakama huwa unaenda kule. Maadamu hakuna walioenda ushahidi ukaonekana na uchaguzi ukatenguliwa, basi ule ndiyo utaratibu. Kwa sababu ukisisitiza maana yake sasa, kwa Kanuni zetu mimi nitataka ulete ushahidi tu. *(Makofi)*

Kukataa taarifa ni suala moja, ameendeleza baada ya kuikataa taarifa. Amesema huenda Mheshimiwa Ole-Sendeka ni kati ya hao ambao hawakushinda. Muwe mnasikiliza vizuri. Muwe mna sikiliza vizuri! Akisimama hapa akisema anataka ushahidi! Ndiyo msome Kanuni. Neno "huenda," hata mimi hapa ukinitolea mfano ukaniambia huenda, maana yake nini? Eeh, tufuate utaratibu tuliojiwekea wenyewe.

Mheshimiwa Agnesta Lambert, endelea na mchango wako.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee na mchango wangu...

**SPIKA:** Ngoja kwanza. Kumbe nimesema uendelee na mchango kabla sijafuta hayo maneno! Lazima yaondoke kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Mheshimiwa Agnesta Lambert.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, umenielekeza nifute maneno, si ndiyo!

**SPIKA:** Nimeshafuta.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunisaidia, ahsante kwa upendo wako. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Ila taarifa yake umeipokea?

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nimeikataa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mnamchanganya mchangiaji. Humu ndani kuna viti vingi viko wazi, mkiendelea hivyo itabidi nimhamishe akasimame mahali pengine ili achangie kwa uhuru. Maana sasa anabaki anawasikiliza ninyi, nimepokea, nimefanya nini, nimepokea, aah! Siyo utaratibu mzuri. Mpeni nafasi achangie ili hoja yake ikae vizuri. Mheshimiwa Agnesta Lambert. *(Makofi)*

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee. Nilikuwa bado niko kwenye hiyo Ibara ya 6 ya Muswada na nilijaribu kuelezea historia ya Wakurugenzi ili tufahamu na tuelewe ni kwa nini tunasema Wakurugenzi hawa kwa sasa, wananchi hawawezi kuwa na imani nao kulingana na historia yao ya huko nyuma. Ndiyo maana katika Taarifa yetu ya Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria tumeshauri mambo kadha wa kadha.

Mheshimiwa Spika, tumesema kwamba Tume iweze kuteua Watumishi wa Umma na wakati inateua hao Watumishi wa Umma ifanye *vetting* ya hali ya juu ya kuhakikisha hao wasimamizi ambao ni Watumishi wa Umma ni wale ambao kwanza hawana ukada kabisa wa vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu tunafahamu na tunatambua *majority* ya Wakurugenzi waliopo sasa ni wale ambao walishiriki kwenye kura za maoni. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** *Mheshimiwa Spika, nilikuwa nampa taarifa Mheshimiwa Agnesta Lambert kwa mchango wake mzuri anaoendelea nao kwamba Jimbo la Bunda Mjini mwaka 2020 Mkurugenzi wake aligombea kura za maoni Mtama akachapwa*

*na Nape akaja kunitangaza mimi, imagine. Taarifa nakupa.* **[Maneno Haya siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusiendeleze mvutano. ulitangazwa nini Mheshimiwa Ester Bulaya? Ulitangazwa nini?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** *Mheshimiwa Spika, nimesema a-imagine, yaani ndiyo anakuja aje anitangaze mimi. (Kicheko/Makofi)* **[Maneno Haya siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wewe unaongelea uchaguzi wa 2020 na nimetoka hapa kutoa maelezo mazuri kabisa. Nadhani hakuna sababu ya kuvutana kwenye hoja hii. Ama mkitaka kunyooka nayo, tunyooke nayo basi tufike mwisho. Mheshimiwa Ester Bulaya, taarifa yako futa mwenyewe. Haya futa. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, sijajua nifute kwenye kipengele kipi, maana kweli aligombea Mtama akawa…

**SPIKA:** Futa yote, kwa sababu siyo hoja ya Mheshimiwa Agnesta Lambert.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, siyo ya Wakurugenzi kumbe.

**SPIKA:** Futa taarifa yako yote kwa sababu unarejea kule nilikotoa maelezo marefu kuhusu uchaguzi wa 2020.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, sikuwepo mimi, sikukusikia.

**SPIKA:** Sasa umenisikia, futa taarifa yako mwenyewe.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, inavyokupendeza wewe.

**SPIKA:** Aah, futa mwenyewe.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, si nimesema ulivyopenda wewe nimeifuta?

**SPIKA:** Aah, futa mwenyewe. Ya Agnesta Lambert, nimefuta mie, hii futa mwenyewe. Mheshimiwa Ester Bulaya, futa taarifa yako. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Nimeshafuta! Haya *Madam*, nimefuta.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert, endelea na mchango wako.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee, lakini ikikupendeza naomba unilindie kidogo muda, maana umeenda sana.

Mheshimiwa Spika,…

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Taarifa.
**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** *Come on!*

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, taarifa. Shabiby hapa. Nipo hapa.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, niendelee?

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert…

Waheshimiwa Wabunge, hii ni taarifa ya mwisho kwa Mheshimiwa Agnesta Lambert. Mheshimiwa Shabiby.

**TAARIFA**

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, naomba mchangiaji afute kauli yake vizuri, kwa sababu amesema

kwamba anafuta jinsi ulivyomwelekeza. Sisi humu hatujashinda kwa magendo, tumeshinda kihalali, aifute vizuri hiyo kauli.

**SPIKA:** Amefuta. Amesema nafuta, kwa hiyo, hiyo inatosheleza kufuta. Mheshimiwa Agnesta Lambert, malizia mchango wako.

**MBUNGE FULANI:** Hata hajaanza amemkatiza katikati.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, mhh! yaani hata sijaanza.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema kwamba kwa kuwa Tume imetoa uhuru na Kamati imeshauri kwamba waweze kuteua Watumishi wa Umma wengine ambao watakuwa na vigezo ambavyo tumevieleza kama Kamati ili waweze kusimamia hizi chaguzi na mwisho wa siku ile nia njema ya Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan iweze kuonekana kwa matendo na siyo katika maandishi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Tume ifanye *vetting* ya kutosha ili kuwapata wasimamizi wa uchaguzi wasio na ukada kama jinsi nilivyosema pale awali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende sasa Ibara ya 10 ya Muswada. Ibara hii imeweka bayana masuala ambayo yatamuondolea mtu kupiga kura. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamtambua mahabusu pamoja na wafungwa wa makosa fulani fulani kwamba wana haki ya kupiga kura. Haijawahi kutokea hapa nchini tukaona mahabusu na wafungwa ambao wana makosa ambayo Katiba inawatambua kwamba wanaweza wakapiga kura wakiwa wanapiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa haraka nikuainishie masuala ambayo yanaweza kumkosesha mtu sifa ya kuandikishwa na kuwa mpiga kura:-

(i) Kuwa chini ya kiapo cha utii kwa nchi nyingine;

(ii) Kutokuwa na akili timamu;

(iii) Kutiwa hatiani kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifo au anatumikia kifungo cha zaidi ya miezi sita; na mwisho

(iv) Kutenda makosa ya uchaguzi na hivyo mtu huyo kupoteza sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Ibara hii utaona jinsi ambavyo mahabusu wanapaswa kupiga kura. Sasa, kwa sababu jambo hili ni geni lakini lipo Kikatiba nilikuwa nashauri kwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan nia ya Muswada huu kuuleta na kuuruhusu uje hapa Bungeni ni ili demokrasia na haki ionekane vimetendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba tunapokuwa tunaingia katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, tunapokuwa tunaingia katika Uchaguzi Mkuu wa 2025 basi mahabusu hawa ambao Katiba imewaruhusu wapige kura, tuwape haki yao ya Kikatiba waweze kupiga kura. Kwa maana nyingine wapewe haki ya kuandikishwa lakini pili waruhusiwe kupiga kura kuwachagua viongozi ambao wanaona wanafaa kuwaongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa harakaharaka nikupe mifano ya baadhi ya nchi chache kabisa ambazo waliweka Sheria hii ya mahabusu kupiga kura na sasa hivi wanaitekeleza tofauti na sisi hapa Tanzania sheria ipo lakini haitekelezekeki. Kwanza *South Africa*, mnamo mwaka 1994 walianza ku-*practice* hii sheria. Nchi ya Ghana mnamo 2010 walianza ku-*practice* hii sheria ya mahabusu kupiga kura. Kenya majirani zetu mnamo 2010 wameanza ku-*practice* moja kwa moja sheria hii ya kuwaruhusu mahabusu waweze kupiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sifa pekee inayomuondelea mahabusu kutokupiga kura ni ikiwa siyo raia wa Tanzania…

**MHE. BONIPHANCE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, basi mniacheni…

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere, Mbunge alikuwa ameshapewa taarifa tatu tayari. Mheshimiwa Agnesta Lambert

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, Ibara ya 135, wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu sisi kama Wajumbe wa Kamati tuliona kwamba ni vyema ikawepo ibara, ikawekwa sheria ambayo itakuwa ni mahususi itakayobaini kosa na adhabu kwa kosa la unyanyasaji wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamechangia sana kuhusiana na unyanyasaji wa kijnsia kwa maana ya nje, mtu umeshatoka nje kwenye uchaguzi na vitu kama hivyo. Lakini nilieleze Bunge lako Tukufu unyanyasaji wa kijinsia hauanzii nje unaanzia ndani ya vyama vyetu. Ndani ya vyama vyetu unyanyasaji wa kijinsia unaonekana moja kwa moja na hususan kipindi cha uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ambaye naongea mbele yako ni mfano unaoishi. Niligombea kura za maoni ndani ya chama changu na niliweza kushinda kura nikawapiga kwa mbali sana wanaume na nilikuwa ni mwanamke pekee yake ambaye nilishinda kura ya maoni. Hili ambalo naliongea ambalo nimelipitia lipo kwenye vyama vyote vya siasa, ndio maana nimesema tuanzie ndani halafu twende nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaposema kwamba tunataka kutengeneza au kuweka usawa wa kijinsia lazima tuangalie namna ya kuhakikisha tunatenda haki, tunaondoa unyanyasaji wa kijinsia kutoka ndani ya vyama vyetu. Mimi niloposhinda kura za maoni nilikatwa …

**SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa…

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja.

**SPIKA:** Dakika moja malizia.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilkuwa nasema kwamba kama inawezekana kuwepo utaratibu kabisa wa kupeleka kwenye vyama vyetu hivi, kwamba mfano mwanamke mimi nimepambana nimeshinda kura ya maoni, si nimewabwaga wanaume jamani? *Let me go*. Kwa nini uniweke pembeni halafu *and then* mnakuja mnatuambia nyie si wanawake mnafursa za Viti Maalum, Viti Maalum siyo hisani.

Mheshimiwa Spika, *actually*, watu huwa wanadhani kwamba kupata Ubunge wa Viti Maalum ni rahisi ni ngumu. Kumshawishi mwanamke aweze kukuchagua ni ngumu sana. Kwa hiyo, ukiona mwanamke amemshawishi mwanamke mwenzake amemchagua aisee huyo ni mwamba kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, namalizia, tunapokwenda nje sasa tupo kwenye chaguzi, unyanyasaji wa kijinsia umekithiri sana na niseme hususan kwa sisi wanawake. Unakuta unagombea jimbo, Mheshimiwa Spika umegombea, wenzangu hapa mmegombea, akinamama huko mmegombea, unyanyasaji wa maneno ya kuondolewa utu wa mwanamke imekuwa ni jambo kubwa sana na watu wanalifanya hadi ndoa za wengine zimeweza kuvunjika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakuta mimi ni mwanasiasa nina uvumilivu wa kisiasa, mume wangu anakwenda kuambiwa kwamba yule mwanamke mnayemuona pale juu anahutubia yule anatembea na wanaume 200 na wote tunawajua. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, unakuta mimi nina uvumilivu kwa sababu najua ni siasa, *what about my husband? What about my wife?* Kwa hiyo, unakuta wanawake wanashindwa kujitoa kwenda kugombea kwa kuhofia mambo mbalimbali yakiwemo masuala haya ya ndoa. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa maana hii taarifa ni ya Kamati yangu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Mhandisi Samwel Hhayuma, ajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia kwenye Miswada hii mitatu inayohusisha suala la uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameona ni muhimu suala hili likaletwa hapa Bungeni tuweze kuchakata kwa uhuru kama ambavyo tunafanya sasa. Pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, naomba nichukue nafasi hii kukupongeza sana kwa ushindi mkubwa sana ulioupata wa kuwa Rais wa *IPU*, hongera sana. Mimi tu nikukumbushe kwamba ulipokuwa kule Duniani unahangaika kutafuta kura, mimi kwa hiari yangu nilikwenda pale Mbeya Mjini, kwenye Jimbo la Mbeya Mjini nikawa mlinzi wa hiari kwenye jimbo lako mpaka uliporudi ukakuta jimbo liko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikueleza kwenye Kata Nzovwe ulikuta mambo yako safi lakini pia Isanga mambo yalikuwa safi, Mwanjerwa mambo safi, Iyunga mambo safi, Isanga mambo safi, Mwakibete mambo safi. Kwa hiyo, nikupongeze sana kwa nafasi hiyo uliyoipata na tunakuombea sana kama mwanamke mwenzetu, kwa namna hiyo tunaamini kabisa hutatuangusha kwa sababu wakati wote ulipopata nafasi katika Nchi hii ya kuongoza kwenye eneo lolote ulilopata nafasi hukutuangusha, ulifanya kazi kwa *style* ya *Standard Gauge Railway,* hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba tu nikueleze ombi maalum kutokana na kazi pia ambayo mimi niliifanya kule Mbeya naomba usinisahau katika ufalme wako. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kwa kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Dkt. Joseph Kizito Mhagama pamoja na Kamati yake kwa namna ambavyo wamefanya kazi nzuri sana ya kuchakata Miswada hii na hii imeturahisishia sana sisi hapa kuendelea kuzungumza na kuweza kutoa maoni mbalimbali. Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, popote ulipo pokea maua yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa UWT, Taifa Mama Mary Pius Chatanda kwa kazi kubwa anayoifanya ya kumuunga mkono Rais katika kutetea wanawake ambao anazungumza mara kwa mara kila mahali anakokwenda kuhusiana na masuala ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia. Tunamtakia kila la kheri yeye pamoja na Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu na *delegation* yake yote waendelee kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Katiba na Sheria lakini pia Ofisi ya Waziri Mkuu, hongereni sana kwa kazi nzuri mnayoifanya. Ni ukweli usiopingika mko vizuri mnachapa kazi barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa spika, hali kadhalika nichukue nafasi kuwapongeza Wabunge wote humu ndani, mmefanya kazi nzuri ninawapongeza kwa michango yenu yote, wale ambao wameshapata nafasi ya kuchangia. Kila anayesimama anatupa nondo zenye uhakika zimeshiba, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kwenye Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Sehemu ya pili ya Muswada huu unaainisha makosa ya uchaguzi, makosa haya ya uchaguzi yanayoainishwa hayajataja suala la ukatili wa kijinsia kuwa ni sheria kamili. Itungiwe sheria kamili ili suala hili kwa kweli liweze kuwekewa wigo mzuri na wigo mpana zaidi na kwamba unyanyasaji huu na ukatili wa kijinsia kwenye masuala ya uchaguzi umekithiri mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepata kushuhudia mwaka fulani, Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo alikuwa anagombea Udiwani kule Tukuyu. Nimeshuhudia nilikwenda kule kama mwana CCM, anatukanwa matusi makubwa makubwa ya nguoni kwenye jukwaa na viongozi wengine wa chama cha upinzani lakini watu wanacheka tu wanafurahi jambo ambalo ni uzalilishaji na ni ukatili wa kijinsia. Nataka niseme kwamba jambo hili tukiliacha liko holela holela maana yake haya yote tunayoyafanya. *(Makofi)*

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Suma Ikenda.

**TAARIFA**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, anachosema Mheshimiwa Jacqueline Msongozi ni kweli. Kipindi cha kampeni ile nilidhalilishwa sana, kwenye mkutano ule wa chama cha upinzani alikuwepo hata baba mkwe wangu mdogo alitaka kupanda akampige ngumi yule ambayo anadhalilisha familia yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante, nilitaka kujazia hapo kwamba ni kweli tunadhalilishwa sana wanawake tunapokuwa tunagombea kwenye majimbo, iwe kwenye kata kama nafasi za udiwani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, naipokea nilikuwepo na huyo mzee namfahamu. Kanuni za adhabu ambazo zimetajwa katika sura ya 16 haina kosa mahususi ambayo inatajwa pale inayohusisha suala la ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa kijinsia kwenye masuala ya uchaguzi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme iko haja na ni muhimu sana, niungane na Wabunge wenzangu wote ambao wamezungumzia kwamba ni lazima tuweke sheria hii itajwe moja kwa moja na yule atakayevunja sheria hii maana yake achukuliwe hatua ikiwa pamoja na kupata kifundo na adhabu nyingine kadhaa wakadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria hii hali kadhalika haijataja unyanyasaji wa kijinsia kwenye masuala ya uchaguzi hasa kwenye makosa ya uchaguzi kwenye masuala ya mtandaoni. Tumekuwa tukinyanyasika sana, wanaume kwa wanawake kwa sababu hii haijachagua. Unyanyasaji wa kijinsia ni kwa wanaume na wanawake ambao wamekuwa wakigombea aidha wakipiga kura. Wamekuwa wakinyanyasika sana hasa kwenye kuchorwa chorwa kwenye mitandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaamka asubuhi unakuta umebebeshwa libwana hata hulijui sura yake unaambiwa kwamba huyu ndiye mume wake huyu mgombea jambo ambalo si sawa, haifai kabisa, hatujafika hatua hiyo katika nchi yetu, tunaongozwa na mila na desturi za Nchi yetu. Kwa hiyo, ni lazima tuweke misingi mizuri ya kuheshimiana hata wakati tunapokuwa na uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchaguzi usiondoe amani, uchaguzi usijaze masuala ya kudharauliana na hata tukakuta hata tunashindwa kuheshimiana, amani ikatoweka eti kwa sababu tu ya uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie kwenye sheria hiyo hiyo, nataka niseme wanawake waliowengi wanakuwa sasa hivi wakipungua sana kwenye kugombea lakini siyo tu kwenye kugombea nafasi mbalimbali lakini pia hata ushiriki wao kwenye kampeni. Kwenye mikutano ya kampeni pia wamepungua kwa sababu wanapoenda kwenye mkutano wanaambiwa mbona yule mgombea ni chakula yake, mbona huyu hivi, mbona huyu hivi. Kwa hiyo, haya masuala yamekuwa yakichafua jamii kiasi ambacho sasa wanawake

wamekuwa waoga wanarudi nyuma hawawezi kujitokeza kindaki ndaki kwenda kugombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie kwamba kwa nini tunasema hii sheria iwepo na itiliwe mkazo iwe sheria kamili ni kwa sababu tumeona hata ndani ya Bunge hili wanawake wengi wananyanyasika humu ndani lakini pia nasema hivyo kwa sababu mimi mwenyewe ni mhanga. Unaweza ukapita tu sehemu kwenye jimbo fulani, ukatembea tu hivi unavuta hewa ya Mwenyezi Mungu tayari. Asubuhi unabatiziwa maneno, asubuhi umejaziwa vitu, kesho yake umejaziwa vitu, sasa hii siyo sawa lazima tuweke sheria madhubuti ambayo itadhibiti hivyo vitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine tunao humu ndani, wako wenzetu humu ndani ambao ni Wabunge wenzetu wameingia humu kutokana na Chama cha Demokrasia na Maendeleo lakini wamekuwa wakinyanyaswa. Wamekuwa wakinyanyaswa na kupewa majina yasiyokuwa na haki katika haki za binadamu. Mtu unaitwa *Covid -19* ukijua ule ugonjwa wa *Covid–19* ni ugonjwa hatari na aliyetaja hilo jina na kueleza mpaka kwenye vyombo vya habari yuko tu mtaani anaendelea kutembea huko hakuna chochote anafanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama tuna nia thabiti ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais ni vizuri tukuhakikisha kwamba…

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**TAARIFA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Msongozi Ngonyani kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, nataka tu nimpe taarifa mzungumzaji kwamba pamoja na yote bado tupo imara sana.

**SPIKA:** Sasa nilikuwa natafakari hapa kama aliyeimara ni ninyi ama kuna mtu mwingine ambaye yupo imara. Mheshimiwa Jacqueline Msongozi unapokea taarifa hiyo. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, huyo aliyenipa taarifa aliwahi kuwekwa ndani kwa muda usiojulikana, kwa muda mrefu. Amekaa magereza huyo Mheshimiwa Nusrat lakini pia Mheshimiwa Agnesta na yeye amepata mateso, Mheshimiwa Esther Matiko, wote hawa ni watu ambao ni viongozi wazuri wanataka kuvunja ile *image* ya wanawake kufanya kazi na kuweza kuongoza katika Nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunataka tuwaambie kwamba wanawake tuko imara na tutasimama ipasavyo kuhakikisha kwamba tunasimama bila kutetereka tukimuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu, kuhakikisha kwamba tutagombea nafasi mbalimbali hatutarudi nyuma na hatutarudishwa nyuma eti kwa sababu ya hoja ya vitisho na mambo mengine kadhaa wa kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa kuhusu uanzishwaji wa dawati la kijinsia. Nipongeze sana huu mpango, kwa sababu utasaidia kupunguza changamoto zinazojitokeza wakati wa uchaguzi. Kwa hiyo, naomba nipongeze sana namna ambavyo wenzetu wameona huu umuhimu wa kuweka suala hilo la dawati la kijinsia lakini pia kwenye suala la Sheria ya Uteuzi. Tunaomba sasa kwenye hii Sheria ya Uteuzi vyama vyote itungwe sheria mahusus ya kuwafanya vyama vyote waweze kuzingatia uteuzi wa kijinsia kwa maana ya *gender balance* kwamba wanawake na wanaume uteuzi wao uweze kuwa na uwiano ambao utakuwa ni uwiano mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitaka niliseme ni kwamba, tunao hapa ma-*senior* wetu ambao wamepita katika mchakato wa ukatili wa kijinsia. Wako akina Mheshimiwa Dada Jenista hawa, kufika hapo si kazi ndogo, wamekutana na mambo ya *up and down* kwenye unyanyasaji wa kijinsia. Akina Mheshimiwa *Engineer* Manyanya wako humu; si kwamba wako

humu kipole pole, wamekutana na hivyo vitu. Mheshimiwa Agness Hokororo wamepitia vitu kama hivyo, mimi mwenyewe halikadhalika, Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ametoa ushuhuda hapa jana. Kwa hiyo ni lazima tuhakikishe kwamba tunaweka sheria ambayo itasimama imara kutokomeza ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, nikwambie kitu; *incase* kama wakakamatwa watu wawili, watatu wanaonyanyasa kupitia mitandao, wanaonyanyasa kwa matusi ya hadharani; lakini pia wakikamatwa na wakapewa adhabu wanayostahili huo unyanyasaji utapungua kwa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusisahau kwamba inawezekana kabisa mgombea akawa na wapambe wake huko nyuma, akawa anawatuma ndio wanaenda kukutengeneza kikatuni, ndio wanaenda kutukana matusi asubuhi mchana na jioni, ndio wanafanya hicho na kila kitu; mimi naomba itakapobainika hawa ni wapambe wa fulani; lakini pia ikibainika kwamba mgombea fulani ndiyo anafanya hiyo kazi; hao nao mgombea wao aondolewe kwenye mchakato wa uchaguzi lakini na wapambe wake wapate adhabu ikiwa ni pamoja na kifungo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka tu niseme kwamba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, wapo akina Mheshimiwa Munde hao wamepitia mambo makubwa, Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata huyu hapa amepata shida kweli kweli ananisimulia kila siku mpaka natoa mchozi. Amekutana na mambo mazito ya kukata na shoka.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi, Mungu akujalie kila la kheri lakini pia usinisahau katika ufalme wako kama nilivyoomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na Mungu akubariki sana; naunga mkono hoja. *(Makofi/Vicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Samweli Hhayuma.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hii miswada mitatu ambayo imeletwa mbele yetu kuhusiana na Sheria ya Tume ya Uchaguzi, Sheria ya Vyama vya Siasa pamoja na Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge pamoja na Madiwani.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitangulie kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo ameifanya ambayo imeweza kutufikisha mahali hapa. Mheshimiwa Rais kwa hakika anastahili pongezi kubwa kwa sababu ameyafanya mambo ambayo yalishindikana kwa miaka 62 ya Uhuru wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesomewa taarifa hapa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, mtani wangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, ikieleza kwa uwazi juhudi ambazo zimefanywa na Mheshimiwa Rais ndani ya utawala wake. Na ametohoa kabisa kuanzia siku ile alipokuja kutoa hotuba hapa ndani ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 22 Aprili, 2021; alieleza nia ya dhati na akaahidi kwamba atasimamia na kuilinda amani na utulivu wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa moja kati ya misingi muhimu ya kuilinda amani, umoja na mshikamano wa nchi yetu ni pamoja na kuboresha hizi sheria ambazo leo miswada yake imeletwa hapa. Kama hiyo haitoshi, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alikaa na viongozi wa vyama vya siasa, jambo ambalo kwa miaka mingi lilikuwa halijafanyika. Viongozi wa vyama vyote 19 walishirikishwa. Pia alikaa na wadau zaidi ya 300 kujadili mustakabali wa nchi yetu na kuona wapi tunakosea, wapi tunaweka mambo sawa sawa. Mkutano ule wa wadau ulitengeneza kikosi kazi ambacho kilikwenda kufanyia kazi mambo mbalimbali ambayo yalionekana yanatatiza Taifa letu,

na kukaonekana kwamba kuna mapendekezo 83 yalipendekezwa na kile kikosi kazi. Kati ya hayo tayari Mheshimiwa Rais wetu ameshayasimamia na kutatua changamoto 64 zilizoainishwa na kile kikosi kazi. Zimebaki 19 tu na ambazo ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais anastahili pongezi za dhati kabisa kwa kusimamia huu mchakato ambao tunaendelea nao hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia wadau walitoa mapendekezo kwamba Muswada wa Sheria uwasilishwe hapa Bungeni pasi na kuletwa kwa hati ya dharura. Leo tumeona, kwa sababu hilo wazo lilitolewa mwezi Septemba; mwezi Novemba tayari likawa limeletwa mezani hapa Bungeni, na leo mwezi Januari tunajadili Muswada huu na ambao ndani ya muda mfupi tutapata majibu na ifikapo kesho kutwa mambo yatakwenda sawa sawa. Kwa hiyo mama yetu anastahili pongezi kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, mtani wangu Mheshimiwa Dada Jenista Mhagama, lakini pia na Naibu wake Mheshimiwa Ummy Nderinango; Nderiananga, samahani, kumradhi; Kiswahili, ulimi hauna mfupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza mtani wangu mwingine Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa namna ambavyo wameweza kusimamia vizuri hii miswada mpaka imeweza kufika hapa ikiwa na mambo mengi mazuri ambayo yataweza kulijenga Taifa letu na kuleta maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niende moja kwa moja kwenye suala lile la jinsia. Sipendi kuongelea kwa kirefu sana kwa sababu Wabunge wengi waliochangia kati ya jana mpaka leo wamechangia kwa kiwango toshelevu sana. Lakini kweli kuna shida ya msingi kubwa ambayo inatatiza katika Taifa letu ya unyanyasaji hasa kwa wanawake, lakini pia hata kwa akina baba katika baadhi ya maeneo. Kwa hiyo kuwepo kwa sheria ambayo inakwenda kukataza inakwenda kuwa na katazo la unyanyasaji

wa kijinsia pamoja na kuweka bayana masuala ya kijinsia yanavyoweza kutumika katika vyama vyetu vya siasa ni jambo jema sana na ambalo litatatua changamoto nyingi sana. Kwa hiyo naipongeza Kamati, naipongeza Serikali kwa kuliona hilo.

Mheshimiwa Spika, na mimi niseme au nitolee mfano; wapo watu jana hapa walitolea mifano katika nchi mbalimbali ambazo tunaziona kwamba zina *best practice* katika demokrasia iliyokomaa duniani ikionyesha kwamba walikaa kwa miaka mingi sana kukiwa hakutolewi haki hata ya kupiga kura kwa wanawake. Kule Uingereza historia inaonyesha kwamba Taifa la Uingereza liliumbwa kuwa dola au dola yake iliundwa mwaka 934; na walikaa mpaka mwaka 1928 ndipo ambapo walianza wanawake kupiga kura. Lakini katika kipindi kile kulitokea Malkia watatu wanawake waliwahi kuongoza nchi ile au Dola ile ya Uingereza lakini na wao walilazimika kutopiga kura pamoja na kwamba walikuwa Malkia.

Mheshimiwa Spika, Malkia Caroline mwaka 1820 hadi 1821 alitawala dola ya Uingereza. Malkia Victoria, Malkia mwenye sifa nyingi sana duniani mpaka jina lake limenasibishwa na maziwa, maporomoko ya maji na kadhalika alitawala kwa miaka 64 kati ya mwaka 1837 hadi 1901 lakini hakuweza kuondoa hiyo sheria. Pia hata Malkia *Mary of Teck* naye alitawala kati ya mwaka 1910 hadi mwaka 1936. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaona kwamba Uongozi wa Dola ya Uingereza ulipitia miaka 83 ikiwa inatawaliwa na wanawake lakini walishindwa kurekebisha kasoro zilizokuwepo. Hapa ndipo tunapoiona nia ya dhati ya uzalendo na ushupavu alionao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha kwamba anafanya nchi yetu iendeshwe kiusawa na kuweza kutimiza ile dhana ya asilimia 50 kwa 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi napongeza Kamati, napongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri waliyoifanya. Ni imani yangu kwamba haya maboresho ambayo yanakwenda kutatua hii changamoto ya unyanyasaji wa kijinsia yataweza

kutupeleka mbele na kuweza kufikia malengo ambayo tumejiwekea.

Mheshimiwa Spika, niseme sasa, kuna mambo ya unyanyasaji ambayo yanatokea wakati wa mchakato wa uchaguzi. Ningeomba haya yashughulikiwe kipindi kile kile cha uchaguzi. Sisi wengine tumepitia katika masuala ya michezo. Kule kwenye mpira wa miguu kuna kitu tunaita *law of the game* (sheria zile 17 za mpira). Pale ni *referee* ndani ya mchezo ule ule anakupiga *red card* kama umefanya kosa la *red card,* anakupiga *yellow card* kama kuna kosa la *yellow card,* na vinginevyo vyovyote itakavyoonekana inafaa lakini ni ndani ya mchezo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo twende kwa utaratibu ule. Yale makosa ambayo yatajitokeza ya unyanyasaji ndani ya kipindi cha uchaguzi basi mamlaka tuone namna ambavyo tutarekebisha hizi sheria au kanuni zake ziweze kutoa adhabu kipindi kile kile; lakini kwa yale makosa ambayo yatatokea nje ya taratibu za uchaguzi basi hayo ndiyo sasa yaweze kuchukuliwa hatua zile ambazo zinaendana na sheria, yaani mahakamani na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza ni kuhusu Sheria Na. 6 ambayo ilikuwa inafanyiwa marekebisho badala ya kusoma kwamba Wakurugenzi watasimamia chaguzi katika ngazi ya majimbo na kata, sasa inasoma kwamba watumishi wa umma waandamizi. Mimi nasema hili ni jambo jema, kwa sababu kwanza inaondoa ile dhana ya mashaka ambayo watu wengi hasa wanaharakati mbalimbali walikuwa wakilalamika. Japokuwa katika *case of appeal* ambayo ilifunguliwa na Serikali Mahakama ya Rufaa Serikali ilishinda. Serikali ikashinda tena kwenye Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni yale ya maridhiano *under* zile *4R* ninafikiri ni busara imeletwa hii Sheria. Kuna haya mabadiliko ya kutambua kwamba wasimamizi wawe watumishi wa umma na waandamizi nafikiri ni jambo jema kabisa na linaondoa zile *doubts.* Sasa mtu akipigwa wala asije tena

kulalamika hapa kwa sababu mambo yamewekwa sawa sasa hivi, na hii itaboresha demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niseme, kuna suala la mchakato wenyewe kwanza kwenye Tume ya Uchaguzi. Tumeona kwamba mabadiliko ya sheria kupitia hii miswada hasa Muswada huu wa Tume ya Uchaguzi imeanzisha Kamati ya Usahili kwa ajili ya wale Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi. Hili ni jambo jema; na hapo ndiyo unaweza ukaona dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais katika kuboresha maendeleo na mchakato mzima wa demokrasia.

Mheshimiwa Spika, kutakuwa na Kamati ya Usahili itasahili watu lakini mwisho wa siku atapelekewa kwa ajili ya *final appointment,* kama ambavyo pia Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi na Makamu wake watakavyopatikana. Ni kwamba sasa amejivua yale mamlaka ya moja kwa moja kuweza kuteua na tayari wapo watu watakuwa wanamsaidia kuchakata lile zoezi na hatimaye kuweza kuondoa zile *doubts* ambazo zilikuwa zinalalamikiwa na wanaharakati wengi. Leo sasa tutaweza kupata angalau mchakato ambao unaanza baadaye yeye anamaliza kwa kuteua wale Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti lakini pia ile Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, tumeona kuna mabadiliko pale kwenye Kamati ya kumshauri, pale ambapo itaonekana kwamba kuna Mjumbe pengine anatakiwa aondolewe Mheshimiwa Rais hatomwondoa tu moja kwa moja na badala yake kutakuwa na kamati ndogo ambayo itafanya kazi ya kumshauri baada ya kuwa wamechakata madhaifu yake au yale mapungufu ambayo yanamtoa kwenye kuwa katika Kamati au Tume ile ya Uchaguzi. Kwa hiyo hili ni jambo jema na linaondoa zile *doubts* ambazo wanaharakati wengi walikuwa wanazishughulikia na itaboresha demokrasia. Kwa hiyo ninapendekeza hilo jambo tukubaliane kama Wabunge tuweze kulipitisha ili hatimaye hii miswada iweze kuwa sheria kamili.

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala la Sheria Na. 18 ambayo inaonyesha kwamba hata Mkurugenzi naye atapendekezwa na

Tume. Baada ya Tume kuchaguliwa au kuteuliwa itakaa na kuweza kutoa mapendekezo kwa Mheshimiwa Rais ili Mkurugenzi yule sasa aweze kuwa *appointed.* Nalo ni jambo jema na litakuwa limetuweka sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la sheria zilizounganishwa. Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani na Sheria ya Uchaguzi wa Rais na Wabunge (Sheria Na. 292 na Sheria Na. 343). Kwa wakati tulionao nafikiri ni sahihi kuweza kuziunganisha. Kule tulikotoka chaguzi za madiwani zilikuwa zinatangulia mwaka mmoja kabla ya chaguzi za Rais na Wabunge; kwa hiyo kwa sasa chaguzi zote zinafanyika pamoja, hakuna sababu ya kuendelea kuwa na sheria tofauti wakati chaguzi zote zinafanyika kwa wakati mmoja. Kwa hiyo ni jambo la busara mimi naliunga mkono kwa asilimia 100…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili ilishagonga Mheshimiwa.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema naunga mkono hoja na ninaomba Wabunge wengine tuunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana; Mheshimiwa Mhandisi Samweli Hhayuma.

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kuwa kunipa nafasi ya mimi pia kuchangia Muswada ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia, na kwa sababu ndiyo nasimama kwa mara ya kwanza kuchangia kwenye Bunge hili baada ya changamoto tuliyopata kwenye Wilaya yetu ya Hanang ya maporomoko ya Mlima Hanang ambao ulishusha udongo, mawe na magogo, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wakati tumepata changamoto tulikuwa kama tumekata tamaa, lakini Mheshimiwa

Rais alikuwa nje ya nchi akaielekeza Serikali yote iangalie Hanang na kwa kweli Serikali ilifanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku ya tarehe 3 ambako tulipata changamoto tulimpokea Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu Mheshimiwa Jenista Mhagama; muda mchache tukampokea Waziri Mkuu na Serikali yote ikahamia Hanang na ikawa ndiyo tumaini letu na kwa kweli changamoto ile ilikuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Baada ya changamoto ile wao kuiona tu nilipokea *message* nyingi sana kama Mbunge mwenzao, nilipokea simu nyingi sana kama Mbunge mwenzao, lakini wewe ulikuja mbio ulikuja na magari mengi ya msaada, Wana-Hanang walihesabu walishindwa. Ule ulikuwa ni mkono wa Wabunge wenzetu kuja kuiangalia Hanang. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipokea misaada na usaidizi kutoka taasisi mbalimbali. Taasisi za dini lakini pia asasi mbalimbali zilitukimbilia. Changamoto ile ilikuwa kubwa, tulikuwa kama tumetaka kukata tamaa lakini kwa sababu Watanzania tu wamoja; Rais wetu alisisimua na kuamsha ile ari ya umoja wetu. Kwa kweli tulipata matumaini mapema na mpaka sasa naweza kusema kwa uhakika kabisa kwamba Wana-Hanang matumaini yao yamekuwa makubwa zaidi na wanaendelea kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yamefanyika mengi, zilikuja Wizara takriban zote. Pale tulipokuwa na shida ya chakula Waziri wa Kilimo alikuwepo. Mheshimiwa Waziri wa Madini tulitembea naye ili kutathmini ile miamba ambayo imeleta changamoto na yeye alipata changamoto alizama kwenye matope yale na karibu *size* ya kiuno. Maana yake ni kwamba Serikali yote ilihamia pale. Tunasema ahsanteni sana kwa ule mwitikio ambao umepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isitoshe Mheshimiwa Rais aliahidi wale waathirika wote ambao nyumba zao zilibomoka Serikali

itawajengea nyumba. Lakini hivi karibuni pia Shirika letu la *Red Cross* ambaye Rais wake ni Mheshimiwa Kihenzile nayo iliahidi kuunga juhudi za Mheshimiwa Rais kwa kujenga nyumba 35. Juhudi hizi Watanzania wengi wameziunga mkono tunasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kwenye eneo hilo niendelee kuomba kwamba Wilaya ya Hanang miundombinu mingi imeharibika; ya barabara, ya maji lakini pia hata upande wa umeme, hasa maeneo yale yanayozunguka Mlima Hanang. Pia tuna changamoto ya upande wa mawasiliano maeneo mengi yameguswa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali isichoke kuja kuendelea kutuangalia na kutupa upendeleo wa kipekee ili tuhakikishe kwamba Hanang tunairudisha ilipokuwa lakini pia ianze maendeleo kama ambavyo tulivyokuwa tumeipangia. Baada ya kusema hayo nijaribu kuchangia kwenye Miswada ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, Miswada hii kama Wabunge wenzangu walivyotangulia kusema imetokana na nia nzuri ya Mheshimiwa Rais kuiongoza nchi yetu kwa kushirikisha kila mmoja wetu. Mheshimiwa Rais alikuja na falsafa ya *4R* wenzangu wamesema sana sitaki kuirudia. Hiyo falsafa ya *4R* ikaja ikazaa kikosi kazi, kikosi kazi hiki kikaja na mapendekezo ambapo 64 yamefanyiwa kazi kwa Daraja A kama Mheshimiwa Magessa alivyosema maana yake ni kazi kubwa imefanyika.

Mheshimiwa Spika, hii iliwasilishwa Mwezi Septemba Mwaka 2023 kwenye Baraza la Vyama vya Siasa ambapo vyama vyote vyenye usajili wa kudumu vilishiriki. Nashawishika kwamba baada ya kuwa wameona wasilisho la Serikali nia ya Rais na Serikali yake wakati ilipoalikwa watu kutoa maoni yao watu wengi walishiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipata ushiriki mkubwa na niwapongeze wote ambao wameshiriki nikianza na Baraza la Maaskofu Tanzania la Wakatoliki – *TEC* ambapo iliwasilishwa na Askofu wa

Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Askofu Yuda Thadeus Ruwa'ichi. Jumuiya ya Wakristu iliwakilishwa na Askofu Mstaafu wa Kanisa Kuu la Kilutheri Tanzania, Askofu Shoo, Baraza la Jumuiya ya Kiislamu nalo liliwakilishwa lakini pia Jumuiya ya Baraza Kuu la Kiislam nao walishiriki wakiwakilishwa na Sheikh Mussa Yussuf Kundecha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zilishiriki taasisi na asasi zaidi ya 31 kwa kuwasilisha kwa kuongea lakini maoni ya maandishi yalipokelewa zaidi ya 400. Watanzania mbalimbali, mtu mmoja mmoja watu zaidi ya 1700 walishiriki kwenye zoezi hili la kupokea maoni ya wadau mbalimbali. Wingi huu wa watu unaonesha kwamba sheria hii ilikuwa na umuhimu mkubwa kwa nchi yetu katika kuhakikisha kwamba masuala yote ya kijamii yanashughulikiwa vizuri, masuala ya kisiasa yanashughulikiwa vizuri na masuala ya kiuchumi. Uchumi wa mtu mmoja mmoja na uchumi wa Taifa yanakuwa yanashughulikiiwa vizuri na sheria hizi.

Mheshimiwa Spika, hii inaonesha kwamba jamii ya Watanzania wanaimani kubwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ukiona kwamba Rais anakubali mamlaka amepewa kwa mujibu wa sheria ya kutengeneza Tume ya Uchaguzi kwa maana ya kuteua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 74, lakini yeye ameruhusu mchakato kwenye eneo hilo kwenye sheria tunayoitunga kwenye kifungu cha tisa cha sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, huu ni utayari wa kipekee ni nia ya Rais ya kwamba kila mtu aweze kutoa maoni yake kila mtu aweze kushiriki na kujenga imani kwa Watanzania kwamba nchi hii ni ya kwetu sote tushiriki kwa kuijenga. Kila mtu atoe mchango wake kila mtu aone namna ambavyo anafaa kushiriki.

Mheshimiwa Spika, bila Rais angekuwa hana nia ya kuwashirikisha na asingetoa nafasi hiyo ya kidemokrasia angeweza kuamua kufanya shughuli kama ilivyo kawaida. Hii baada ya kuwa mapendekezo yale yametolewa kwamba sheria hizi ziende Bungeni na ziende haraka na zisipite njia ya kwenda

kwa dharura. Maana yake ni kwamba kila mtu wazo lake lilichukuliwa.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa Tanzania ni ya Watanzania, maoni yametolewa ya wengi na kila mtu anatazama jambo kwa jinsi anavyoona. Tuko zaidi ya milioni 61, haiwezekani wazo la kila mtu likawa ndiyo sahihi lazima utafute wastani wa Mawazo ili kuhakikisha kwamba kwa pamoja tufikie *consensus* ya kuamua mambo yetu. Hili ndilo lililofanyika na haya yaliyo mbele yetu ni baada ya mchakato huo kuwa umepita sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Watanzania wenzangu si kwamba tu kila jambo ambalo umeona wewe halikufurahishi ukataka lisiwafurahishe Watanzania milioni 61. Jambo litakalo kufurahisha siyo lazima liwafurahishe Watanzania milioni 61. Maana yake ni kwamba lazima tupeane nafasi ili nchi hii iendelee kustawi kiuchumi, kisiasa na kijamii. Tukipeana nafasi nafasi hivyo kila mtu atapata haki yake na kila mtu atatimiza wajibu wake hatimaye tutachangia mchango unaostahili kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya ambayo nilikuwa nimepanga kuyaongea jioni hii. Naomba nisisitize tunayoyafanya leo ni kwa ajili ya Watanzania wote. Tuko hapa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuliochaguliwa na Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka kwenye majimbo yetu. Wale ni watu halali ni wawakilishi halali wa Watanzania Mheshimiwa Rais amepatikana baada ya uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, mambo yote yanayofanyika ni kwa nia njema ya kuiendeleza nchi yetu. Hakuna jambo lolote ambalo linafanyika ndani ya Bunge hili ambalo si maslahi ya Watanzania kwani sote ni Watanzania na tunasimama kwa ajili ya Watanzania. Naiwakilisha Hanang lakini majimbo mengine pia yapo. Tukiwa na maoni tofauti lazima tuvumiliane ili nchi yetu iende mbele na lazima tufikie *consensus* kama nilivyotangulia kusema hapo awali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo naunga mkono miswada iliyo mbele yetu na hatimaye

nawaomba Wabunge wenzangu tuunge mkono nchi yetu iende mbele. Taratibu zilizopendekezwa za masuala ya uchaguzi. Masuala ya uongozi wa vyama vya siasa tuweze kuyapeleka mbele ili Watanzania waweze kunufaika na kupata haki yao stahiki ya kuchagua na kuchaguliwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge majina niliyokuwa nayo hapa walioomba kuchangia kwa siku ya leo yamekwisha na kwa hivyo tutaishia hapa. Wengine watakaokuwa wanataka kuchangia wataanza kesho lakini wale wa leo orodha yao imekamilika.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.10 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 1 Februari, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*